

## **Book Publisher:**

Remili Enterprises Company  
P.O. Box 2311, Ihila Street Buhongwa Mwanza, Tanzania.  
Phone: +255 767 285 417; +255 753 455 574  
Email: [venerandojmilinga@rocketmail.com](mailto:venerandojmilinga@rocketmail.com)

## **Printed in Tanzania 2014**

**First Print:** 50 copies

**Second Print:** 2000 copies

**ONYO:** Haki zote za kitabu hiki zimehifadhiwa kwa mujibu wa sheria ya haki miliki. Hairuhusiwi kuchapisha kitabu hiki, kukinakiri kwa namna yoyote ile, hairuhusiwi kikitangaza wala kukisambaza popote bila idhini ya mwandishi au msambazaji wake Remili Enterprises Company.

**Book Editor:** Jacob K.Tunga

Front and Back Cover designed by: Juma V. Milinga



**ISBN 978-9987- 9797-1-4**

---

*Mbinu za kupata Pesa nyingi hadi kuwa Bilionea, 2014*

## **YALIYOMO**

YALIYOMO .....	ii
SHUKRANI .....	iii
UTANGULIZI .....	iv
UJUMBE WA MWANDISHI .....	v

## **SURA YA KWANZA1**

VYANZO VYA UMASIKINI TANZANIA .....	1
-------------------------------------	---

## **SURA YA PILI**

MIRADI 66 INAYOWEZA KUKULETEA PESA NYINGI HADİ KUWA BILIONEA .....	19
---	----

## **SURA YA TATU**

MAMBO 34 AMBAYO NI MWIKO KWA MATAJIRI .....	88
---	----

## **SURA YA NNE**

MBINU ZA KUPATA MTAJI .....	108
-----------------------------	-----

## **SURA YA TANO**

MAWAZO POTOFU KUHUSU PESA NA UTAJIRI MKUBWA .....	121
---	-----

HITIMISHO .....	130
-----------------	-----

REJEA .....	134
-------------	-----

## **SHUKRANI**

Natoa shukrani tele kwa Mungu muumba wa Mbingu na Nchi aliyenijalia kukamilisha utungaji wa kitabu hiki kizuri kikiwa cha kwanza maishani mwangu. Natoa shukrani kwa familia yangu; mke wangu Regina na watoto wangu Happiness na Neema kwa jinsi walivyonyumilia kwa muda wote nikiwa natayarisha upatikanaji wa kitabu hiki. Hii ni pamoja na Janeth na Wema binti ninaowalea nyumbani kwa jinsi walivyokuwa faraja kwa familia yote wakati wote wa kuandika kitabu hiki. Namshukuru sana rafiki yangu Jacob Kalenzi Tunga kwa kuhariri kitabu hiki chote kabla ya kuchapishwa. Mwisho Nawashukuru wote waliohusika kwa namna moja ama nyingine kuhakikisha kitabu hiki kinachapishwa na kuanza kusambazwa sokoni.

## **UTANGULIZI**

Hongera sana kwa Kununua kitabu hiki. Kwa Kununua Kitabu hiki umechagua kuwa tajiri, tena bilionea. Umeamua kuwa bilionea Kwa bei ndogo tu.

Kitabu hiki kinaeleza orodha ya mawazo au miradi 65 ambayo ukiitekeleza hakika unaondoka kwenye ukurasa wa watu fukara na maskini milele. Kitabu kinataja kwa mifano hai na kwa mchanganuo unaoelewaka. Miradi sahihi na makini ambayo ina mifano na mahesabu rahisi kueleweka imefafanuliwa kwa upana. Ukisoma kitabu hiki utataka uwe unakirudia mara kwa mara kukisoma kwani Hakichoshi kusoma.

Vyanzo vikuu vya umasikini Tanzania vinavyowafanya wengi wasiweze kujinasua katika tope zito la umasikini vimefanuliwa kwa upana. Sababu kama vile Uvivu wa Kufikiri, kupenda starehe, kuchelewa kuamka, elimu mbovu, malezi mabaya, nk; vimechambuliwa kwa kina sana.

Sura ya mwisho inafafanua mbinu ambazo matajiri wakubwa huzitumia ili kupata mitaji wanayotaka. Mbinu hizo zimedadavuliwa vyema na hakika ukizisoma utapata mbinu sahihi za kupata mtaji wa mradi wowote unaoutafuta.

Aidha, miiko zaidi ya kumi inayowapasa kufuatwa na mtu ye yeyote anayetaka kuendelea kuwa tajiri na bilionea maisha yake yote imefafanuliwa ili kutorudi nyuma tena kifedha na kafilisika. Ukikiuka miiko hiyo, hakika hautachelewa kafilisika kabisa.

## **UJUMBE WA MWANDISHI**

Kwanza, Hongera kwa Kununua kitabu hiki. Nakuhakikishia kwamba ukikisoma kitabu chote hiki, hakika utaweza kuondoka kwenye umaskini si zaidi ya miaka mitano kuanzia sasa. Baada ya miaka kumi au chini ya hapo utakuwa bilionea. Wewe amini tu na uanze kazi kwa vitendo kama inavyoelezwa ndani ya kitabu hiki. Naamini kwamba baada ya kupata mbinu za kujipatia Utajiri Usiofilisika milele ndani ya kitabu hiki, ni dhahiri hautafilisika kamwe.

Kwa kusoma kitabu hiki Nakuahidi Kwamba huwezi kubakia masikini. kitabu hiki ni lazima ukisome ili uwe siyo milionea tu bali bilionea mkubwa Tanzania. Huwezi kusoma kitabu hiki usiwe bilionea kamwe!!!

## **SURA YA KWANZA**

### **VYANZO VYA UMASIKINI TANZANIA**

Kuna sababu nyingi sana hapa Tanzania za kwa nini watanzania ni masikini sana ikilinganishwa na mataifa mengine kama yale ya Asia, Amerika na Ulaya. Kwa uchache nitaeleza vyanzo vipatavyo kumi na nne (14) ambavyo mimi naviona kama vikwazo vya watu kupiga hatua za maendeleo Tanzania:

#### **Chanzo Na. 01: Uvivu wa Kufikiri**

Ukiongea na watanzania walio wengi kote vijijini na mijini, utaona kwamba kila mtu anatamani kuwa na maisha bora. Hakuna anayeridhika na hali duni aliyonayo. Hata hivyo pamoja na rasilimali nyingi zilizopo kila kona ya nchi, bado watanzania wengi wanaishi maisha duni kifedha, kiuchumi na kifikra. Kwa mfano, Umewahi kujiuliza tangu umezaliwa na kumaliza shule ya msingi umewahi kupata kiasi gani cha pesa mikononi mwako? Umewahi kujiuliza pesa zote ulizowahi kupata ziko wapi? Je, umewahi kujiuliza kwa nini hauna pesa za kutosha mahitaji yako yote kwa Mwaka mzima? Umewahi kujiuliza ni kwa nini baadhi ya miezi hauna pesa mfukoni mwako? Kwa nini umeshindwa kuwasaidia wazazi wako watoke katika umasikini wakati wamekusomesha ili uwe mkombozi wao kiuchumi? Umewahi kujiuliza ni lini ndugu zako wataondoka kwenye tope la ukosefu wa pesa za kuwatoa kwenye tope la ufukara? Unajiuliza ni kwa nini hautajiriki? Unajiuliza kwa nini wewe huwezi kulipa hata karo za watoto wako shuleni?

Kwa sababu ya uvivu wa kufikiri maswali kama hayo hapo juu, watu wengi huendelea kuzama kwenye ufukara. Kwa kutowaza kwa kina ili kupata majibu kwa kina ya maswali kama hayo, watu wengi huendelea kufungwa akili zao na fikra hata wasione fursa zilizopo kandokando yao. Watanzania wengi tuna uvivu wa kuwaza kwa kina ili kupata jawabu la maswali yao, wanalazimika kumtupia lawama Mungu kwamba yote ni mapenzi yake Mungu. Ukweli ni kwamba kutokuwaza kunaendelea kuleta ufukara zaidi. Watanzania wengi tuna uvivu wa kuwaza kwa kina, hatutaki kufikiri sana, hatuna muda wa kutafakari hadi jawabu lipatikane, huwa hatuchambui maswala. Huwa hatudadavui na kupekeua hoja na maswala ya muhimu

yanayoweza kuleta jawabu la maendeleo ya mtu, familia na taifa lote. Hali hii ni moja ya sababu kuu za ufukara mkubwa kuendelea mionganini mwa watanzania asilimia kubwa na hivyo idadi ya watu mafukara imeendelea kuongezeka kila siku Tanzania.

Sio kwamba watanzania hatuna akili kama nchi nyngi zilizopiga hatua kimaendeleo, la hasha. Akili nyngi za kuzaliwa nazo tunazo. Lakini watanzania wengi akili zetu ni kama zimefungwa na shuka au blanketi fulani na hivyo hatuwezi kujiondoa kwenye umasikini hata kama tungepewa lundo la pesa kila upande. Dawa pekee ya kuufuta umaskini Tanzania ni kubadilisha tabia yetu ya uvivu wa kufikiri. Tunapaswa kufikiri ni jinsi gani tuweze kuwa na pesa nyngi hadi kuwa mabilionea.

Tunapaswa kuvuta taswira ya mbali zaidi kuelekea kumiliki pesa na uchumi hadi tuweze kuwa mabilionea. Tunapaswa kuwaza sana jinsi ya kutatua matatizo yetu. Waza jinsi ya kuondoa kero za watu ambapo kwa kufanya hivyo utapata mabilioni ya pesa. Mashuka au mablanketi yaliyofunga akili na fikra zetu yataadondoka chini. Dawa pekee ya kufuta ufukara kwa familia yako na wewe mwenyewe ni kuhakikisha kwamba uvivu wa kuijuliza maswali mengi kwako ni mwiko. Kutafakari kwa kina na kufikiri mpaka jibu lipatikane ndio mwarobaini wa ufukara wa nchi zetu. Misaada ya kifedha na mikopo bila kuwaza na kufikiri sana chanzo cha tatizo la ufukara wetu haitakuwa suluhisho. Nakusihu wewe leo uanze kuijuliza chanzo cha umaskini wako mpaka ukipate, na ukikipata ujiulize namna ya kukiiondoa jiulize zaidi hadi upate jawabu la kukuiondoa kwenye tope la umasikini.

## **Chanzo Na. 02: Malezi Mabaya**

Sababu nyingine ya ufukara wa watanzania inatokana na malezi katika familia zetu. Malezi tuliyopewa yana nafasi kubwa ya kutufanya kuwa matajiri au mafukara maisha yetu yote. Malezi tuliyopewa tangu utotoni ndiyo yanatufanya tuwe na falsafa za maisha tuyatakayo. Huwezi kuwaza kumiliki utajiri mkubwa wakati hukuwahi kuwaona wazazi wako wakimiliki utajiri mkubwa. Kama wazazi hawajawahi kukuambia kwamba utajiri ni haki yako, hhuwezi kuwa tajiri. Malezi ya wazazi na walezi wengi huwafanya watoto wao waendelee kuwa na fikra tegemezi. Fikra mgando za watoto hutokana na fikra mgando za wazazi. Fikra na malezi yenye mwelekeo wa kujitegemea kifedha na kujiondoa kwenye umaskini ndiyo dawa pekee ya kuwafanya watoto wetu wasiwe na fikra zilizogandana.

Mzazi epuka kuwalea watoto kwa kuwadekeza sana kiakili na kimawazo. Wapo wazazi au walezi ambao huwakataza watoto wao hata kuosha vyombo vy ya nyumbani, huwakataza hata kuteka maji bombani au kisimani, huwakataza kufua nguo zao, huwakataza kupika chakula, huwakataza kufanya usafi majumbani mwao kama vile kudeki nyumba au kufagia uwanja wa nyumbani eti kwa sababu tu wameajiri mfanyakazi wa kufanya kazi zote hizo. Mfano kama huo ni chanzo cha kuwafanya watoto wetu wasiweze hata kuwaza. Mtoto hawezi kuwaza kwa sababu hana jambo la kufanya awapo likizo nyumbani kwa wazazi. Siku atakapoanza maisha ya kujitegemea atakuwa anasubiri watu wengine wawaze kwa niaba yake. Hata akipewa kuongoza watu au shirika la umma au binafsi atashindwa kabisa kuwa mbunifu. Atakuwa mtu mwenye utegemezi kifikra kwa sababu hakulelewa kwenye mazingira ya kuwaza bali alilelewa kwenye mazingira ya utegemezi kwa kufanyiwa kila jambo. Huu ni ujinga uliomo kwa wazazi wengi wa kisasa. Kumbuka kuwa kuwalea watoto wako hivyo ni kujenga taifa la wavivu wa kazi na mafukara.

Aidha, malezi ya wazazi wengi Tanzania hayamwandai mtoto kuwa mjasiriamali bali yanamwandaa mtoto kuwa na utegemezi wa kifikra, kifedha na kiuchumi. Wazazi na walezi wengi hawawalei watoto wao kwa mtazamo wa kuwawezesha wajitegemee baadaye kifedha badala yake

huwalea katika mwelekeo wa utegemezi wa kudumu kifikra na kiakili. Utasikia mzazi anamhamasisha mtoto, "soma sana uje uwe mwalimu" au "mwanangu nataka usome sana ili uje kuwa daktari". Kauli kama hizi ni nzuri sana kwa watoto wetu lakini tukumbuke pia kuwa zinawafanya wasiwe na fikra chanya kumiliki makampuni yao binafisi ya uwekezaji na biashara. Wao ndoto zao zitakuwa ni kuajiriwa tu badala ya kujijiri. Sisemi kwamba kuajiriwa ni vibaya, ninachosisitiza hapa ni kwamba malezi kama hayo hayasadidii watoto wetu kwa baadaye kuweza kumiliki uchumi na kuwa na utayari kisaikolojia wa kumiliki pesa nydingi sana na hatimaye kuwawezesha kuwa mamilionea na mabilionea. Mzazi unapaswa kumwandaa kisaikolojia mtoto wako wa kike au wa kiume kumiliki utajiri mkubwa na pesa nydingi. Mweleze mtoto wako kwamba anatakiwa asome sana ili aweze baadaye kumiliki makampuni yake binafsi yenyenye kumiliki utajiri mkubwa wa mabilioni ya pesa kama Bill Gates wa Marekani au kama Reginald Mengi wa Tanzania anayemiliki makampuni mengi sana yanayompa mabilioni ya pesa kwa mwezi.

### **Chanzo Na. 03: Elimu tegemezi**

Chanzo kingine cha umaskini wa watu wengi ni aina ya elimu wapatayo mashulenii na vyuoni. Asilimia kubwa ya vijana hufundishwa kuajiriwa na si kujijiri. Walimu wengi utawakuta wanakazana kuwafundisha wanafunzi wao jinsi ya kufaulu mitihani ya mwisho ya shule au chuo. Lengo kuu mara nydingi linakuwa kuwawezesha wanafunzi wao wafaulu mitihani na kisha wakaajiriwe na serikali au makampuni au mashirika ya umma.

Ni walimu wachache sana shuleni na vyuoni ambao huwafundisha na kuwahamasisha wanafunzi wao wakajitegemee kwa kuanzisha makampuni yao binafsi ya biashara, uzalishaji na kilimo. Kwa mfano; wanafunzi wanaohitimu kozi za Ualimu wote wameambiwa na kuaminishwa kwamba wakihitimu tu ajira ziko nje nje. Wanaohitimu kozi za Udaktari, Uuguzi, Kilimo, Uhandisi, Uhasibu, Uandishi wa habari, Masoko, n.k wengi wao wanapohitimu huzunguka huku na kule wakitafuta ajira. Huzunguka kila ofisi wakiuliza kazi ya kuajiriwa. Wanatembea na vyeti vyao mkononi kwenye bahasha za kaki wakitafuta mtu awape kazi. Wanazunguka mwaka wa kwanza, wa pili hadi wa tano wakitafuta ajira. Badala ya kuzunguka

huku na kule kutafuta uzoefu, ujuzi na mitaji; wao huzunguka kutafuta ajira.

Sababu kama hiyo ni mionganini mwa vyanzo vyatatu kuzidi kuwa na umaskini. Umaskini wa fikra. Umaskini wa kuwaza. Elimu itolewayo katika shule zetu Tanzania haimchochei mwanafunzi kujiajiri mwenyewe kwenye kampuni yake binafsi iwe ya kilimo, ufundi, huduma, nk. Wakufunzi wa vyuo na shule hawafundishi wanafunzi wao mbinu za kujiajiri. Hawafundishi wanafunzi mbinu za kuuteka utajiri uliopo Tanzania. Hawafundishi watu jinsi ya kuumiliki uchumi mkubwa. Mtu anayeajiri akiwa amehitimu shahada ya kwanza au ya pili anaonekana kama anatafuta pesa ya kula tu. Wengi mtaani wanassema "kuganga njaa". Marafiki, Jama na ndugu zake watamsimanga, walimu wake waliomfundisha watamshangaa kwa nini hajapata ajira, wanachuo wenzake nao pia, na jamii yote inamtazama kama mtu ambaye bado hajapata mwelekeo. Hali hii huwakatisha tamaa ya kujiajiri vijana wengi wanaohitimu shule na vyuo nchini. Wengi hulazimika kuanza kusaka ajira hata kama itawachukua miaka 5 wakiwa wanatafuta ajira na kujikuta wanabakia kuwa maskini kifedha na kiuchumi.

Suluhisho kwa tatizo hili ni kubadilisha mitaala ya shule na vyo vyetu nchini kuanzia shule za awali, shule za msingi mpaka vyuo vyote vyatatu ya juu. Watoto kuanzia shule za awali mpaka vyuo vikuu wafundishwe kujitegemea, wafundishwe kujiajiri, wafundishwe kuanzisha makampuni yao binafsi, wafundishwe uzuri wa kujiajiri wenyewe kwenye kampuni zao, waone fahari kumiliki uchumi wao wenyewe kupitia makampuni yao; wazazi na serikali waendelee kuwawezesha na kuwahamasisha vijana kumiliki makampuni yao ya biashara, kilimo, uhandisi, mafuta, gesi, usafirishaji, teknolojia, n.k. Kwa kupandikiza fikra chanya kama hizi kuanzia shule za awali mpaka vyuo vikuu, watu watabadilika fikra na mitazamo, watu wataanza mapema kujiajiri, watu wataanza kuwa mamilionea wakingali vijana, watu watakimbilia kuanzaisha makampuni yao na kuweza kumiliki uchumi mkubwa. Hakuna mtu ataona fahari sana kuajiriwa akilinganisha na kujiajiri kwenye kampuni yake. Kila mtu atawaza kuwa na kampuni yake binafsi ya huduma, uzalishaji, au biashara.

## **Chanzo Na. 04: Kufanya Miradi isiyokuwa Endelevu**

Je, Umewahi kufikiria kufanya miradi itakayokunufaisha wewe mpaka wajukuu wa wajukuu zako? Je, umewahi kutafakari kwa kina na kuijiliza kama mradi huo unaoufanya hivi sasa utadumu hata kama wewe ukifariki dunia? Je, huo mradi unaoufanya kwa sasa unataka udumu kwa kipindi gani? Mwaka mmoja, miaka mitatu, miaka mitano, miaka minane, miaka kumi, miaka kumi na tano, miaka ishirini, miaka thelathini, au miaka 100? Je, watoto wako au mke/mume wako anaweza kuundelea kunufaika kifedha kwa mradi huo hata wakati utakapokuwa haupo duniani?

Maswali kama hayo ndiyo ya msingi ya kuijiliza endapo unataka uwe tajiri milionea au bilionea. Epuka tabia ya kuwa tajiri ambaye anavuma sana kwa muda na akishafariki na utajiri wake unakufa pamoja naye!!! Epuka kuanzisha miradi au biashara kwa kuiga au kufuata mkumbo wa wengine hapo ulipo. Miradi ya kuiga wenzako bila kuifanyia utafiti wala kuwa na uzoefu nayo huwa haidumu. Hakikisha kuwa kampuni yako, miradi yako au biashara yako umeielewa vizuri na kwa kina kabla ya kuanza, hakikisha umeifanyia uchunguzi, upelelezi wa kutosha na utafiti wa kutosha kabla hujaanza kutekeleza chochote. Hakikisha kwamba haufanyi miradi isiyokuwa endelevu kwa zaidi ya miaka kumi.

## **Chanzo Na.05: Kudhania kuwa Fedha ndiyo Msingi wa Maendeleo**

Hapa Tanzania, tatizo kuu la wengi kuendelea kuwa maskini siyo ukosefu wa pesa. Pesa siyo tatizo hata kidogo. Tatizo kubwa ni kufikiri vibaya kwamba pesa ndiyo kila kitu. Watu wengi hufikiri kinyume. Mathalani, Kuna watu utawasikia wakisema kwamba “sina mtaji” au utawasikia wakisema, “tatizo ni mtaji tu” au utasikia wakisema “nikipata pesa nitafanya hiki au kile”. Huku ni kufikiri kinyume na ukweli.

Tanzania yetu na duniani kote kuna pesa nyingi sana. Mabilioni ya pesa yamezagaa kila kona ya dunia. Pesa kibao zinakusubiri wewe ukazichote. Ili uzichote pesa hizo ni lazima uwe na choteo la pesa. Ili kuweza kuchota pesa nyingi ni lazima uwe na choteo kubwa. Choteo kubwa ni lazima ultengeneze wewe mwenyewe. Choteo ninalolisema hapa ni Mradi wako

endelevu, mawazo chanya uliyo nayo, kazi yako na ari yako ya kuchota pesa zitoke kule zilipo kuja kwako bila kukatika.

Hivyo basi, kama pesa ingeikuwa ni dawa ya kilajambo Tanzania, watu wake wasingegekuwa maskini kwa kiwango kama kama ilivyo sasa. Kama tatizo lingegekuwa pesa, nchi yetu ingeikuwa mbali sana kimaendeleo. Ukiufigatilia kwa mfano; tangu nchi ipate uhuru wake zaidi ya miaka 50 iliyopita, Tanzania imeshapatiwa pesa nyngi sana kama misaada na mikopo kutoka kwa nchi waitwao wahisani au washirika wa maendeleo. Lakini ukweli ni kwamba umaskini wa kipato cha pesa umeendelea kuitafuna nchi na wananchi wake karibu kila kona. Nchi za Ulaya, Amerika na Asia zimekuwa na hata leo zinaendelea kumwaga fedha nyngi Tanzania kupitia serikalini na kwenye mashirika ya kiraia (NGOs).

Pamoja pesa nyngi sana kumiminwa Tanzania zikitokea nchi wahisani, bado mabadiliko ya kiuchumi na kijamii yamekuwa hayaonekani ukilinganisha na nchi zilizokuwa sawa na Tanzania katika bara la Asia miaka ya 60 na kwa sasa zimegeuka kuwa wahisani wa Tanzania. Kwa nini Taifa halisongi mbele kifedha, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia Kama fedha ingeikuwa ndiyo dawa ya umaskini? Jibu lake kubwa ni kwamba; taifa linaumwa upungufu wa fikra sahihi. Wananchi na serikali yao wanaumwa ugonjwa wa kwa kudhani kwamba pesa ni msingi wa maendeleo.

Wanasiasa, madiwani, wabunge, mawaziri, Rais na wananchi wote wanatafuta pesa huku na kule duniani. Badala ya kutafuta mawazo endelevu na chanya wengi wanatafuta pesa kutoka mahali pasipokuwa endelevu. Wanatafuta pesa kutoka kwenye miradi isiyodumu kwa miaka mingi zaidi ya mia moja. Hata wanapogombea nafasi za uongozi ukiwasoma miyoni mwao utakuta wanasiasa hao wanatafuta pesa badala ya maendeleo endelevu. Hakuna fikra zenye kuwaza kimkakati. Wengi hawafanyi uchambuzi. Wengi wanataka miradi inayoleta pesa nyngi haraka lakini haidumu vizazi hadi vizazi. Kupanga vipaumbele endelevu na kuweza kuthubutu kutekeleza wengi hushindwa. Nchi ina upungufu wa watu makini wenye fikra makini wa kusimamia na kutathimini mipango yetu ili kuondokana na umaskini unaotukabili. Watu wengi kwenye mashirika, makampuni na serikalini huwaza kupata pesa za kula na kustarehe zaidi

kuliko kuwaza zaidi kuhusu namna ya kupiga hatua za maendeleo. Tatizo kubwa hapa ni kwamba watu wengi wana ufinyu na upungufu wa fikra endelevu. Wengi wanakuwa wagumu wa kufikiri, kupanga na kuchagua vipaumbele endelevu na siyo ufinyu wa bajeti na pesa.

Tanzania kuna upungufu wa ujasiri wa kuanza jambo hata kama jambo linawezekana na linaweza kuleta tija kifedha na kiuchumi watu hawachukui hatua kuliendea. Karibu kila mtanzania amewahi kusikia watu wakisema, "hapendwi mtu inapendwa pochi" wakiwa na maana kwamba pesa ndiyo kila kitu wanachotafuta. Kama watu wangekuwa na bidii kutafuta kazi za uzalishaji kama walivyo na bidii ya kutafuta pesa, nchi hii ingekuwa mbali sana kiuchumi na kimaendeleo. Badala ya watu kuwakuta wakitafuta kazi endelevu na za uzalishaji; wanatafuta pesa zisizokuwa endelevu na matokeo yake ni umaskini tu unaoendelea kutafuna kizazi na kizazi.

Watu wengi wanaopata pesa bila kuzifanyia kazi ya uzalishaji, huwa haidumu kwa muda mrefu. Matumizi endelevu ya pesa hiyo hayataonekana. Ndiyo maana hata watu wanaoshinda BAHATI NASIBU ya pesa nydingi ukiwafuutilia hawajaweza kupiga hatua kubwa za maendeleo pamoja na ushindi huo mkubwa wa bahati nasibu ya pesa nydingi. Kusema kwamba ukiwa na pesa unaweza kufanya lolote unalotaka ni makosa makubwa. Tanzania bado kuna watu wengi wanaamini na kudhania kwamba pesa ndio msingi wa maendeleo na kwa hiyo hushinda mitaani kutafuta pesa kwa udi na uvumba.

Ukweli ni kwamba pesa siyo msingi wa maendeleo. Msingi wa maendeleo ni kazi zenye tija kiuchumi na kifedha. Pesa hazina uwezo wa kuleta maendeleo. Watu wenye mawazo chanya ya maendeleo ndio wanaoleta maendeleo. Hivyo, usitafute pesa. Tafuta maendeleo. Tafuta fikra. Tafuta kazi yenye kuleta tija kwako na kizazi chako. Usizunguke huku na kule, nchi moja hadi nchi nydingine kutafuta pesa. Usinzunguke mtaa hadi mtaa, ofisi hadi ofisi, mtu mmoja hadi mtu mwengine eti kutafuta pesa; pesa utakazopata kamwe hazitadumu kwa mtindi huo. Utazidi kutafuta pesa badala ya pesa kukutafuta wewe. Kuzunguka huku na kule kutafuta pesa ni kukosa uelewa sahihi wa msingi wa maendeleo. Tunapaswa kuzunguka huku na kule duniani au mitaani kutafuta mawazo, ushauri, uzoefu, maoni na maelekezo ya jinsi ya kupata maendeleo na siyo kutafuta pesa.

Msingi wa maendeleo siyo pesa ni fikra chanya za kukubali maendeleo yatokee. Hata kama watu ungewapa pesa nyingi kiasi gani kama hawajawa na fikra za maendeleo na utashi kabisa wa kutaka maendeleo hayo kwa moyo wa dhati, pesa hizo kwao zitakuwa sawa na makaratasi tu.

Ukiwa na fikra chanya na ukawa na mawazo chanya ndipo utaweza kupata maendeleo. Kupata maendeleo makubwa huanzia kwenye fikra sahihi kabla ya kupata pesa. Lazima uwe na miradi sahihi ulioifanyia uchunguzi na una uhakika kwamba ukiifanya utapata pesa nyingi zaidi. Fikiria kwanza kipi unataka kufanya na kwa nini na lini unataka ukifanye, hapo hata ukipewa pesa utazielekeza kwenye mradi huo huo.

### **Chanzo Na. 06: Sheria na Sera Mbovu**

Chanzo kingine cha umasikini Tanzania, ni uwepo wa sera na sheria za nchi ambazo hazimwezeshi mtanzania mzawa. Ni rahisi kwa mwekezaji kutoka nchi za nje kupewa kitu kinaitwa “Tax Holiday”. Lakini siyo rahisi kwa mtanzania mzawa mwekezaji kupewa likizo hiyo ya kutolipa kodi kwa miaka mitano kama wapewavyo makampuni kutoka nje ya nchi. Utamaduni huu wa kuwapendelea wawekezaji wa nje kuliko wa ndani unaleta hali ya kukata tamaa na kutowashawishi wananchi wapende kulipa kodi kwani hakuna usawa. Watanzania wazawa wakianzisha kampuni au biashara hawapewi ‘Likizo ya Kodi’ hata mwaka mmoja kama ilivyo kwa wawekezaji toka nje ya nchi. Watanzania wanaowekeza katika lolote wanatakiwa kulipa kodi ya mapato mara nyingi hata kabla ya kuanza biashara yenewe. Wanatakiwa walipe kodi ya mwaka mzima kabla hawajaanza miradi au biashara. Sera kama hii, haiwezi kuwasaidia watu wengi kuingia kwenye kumiliki uchumi mkubwa.

Mfano mwingine ni ile sheria ya mafao ya uzeeni. Sheria hiyo huwawezesha viongozi wa kisiasa wamalizapo muhula wao wa kisiasa kupewa kiinua mgongo kikubwa sana pamoja na pensheni kubwa kila mwezi. Wakati mwingine hulipwa kiinua mgongo hadi zaidi ya Tshs 100,000,000 kwa kipindi cha kwa miaka 5 tu. Malipo kama haya ni tofauti na malipo ya kiinua mgongo walipwacho Wafanyakazi wa sekta nyingine kama vile; elimu, kilimo, uhasibu, udaktari, nk katika utumishi wa umma na sekta

binafsi ambapo wafanyakazi wa sekta kama hizo baada ya miaka kama 25 hadi 40 hivi wakiwa kazini ndipo wanaweza kuwa na matumaini ya kuweza kupewa kiinua mgongo kama hicho cha milioni mia moja. Kama sheria zinazosimamia malipo ya uzeeni zingekuwa za haki (fair play) na za kuzingatia haki sawa kwa wote, basi kila mwananchi anayefanya kazi kwa miaka mitano bila kujali ni kazi za kisiasa au za kitaaluma, basi sheria hiyo ilipaswa iruhusu kila mtanzania mfanyakazi apate kiinua mgongo cha Tshs 100,000,000 kwa kila miaka mitano aliyofanya kazi. Kwa mfano, kama atafaya kazi miaka 35 apewe kiiunua mgongo kama hicho kwa kila miaka mitano aliyokaa kazini yaani 35 gawanya kwa 5 mara 100,000,000. Kwa hiyo mwananchi aliyefanya kazi kwa miaka 35 ya Uuguzi, ualimu, Uhasibu au udaktari, n.k alipaswa kisheria naye alipwe kiinua mgongo cha Tshs 700,000,000 ili kuwa na uwiano sawa kisheria kwa wanasiasa na watu wanaofanya kazi za kitalaam. Kinyume chake ni kwamba, wale wanaofanya kazi za kitalaam, sheria zimekuwa haziwalindi kwenye suala la sheria za malipo ya uzeeni. Hali kama hii, inawafanya watu wengi wanapostaifu, wazidi kuwa maskini wa fedha na mali.

Sheria nyingine isiyo na usawa na inayoleta umaskini hasa kwa wazee ni ile ya mifuko ya pensheni ambayo huwafanya wazee wawe fukara sana mara wanapostaifu. Wanakuwa fukara kwa sababu pensheni wanayolipwa ni kidogo sana ikilinganishwa na pensheni wanayolipwa wastaaifu wa kisiasa. Ubaya zaidi ni kwamba pensheni hiyo wanayolipwa pamoja na kwamba ni ndogo huwa haiongezeki kila mwaka ili kuendana na mfumko wa bei na thamani ya pesa (no pension indexation) kama wanasiasa wao wanavyoongezewa pensheni zao kila mwaka wa fedha.

Wazee waliostaaifu kazi (chilia mbali wale ambao hawakuwa Wafanyakazi za kuajiriwa) wanaendelea kuwa masikini kila mwaka kwa sababu pensheni zao za kila mwezi hazongezeki kila mwaka. Kila mwaka hata mfumko wa bei ungepanda kivipi pensheni zao huwa hazongezeki hadi kifo kitakapowachukua tofauti na sheria inayosimamia pensheni kwa wanasiasa kama vile Rais, Makamu wa Rais, Mwanasheria Mkuu, Waziri Mkuu, Wakuu wa Mikoa, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, nk. Sheria yao inasema kwamba mstaifu wa cheo hicho atalipwa pensheni

isiyopungua 80% au 50% ya mshahara wa mtu aliye kwenye cheo hicho alichokuwa nacho wakati huo. Sheria kama hii, huwafanya wanasiasa waendelee kuneemeka na kustawi huku wenzao walolitumikia taifa kwa kazi za kitalaam wakiendelea kuzama katika lindi la umaskini.

Sheria nyingine mbovu ni ile ya Ndoa ya Mwaka 1971. Sheria hii inawaruhusu wasichana kuingia kwenye ndoa wakiwa bado na umri chini ya miaka 18 huku ikiwazuia wavulana kuoa wakiwa chini ya umri huo. Sheria hii inachangia kuwafanya vijana wa kike wakubaliwe na wazazi kuingia kwenye ndoa badala ya kulazimishwa kisheria kupata elimu ya juu. Wengi wanaingia kwenye ndoa wakiwa bado wadogo na kuwafanya watumbukie kwenye ufukara wa fikra na fedha.

Sheria mbovu nyingine ni ile ya magazeti ambayo hairuhusu gazeti kutoa habari ambazo zinawaudhi walioko madarakani. Hataka kama gazeti hilo litakuwa linatoa elimu ya uraia au gazeti linatoa taarifa sahihi, bado gazeti hilo chini ya sheria hiyo ya magazeti itamnyanya waziri asubuhi na kulifungia gazeti hilo labda kutokana na kuchapisha habari zisizowafurahisha wenye madaraka. Hali kama hiyo huwafanya siyo tu Wafanyakazi wa kampuni inayochapisha gazeti hilo kuwa maskini wa kipato kwani mapatao yao yote yalikuwa yaktokana na mauzo ya gazeti hilo. Siyo tu Wafanyakazi wa kampuni hiyo watajikuta wakikosa kipato, bali hata wananchi waliokuwa wakipata elimu na taarifa kutoka gazeti hilo watakosa maarifa na taarifa za maana ambazo zingewapatia ufahamu wa mambo muhimu ambayo huleta kipato

Swala lingine linaloleta umaskini ni sera mbovu ya elimu na afya Tanzania. Kwa mfano, Sera ya “kila kata iwe na shule ya sekondari” au kila kata iwe na “kituo cha Afya” haijasaidia kukuza maendeleo na badala yake sera kama hizo zimeendelea kuleta umaskini kwa vijana wanaomaliza elimu kwenye shule hizo za umma ambazo hazina viwango thabiti vyakutoa elimu yenye maana kwao kwa maendeleo yao. Shule nyingi hazina vigezo vyote vyakuitwa shule, lakini serikali imeendelea kuruhusu wazazi wapeleke watoto wao kwenye shule hizo. Asilimia kubwa ya vijana wanaomaliza kidato cha nne hawawezi kuendelea na elimu ya juu au ya ufundi kwa sababu hakuna

elimu ya maana waliyoipata shulenii. Zaidi ya 60% wanapata daraja la 4 au Sifuri kwenye matokeo ya mitihani yao ya kidato cha nne. Hii hatimaye huwafanya watumbukie kwenye umaskini zaidi kwakuwa pamoja na kuhitimu kidato cha nne kwenye shule za "kata" hawawezi kuitumia elimu hiyo kujajiri wala kusonga mbele kielimu. Serikali imeshindwa kuboresha shule za umma kama ambavyo pia imeshindwa kuboresha vituo nya afya. Vingi katika wilaya na kata nyngi vimeendelea kushindwa kuleta afya kwa wananchi na badala yake hali za afya za wengi walioko vijijini ni duni na hatimaye umaskini unazidi kuwabana walio wengi hasa vijijini.

Sheria na Sera kama hizi zimeendelea kusababisha watanzania wengi kuzama katika tope la ufukara wa fikra, afya na pesa. Wananchi wengi hawana uwezo wa kutojitegemea kifikra. Ni tegemezi sana kutokana na elimu tegemezi waliyoipata. Wanashindwa hata kubuni mbinu za kujitoa kwenye ufakara na wakapata pesa nyngi za kuwatoshha mahitaji yao na familia zao. Wengi wa wananchi hawawezi hata kuwaza au kufanya miradi ya maendeleo kwa kutegemea elimu waliyoipata mashuleni. Hii ni hatari sana.

### **Chanzo Na. 07: Ukosefu wa Wivu wa Maendeleo**

Kumbuka ili ufanikiwe kuwa na pesa nyngi sana lazima uwe na wivu wa kupata pesa nyngi. Lazima uwe na hamu na nia ya dhati ya kufanikiwa mpaka kwenye viwango nya kimataifa. Kama hauna wivu wa maendeleo, ari, nia, hamu na tama ya kufanikiwa kuwa na pesa nyngi, utaendelea kuwa fukara na maskini wa kipato. Kutokuwa na wivu wa maendeleo kwa watanzania wengi ndiko kumezifanya familia nyngi kutoinuka kutoka kwenye ufukara na umaskini. Kama utauchukia umasikini kama unavyochukia njaa ya chakula, ni wazi kabisa utajituma kwa bidii na kwa umakini mpaka utatajirika tu.

### **Chanzo Na. 08: Kutokuwa na Tabia ya Kujisomea Vitabu**

Tanzania ina wasomi wengi lakini wasiosoma. Wengi wakihitimu masomo yao hawana tena utamaduni wa kujisomea vitabu hata vile vinavyohusu taaluma zao. Wanasona sana wakiwa mashuleni au vyuoni ili waweze kufaulu mitihani yao ya shule au vyuo na waweze kujipatia vyeti vyao.

Baada ya kuhitimu shule au chuo, kujisomea tena hugeuka shubiri mwitu kwao kama siyo mwiko kwao. Kama wasomi hawasomi vitabu vyat fedha, wala majaarida ya kilimo, biashara, nk je wale amba siyo wasomi watasoma kweli?

Miradi mingi Tanzania huanza kwa kukurupuka sana. Wengi wetu hukurupuka usingizini bila kutafuta kwanza maarifa na taarifa za kutosha kuhusu miradi tunayoutaka kuufanya. Wengi kabla hawajaanza mradi wowote hawaijelimishi zaidi kuhusu mradi huo. Hawasomi hata vitabu au vijarida kuhusu mradi huo. Wengi hawasomi au kuhudhuria hata kozi ndogo zinazohusu miradi wanayotaka kuanza. Hata kama wanaweza kuhudhuria kozi hizo huwa hawaendi. Hili ni tatizo kubwa na sababu kubwa ya umasikini wa pesa nyingi kwa watanzania wengi. Haiwezekani kuendelea kama taifa au kama familia kama hatusomi vitabu vyat maendeleo, biaashara, utawala wa fedha, uchumi na ujasiriamali. Haiwezekani kamwe kuwa na pesa nyingi. Ukitaka uwe na pesa nyingi sana na uinuke kabisa toka kwenye tope la umasikini tafuta vitabu vyat matajiri walioendelea zaidi, wenye pesa nyingi, na miradi mingi mikubwa.

Soma majalida yao, ongea nao ukiweza. Ongea na watalaam wengi hasa wenye pesa nyingi zaidi kadri uwezavyo ili upate elimu na siri zaidi kuhusu miradi inayoweza kukupa pesa nyingi. Nenda ukawaulize watu wanaofanya miradi kama unayotaka ukafanye. Kwa kusoma vitabu vyao utajua kwa kina kwa nini wamefanikiwa au kwa nini hawajafanikiwa kuwa na ppesa nyingi. Ukiisoma vitabu vyat waliofanikiwa kuwa na pesa nyingi utajifunza kwa nini wameacha miradi yao au kwa nini wameshindwa kusonga mbele na miradi fulani. Kwa kusoma vitabu vyat mabilionea wenye mafanikio, utapata somo la kutumia kwenye miradi yako ili kufanya vizuri zaidi kwenye miradi yako.

Epuka kufanya makosa waliyoyafanya matajiri unaowasoma kwenye vitabu vyao. Hii haina maamba wewe hautakosea, bali ujifunze kutokana na makosa ya watu wengine. Soma sana vitabu vyat mabilionea na wewe utakuwa bilionea. Acha uvivu wa kusoma. Acha kumaliza wiki nzima bila kujisomea kitabu cha maana. Tembea kila wakati ukiwa na kitabu chenye kukupatia elimu yenye tija kiuchumi. Nunua na usome vitabu vyenye akili ya kitajiri. Nunua kitabu chenye elimu ya biashara. Nunua na usome vitabu vyenye elimu ya fedha.

Pendelea kusoma vitabu vyenye kukuelimisha kuhusu usimamizi wa fedha na miradi. Achana na tabia ya kusoma majorida au vitabu visivyokuongeza akili au udadisi. Hakikisha unasoma mawazo ya matajiri kwa kusoma vitabu vyao walivyoandika. Soma vitabu vyta ujasiriamali uwe mjasiriamali. Huwezi kamwe kufanikiwa kuwa na fedha nyingi na ukawa bilonea kama husomi vitabu vyta mabilionea.

### **Chanzo Na. 09: Kuzaliwa katika Familia Fukara**

Mtu anayezaliwa katika familia fukara yuko katika nafasi ya kuendelea kuwa fukara kama wazazi wake. Wazazi fukara watashindwa kumrithisha elimu mtoto wao ambayo ingeweza kumuondoa kwenye mzunguko wa ufukara. Elimu kama nyenzo pekee inayoweza kumtoa mtoto kwenye urithi wa ufukara kutoka kwa wazazi wake ikikosekana inamfanya mtoto huyo naye kuwa fukara na hatimaye atazaa watoto katika ufukara nao wataendelea kuishi katika ufukara na kizazi kinaendelea kuwa fukara hadi kizazi na kizazi.

Familia zenyenye hali ya ufukara wa kipato ili ziondoke kwenye shimo la ufukara ni mpaka pale serikali au taasisi za wasamaria wema zitakapojitekeza na kuwawezesha watoto wa familia hizo kupata elimu sahihi itakayowawezesha kujitaa kwenye mzunguko wa ufukara.

### **Chanzo Na. 10: Kifo cha Mapema cha Wazazi**

Wazazi wengi wanapofariki ghafula, husababisha umaskini mkubwa sana kwa watoto waliokuwa wakiwategemea kifedha na kiuchumi. Watoto kuondokewa na wazazi wakiwa hawajatimiza ndoto za watoto wao huleta umaskini kwa watoto kwani hawataweza tena kupata elimu na mahitaji waliyokuwa wakipewa na wazazi wao. Kwa hiyo vifo vyta mapema vyta wazazi ni chanzo kikubwa cha umaskini kwa watoto. Huenda watoto wakatumbukia katika shimu refu sana la umaskini.

Ni vyema wazazi wakajitahidi Kuweka miundombinu mapema itakayosaidia watoto kifedha hata kama wazazi hawapo tena. Lakini kama mzazi atafariki watoto wakiwa bado hawajamaliza hata elimu ya sekondari, hii itawafanya watoto hao kuwa mafukara sana endapo hakutakuwa na juhudii za serikali

za kuwasomesha watoto yatima au kama hawatapata mashirika hisani ya kuwaendeleza kielimu, itakuwa ndio mwisho wao kifedha na kiuchumi.

### **Chanzo Na. 11: Utamaduni wa Kuchelewa kuamka Asubuhi**

Watanzania wengi wanadhani kwamba kama umejajiri ndio wakati wa kwenda kazini kwa muda unaoutaka. Hili ni kosa kubwa sana wanadolifanya wajasiriamali wengi. Utakuta watu kwenye miji mingi (niliyowahi kupita) inafika saa tatu asubuhi hawajafungua maduka yao au ofisi zao. Hii ni hatari kwa biashara yako au huduma unayoitoa. Kuchelewa kuamka na kuchelewa kufungua ofisi yako ni hasara kubwa sana. Watanzania wengi wanachelewa kuamka na wanawahi kwenda kulala. Watanzania wengi wanapenda usingizi.

Wengi hudhani kwamba kama umejajiri ndio muda mzuri wa kulala mpaka saa tatu asubuhi. Utamaduni huu wa kulala sana ni hatari kwa uchumi wa familia nyingi za kitanzania. Ukitaka kuwa na pesa nyingi kuwa milionea au bilionea lazima ukatae kulala sana usingizi.

Amka mapema na anza kazi zako mapema. Epuka kulala sana. Soma vitabu sana badala ya kunywa pombe sana jioni. Badala ya kutazama televisheni au kukesha kwenye sherehe mpaka usiku wa manane kila siku au kila wiki na kisha ukachelewa kuamka asubuhi, ni vyema ukachukua muda mrefu kujipanga na kutumia muda mwingu kufikiri zaidi jinsi ya kuendesha miradi yako na maswala muhimu ya maendeleo ya familia yako na nchi yako.

### **Chanzo Na. 12: Kupenda Kupumzika Kuliko kupenda Kazi**

Chanzo kingine cha watanzania kuendelea kuwa masikini ni utamaduni wa kupenda kupumzika na kustarehe huku wakipenda burudani kuliko kupenda kazi za kuwapatia kipato. Wapo watanzania wengi ambao kwao kazi ni kama utumwa. Wengi hawafanyi kazi kwa furaha. Wengi hawafanyi kazi kama wajibu wa mwanadamu awapo hapa duniani. Kuna watanzania wanaodhani kwamba lengo la kuishi juu ya uso wa sayari hii siyo kufanya kazi bali ni kustarehe kwenye kumbi za miziki, kumbi za sinema, vilabuni,

viwanja nya michezo mbalimbali na kwenye tafrija za kila aina. Utamaduni huu, unaendeleza ufukara wetu watanzania walio wengi.

Kuna watu wengi Tanzania ambao hawataki wajulikane wanafanya kazi gani kwa woga kwamba kazi wanazozifanya ni za aibu na hazifai hata kutajwa mbele za watu. Aidha, kuna wengine wanaona fahari kutaja wanakofanya kazi kwa sababu sehemu hizo zinasifikasi sana kwamba zina watu wenge pesa.

Utasikia watu wengi wakitaja mashirika makubwa au taasisi za fedha kama vile “....yule jamaa ana hela sana kama mfanyakazi wa TRA....” au utasikia watu wakisema kwamba huyu jamaa anahela sana kama mfanyakazi wa Benki Kuu, nk. Kwa hiyo badala ya watu kupenda kazi wanapenda starehe na kukaa raha mstarehe. Na pale wanapopata kazi hasa za kuajiriwa wanataka mishahara mikubwa sana. Watu wana mtazamo kwamba kufanya kazi ni kama laana. Kwa hiyo wanaona kwamba kazi fulani hazifai au ni za kike au za kiume na hivyo huzikwepa.

Muda mwingu watu wengi wanataka wapumzike sana. Ikifika mwisho wa wiki au siku kuu ya kupumzika kitaifa watu wanatamani wangeendelea kupumzika. Wakati huo huo, watu hao hao wanataka walipwe mishahara mikubwa na wasilipe hata kodi ikibidi. Tatizo hili kwa vijana wa kisasa ni kubwa sana. Wengi wamekumbwa sana na utamaduni huu wa kupenda kupumzika na kula burudani na starehe. Vijana wengi wanawaza kuzunguka mijini huku na kule wakienda kwenye matamasha ya muziki, wakienda kwenye disco na klubu za usiku na kwenye kumbi za starehe kwa muda mrefu bila hata kujali kama wanapoteza muda ambao kamwe hawataupata tena.

Utawakuta watanzania wengi wanapenda michezo ya kuigiza, filamu, mpira wa miguu, muziki, nyimbo, na ndivyo utakuta vimewatawala kila mahala walipo hata kwenye simu zao za mikononi, utakuta zimejaa nyimbo na muziki. Wawapo kwenye televisheni, wengi hutazama vipindi nya burudani zaidi kuliko makala za maendeleo na mengine mengi ambayo hayana tija kwa maendeleo yao. Utamaduni huu wa watanzania tusipoukataa kabisa, nchi hii haitaweza kupata maendeleo hata kwa miaka 20 ijayo itakuwa bado inazunguka pale pale kwenye tope la umaskini.

## **Chanzo Na. 13: Kupenda Ngono Sana**

Katika vitu vinavyochangia watu kutumbukia kwenye umaskini mkubwa ni pamoja na utamaduni huu ambao umechukua kasi kubwa sana siku za karibuni mionganoni mwa watanzania wa rika zote. Kupenda ngono na starehe yaweza kuwa tabia inayochangia watu wengi kuendelea kuwa maskini sana. Ukienda vijiji na mijini swala la watu kupendelea ngono limeongezeka sana. Starehe za kunywa pombe vilabuni huendana na kupenda ngono.

Watu wengi hupenda kukesha kwenye vilabu vya pombe kwa ajili ya kustarehe huku wakitafuta watu wa kufanya nao ngono. Wengine hukesha kwenye sherehe mbalimbali na kufanya ngono huko huko, Wengine hukesha kwenye ngoma za asili kama vile ngoma za mdundiko hasa mikoa ya pwani ambapo swala la ngono kutendeka wakati wa ngoma kama hizo huwa jambo la kawaida. Wengine hukaa muda mwangi kwenye fukwe bila kazi yoyote zaidi ya kwenda kutafuta watu wa kufanya nao ngono, nk. Hayo ni baadhi tu ya mambo ambayo huwafanya watanzania wengi wajikute wakibakia maskini wa kutupwa. Matendo ya kupenda kufanya ngono kila mara au kila sehemu yanaambatana na matumizi makubwa ya pesa ambapo hatimaye mhusika anaendelea kudidimia katika umaskini.

Tabia au utamaduni huu ukiendekezwa sana huwafanya watu wengi kuwa watumwa wa ngono. Hii huwafanya wengi kujikuta wakiwa hawana pesa za kuendesha starehe hizo za ngono na pombe. Watu wanaopenda ngono sana hawawezi kuwa na muda wa kutosha kufikiri kwa kina wala hawana muda wa kuwaza sana kufanya kazi za maendeleo.

Wapenzi na washabiki wa ngono hawana muda wa kufikiri kwa kina kuhusu kizazi kijacho. Wanawaza jinsi ya kupata pesa kisha wakastarehe na wapenzi wao tu. Haijalishi pesa wanazotumia kwenye starehe wamezipataje; iwe kwa wizi maofisini, ujambazi, uongo, kuuza mali haramu au bandia, wao hawajali chochote. Wanachowaza ni ngono na starehe tu. Hii ni hatari sana kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja hadi wa taifa lote kwa ujumla.

## **Chanzo Na. 14: Kuogopa Kuanza Biashara au Mradi**

Watu wengi huogopa kuanza mradi ambao wengine hawaajaanza. Wengi hujisikia faraja kuanza mradi au biashara ambayo wengine wameshaanza. Kila mtu huogopa kuanza. Anategea wengine waanze kwanza ndipo na ye ye aanze. Kuna watu wanapata wazo zuri sana la kuanza biashara au mradi fulani, lakini kwa sababu hawaoni wengine walioanza biashara hiyo au mradi huo wanaogopa kuanza. Wanaogopa kupata hasara. Utamaduni huu umezoeleka sana Tanzania kiasi kwamba mtu mmoja akianzisha mradi au biashara fulani utaona watu wengi wakiibuka kuifanya. Mtu akifungua duka la dawa mtaani, utakuta wengine wote wanaanza. Mtu akifungua huduma ya mama lishe hapa, mwininge naye anaanza jirani yake. Utamaduni huu unaendelea kuwafanya watanzania kuwa maskini kwa sababu ya woga mkubwa walionao wa kutoanza biashara au mradi mpaka pale waonapo wenzao wameanza. Jifunze kuanza wewe na wengine wakufuate. Usiogope. Anza utafanikiwa sana.

## **SURA YA PILI**

### **MIRADI 66 INAYOWEZA KUKULETEA PESA NYINGI HADI KUWA BILIONEA**



Hongera kwa kuanza kusoma sura hii. Hapa ndipo sasa nitaanza kukueleza kiini cha kitabu hiki. Kwa kusoma sura hii yote nina hakika utaamua vyema kuwa siyo milionea tu bali kuwa bilionea pia. Sura hii inaeleza miradi ipatayo 66 ambayo ina mawazo chanya na ufanuzi wa wazi unaoweza kukufanya upate pesa nyingi sana kwa muda mfupi hadi kufikia kuwa bilionea. Ukiamua kwa dhati, hakika utakuwa bilionea mkubwa.

Miradi iliyoelezwa katika sura hii imefafanuliwa kwa msisitizo mkubwa wa kimahesabu ambapo ukiifanya kwa umakini, kwa utafiti, upelelezi na ujasiri mkubwa, ukafanya kwa bidii bila woga wala uvivu, ni hakika utakuwa bilionea ndani ya miaka mitatu au chini ya hapo. Ninakupa ahadi (Guarantee) ya miaka 3 kama utachukua moja ya mradi au wazo lililofafanuliwa ndani ya kitabu hiki, hakika utakuwa bilionea.

Ifuatayo ni Miradi iliyofafanuliwa kwa kina na kwa mifano ambayo inaweza kukufanya ukapata utajiri mkubwa ambao utadumu hadi kwa watoto wako na watoto wa watoto wako mpaka watoto wa watoto wa watoto wa watoto wako.

#### **1. Mradi wa Miti ya Mbao**

Mradi huu ni mradi ambao mtu akiufanya kwa muda wa miaka 5 mfululizo baada ya miaka kumi ataanza kuvuna pesa. Unaweza kupanda miti ya

mbao kama vile mikaratusi, griveria, mininga, na mingine mingi iliyopo karibu na wewe ambayo wajasiriamali wengi siku hizi wanauzu maeneo mbalimbali mijini na vijijini. Hesabu za mradi huu ni kama ifuatavyo:

Tafuta shamba lenye ukubwa wa ekari kuanzia 3 hadi 10 au kulingana na uwezo wako. Kwa ajili ya kujifunza tuchukue mfano tu kwa mtu ambaye amefanikiwa kupata shamba la ukubwa wa ekari 5. Mtu huyu akipanda miti ya mbao anaweza kulijaza shamba hilo miti ipatayo 10,000. Ukipanda miti inayokomaa baada ya miaka 10 hadi 15 kama vile karutusi na mingineyo ambayo wataalam watakuambia (endapo ukiamua) ndiyo kusema kwamba kama una umri wa miaka 30 kwa sasa utakapokuwa na umri wa miaka 40 hadi 45 wewe utakuwa tajiri asiyefiliska. Utakuwa tajiri unayekula fedha bila kutoka jasho wala kuwaza kufilisika kamwe!!!

Mradi wa miti ya mbao ukiishauweza kuutekeleza unaweza kuuza mbao za miti yako kwa taratibu kabisa. Unaweza kuamua kuuza mti mmoja tu kwa kila wiki. Kwa hali ilivyo kwa sasa sehemu nyingi Tanzania, mti mmoja uliokomaa unaweza kutoa mbao 50 hadi 100 za kuezeka nyumba au kutengeneza fremu za milango, madirisha na samani mbalimbali. Kwa sasa sehemu nyingi za Tanzania Ubao mmoja huuzwa shs 8,000 hadi 20,000 kutegemeana na aina ya mti, mji na soko lenyewe. Kama ukuza ubao mmoja kwa bei ya hasara ya Tshs 8,000 na ukapata mbao chache za makenchi zipatao 50 tu kwa kila mti unaovuna kwa wiki wewe utakuwa unaweza kuingiza fedha  $8,000 \times 50 = \text{Shs } 400,000$  kwa wiki. Na hapo umeuza mti mmoja tu kwa wiki.

Kama utaamua kuuza miti 5 tu kwa kila wiki utapata pesa kama ifuatavyo:  $8,000 \times 250 = 2,000,000$  kwa wiki moja tu. Na kwa mwezi utaweza kuingiza fedha kama ifuatavyo: Shs  $2,000,000 \times 4 = 8,000,000$  kwa kila mwezi. Hapa ni sawa na kusema utakuwa unavuna miti 20 tu kwa mwezi. Kama una shamba la miti 10,000 hapo ndiyo kusema kwa mwaka utavuna miti ipatayo 240. Tuseme kwamba hata kama utakuwa hupandi miti mipya kabisa ni sawa na kusema kwamba shamba lako litaishiwa miti baada ya miaka ipatayo 40. Baada ya miaka zaidi ya 40 ndipo shamba lako litaishiwa miti yote. Hapa ni sawa na kusema kwamba kwa muda wa miaka 40 utakuwa

unakula pesa bila jasho. Hakuna kufilisika tena. Hakuna umaskini kwako wala kwa kizazi cha watoto wako. Wajukuu wako wote na watoto wa watoto wao hawatakuwa maskini kamwe.

## 2. **Mradi wa Kuweka Akiba.**

Watu Wengi hawajui kwamba unaweza kutajirika kwa kuweka fedha kidogo kila siku, kila wiki, kila mwezi au kila mwaka. Wahenga wa kiswali husema, kidogokidogo hujaza kibaba au haba na haba hujaza kibaba. Usemi huu una umuhimu wake. Wataalam wa mambo ya fedha walishafanya utafiti na kubaini kuwa kama mtu anataka kutajirika na akaishi bila hofu maishani mwake, awe na tabia ya kuweka akiba kidogokidogo na baada ya muda watu watamshangaa akiwa tajiri.

Kwa mfano kama wewe msomaji wa kitabu hiki ukianza kuweka akiba ya shilingi elfu kumi tu kwa siku kuanzia mwaka huu, baada ya miaka 5 utakuwa tajiri mkubwa. Hebu tazama hesabu hii ndogo: Shs 10,000 x siku 30 x miezi 12 x miaka 5 = 18,000,000.00. Hii inamaanisha kwamba baada ya miaka 5 utakuwa na jumla ya fedha zipatazo milioni kumi na name. Hapo pipi, hujawa tajiri? Hujaweza kuanzisha mradi mwingine endelevu kama vile shamba la miti ya mbao? Je, huwezi kuanzisha Shamba la miti ya matunda kama vile machungwa na parachichi? Tafakari kwa kina!!!!

Kwa utafiti mdogo nilioufanya kwa waendesha boda boda hasa walioko mijini; inaonesha kuwa wanapata kati ya shs 10,000.00 hadi 40,000.00 kwa siku. Mwendesha Bodaboda anayepata kipato kama hicho kama anaifanya biashara hiyo kwa malengo baada ya miaka mitano anapaswa aache biashara ya Bodaboda afanye kazi nydingine kabisa endapo mpango wake sio kuzeekea kwenye kuendesha bodaboda.

Kwa upande wa wafanya kazi wa serikali, hapa naomba nitoe mfano kwa walimu kwani ndio kundi kubwa hapa Tanzania. Walimu wengi wa shule za Msingi na Sekondari wanapata kipato kutokana na mishahara yao. Kwa uchunguzi wa uhakika nilioufanya Walimu wengi wanapata Mshahara kuanzia Shs 270,000.00 hadi 1,500,000.00 kwa mwezi. Taarifa hii za kati ya miaka ya 2012 hadi 2015. Hata hivyo, inaonekana kuwa walimu wengi

wanakosa malengo ya kukua kiuchumi katika maisha. Walimu wenyewe malengo ya kukua kiuchumi, wamekuwa haraka sana na kuondoka kwenye orodha ya walimu wasiokuwa na kipato kikubwa na sasa wako kwenye orodha ya walimu walijotajirika. Tatizo la kutoweka malengo ya maisha, limewafanya walimu wengi kuishia kuwa na madeni mengi kwenye taasisi za kutoa mikopo na kwa watu binafsi.

Kwa mfano, Mwalimu mwenye mshahara wa shs 400,000 anaweza kutajirika sana kama akiamua. Kama mwalimu mwenye kipato cha shs 400,000 anaweza kuamua kuweka shs 210,000 za Chakula chake cha kila siku ikiwa ni sawa na shs 7,000.00 kwa siku. Akiweka akiba ya shs 5,000 kila siku itakuwa ni sawa na shs 150,000 kwa mwezi. Atabakiwa na Shs 40,000 katika mshahara wake wa mwezi ambazo anaweza kuzitumia kwenye mengineyo ikiwemo ndugu, wazazi, jamaa na marafiki. Kama kila mwezi mwalimu huyo atafungua akaunti maalum ya malengo benki ni kwamba baada ya mwaka mmoja atakuwa na akiba ya Shs 1,800,000. Kama mwalimu alilenga Kununua pipipiki ya biashara, anaweza kuinunua bila hata kwenda kukopa benki au popote pale.

Mwalimu huyu akiamua kuendelea Kuweka akiba ya Tshs 150,000 kwa mwezi, baada ya miaka mitano (5years) atakuwa na mtaji unaofiki TShs 9,000,000. Pesa kama hizo anaweza kuzitumia kununua au kufanya mradi mwingine mkubwa na wa kudumu unaoweza kumwingizia kipato cha ziada zaidi kama ambavyo imeelezwa katika kitabu hiki. Kupata Mtaji wa shs 9,000,000 bila kwenda kukopa popote siyo mtaji mdogo.

Mtaji kama huo waweza kutumika kuanzisha mradi wa shamba kubwa la mazao ya kudumu kama vile machungwa, miti ya mbao, biashara yoyote endelevu, ufugaji wa kuku, ng'ombe wa maziwa, nk. Mwalimu ukiamua kujipanga leo unaposoma kitabu hiki nakuhakikishia kwamba hautakuwa mwalimu maskini.

Naomba pia niwazungumzie wafanyakazi wenyewe kipato cha kuanzia Tshs 1,000,000 kwa mwezi. Hawa ni wafanyakazi wa serikali na mashirika makubwa ya serikali na yasiyokuwa ya serikali kama vile vyuo vikuu binafsi na vya umma, mashirika ya nje (INGOs), taasisi kubwa kama vile Mamlaka

ya mapato (TRA), Benki kuu, mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Mashirika ya Bima, Mabenki, Wakuu wa Vitengo au Idara za serikali, nk. Hawa wana kipato kikubwa kiasi kwamba wanaitwa kuwa wako katika kundi la wenye kipato cha kati. Yaani siyo watu maskini wala matajiri. Wafanyakazi wengi walioko katika kundi hilo wana kipato kisichopungua shs 1,200,000 kwa mwezi. Hawa wafanyakazi wanaweza kuondoka kwenye umaskini haraka sana kuliko kundi lolote hapa Tanzania. Kwa mfano, kama mfanyakazi wa kundi hilo nililolitaja ikiwa ni pamoja na sekta binafsi ya Afya au ya serikalini, ataamua kuweka akiba ya shs 450,000 tu kwa mwezi kwa muda wa miaka mitano atakuwa na jumla ya shs  $450,000 \times 12 \times 5 = \text{Shs } 27,000,000.00$ . Hii ndiyo kusema kuwa atakuwa na akiba ifikayo Tshs 27,000,000 kwenye akaunti yake bila kuongeza riba atakayoongezewa na benki kila mwaka. Au kama akiweka akiba hivyo hivyo kwa kipindi cha miaka 15 mfululizo atakuwa na jumla ya shs 81,000,000.00. Mtaji wa Shs 27,000,000 ndani ya miaka 5 tu au Tshs 81,000,000 ndani ya miaka 15 ni mtaji amba unatosha kuanzisha mradi mwingine endelevu utakaomsaidia ofisa huyo kuondokana na utegemezi wa kutegemea mishahara peke yake ili kuendesha familia. Watanzania tukiamua inawezekana kabisa kuutokomeza umaskini.

Tatizo letu tulio wengi siyo ukosefu wa pesa, tatizo letu kuu ni ukosefu wa fikra zilizo pana na chanya. Tatizo kubwa wengi tunakosa kuona mbali na kutafakari zaidi na hatutaki kutazama kuna nini mbele yetu tumepanga kufanya kwa ajili yetu na watoto wa watoto wetu.

### **3. Mradi wa Miti ya Machungwa**

Mradi wa kupanda miti ya matunda unaweza kukuondolea umaskini wewe na kizazi chako chote. Wajukuu na watoto wako wote hawatakuwa maskini kamwe kama utafanya mradi wa kupanda miti ya matunda. Mradi wa miti ya matunda ni mradi mzuri sana na siyo lazima uwe kwenye shamba kubwa sana. Ukipata shamba lenye ukubwa wa ekari 2 tu ukapanda miti ya matunda peke yake, hapo umevunja minyororo ya umaskini. Minyororo ya umaskini inavunjika baada ya miaka 5 tu tangu uanze kutekeleza mradi huo. Ukiwa na shamba la ekari 2 unaweza kupanda miti ya matunda aina moja au mbili tu. Kwa mfano, Unaweza kuchagua miti ya Machungwa, au miti ya Parachichi.

Ukiamua kufanya mradi wa miti ya machungwa, utapaswa kupanda miti ipatayo 1,225 kwa kila ekari moja sawa na miti 2,450 kwa ekari 2 ulizonazo. Mti wa chungwa kama umestawi na kama umepanda mbegu nzuri na kufuata ushauri wa kilimo cha kitaalam mchungwa mmoja unaweza kutoa machungwa yapatayo 250 kwa msimu mmoja. Ukizidisha kwa miti 2,450 yote iliyoko shambani utapata machungwa yapatayo 612,500 kwa msimu mmoja. Endapo kila chungwa utaliuza kwa shs 200 tu ni sawa na kusema kwa msimu mmoja wa mwaka wewe utavuna pesa kama ifuatavyo:  $612,500 \times 200 = 122,500,000$  kwa mwaka mmoja tu. Hii ni sawa na kipato cha Tshs 10,208,333 kwa mwezi. Hesabu hii ni maksio ya chini kabisa. Aidha, hesabu hizi siyo za kubabaisha, ni ukweli unaoweza kutokea kwako ukiamua leo.

Miti ya machungwa inaweza kuendelea kuishi kwa zaidi ya miaka 10 ikiwa inazalisha machungwa safi bila wasiwasi ili mradi tu miti hiyo itunzwe kwa kufuata kanuni za kitalaam kama vile kuwekewa mbolea ya samadi, maji ya kutosha, na dawa ya kutibu magonjwa ya ukungu, nk. Hapa tunaona kuwa ukiamua kununua ekari 2 tu na kufanya kilimo cha machungwa pekee yake, utakuwa tajiri mkubwa Tanzania ndani ya muda mfupi wa miaka 5 tu. Gharama ya kununua ekari mbili kwa mwananchi mwenzako siyo kubwa sana. Ekari moja sehemu nyingi za vijijini waweza kuelewana na mwananchi kwa bei isiyozidi Tshs 200,000.00. kuna sehemu nyingine waweza Kununua ekari moja kwa shilingi 50,000 tu.

Huwezi kuwa na shamba la miti ya machungwa halafu ukafa ukiwa maskini. Kumbuka kwamba hapa nimezungumzia miti ya machungwa tu, lakini waweza pia kufanya kilimo cha matunda kama passion, avocado, nanasi, maembe, limao, tangawizi, vitunguu, nk. Ukifanya mradi wa matunda ya avocado kwa mfano, unaweza kupata pesa nyingi sana kwa muda mrefu wa maisha yako. Ukifanya mradi wa kilimo cha maembe nacho pia kinaweza kukupatia fedha nyingi kwa maisha yako yote ili mradi ufanye mradi huo kwa kuzingatia utalaam wa kilimo hicho. Kama ungependa kufanya mradi huu, jitahidi Kununua vitabu vya ufanuzi zaidi kuhusu kilimo hicho. Aidha, waone watalaan wakusaidie ushauri wa kitalaam.

#### **4. Mradi wa Nyumba za Kulala Wageni (Guest Houses Project)**

Mradi huu unaweza kukuondolea umaskini maishani mwako wewe na watoto wa watoto wako. Ukitaka mradi huu ukusaidie kuondoa umaskini ni vyema ukatafuta eneo zuri na kubwa hasa kwenye miji inayokua au inayochipukia kibashara au kiserikali. Hapa Tanzania Kwa mfano miji inayokua na kuchipukia kutoka vijiji na kuwa miji au miji kuwa manispaa ipo mingi.

Kwa kutaja michache tu miji midogo na ya kati inayokua kwa haraka au inayochipukia kuelekea kuwa miji ni kama vile vijiji nya Nyakanazi, Katoro, Bwanga, Rusumo, Tunduma, Namanga, Kyaka, Omurushaka, Tinde, Lamadi, Mugumu, Tarime, Butiama, Kakonko, Nguruka, Mpanda, Gairo, Dakawa, Bombo, Chalinze, Kigamboni, Uvinza, Manyovu, Chatto, Geita, Bukombe, Isaka, Kaliua, Ulyankulu, Runzewe, Igunga, Nzega, nk. Miji kama hii na mingine mingi inakua haraka kwa sababu za kisiasa, kibashara, kiuchumi au hali ya hewa.

Kwa mtu anayeona mbali, miji kama hiyo inafaa kwenda kuwekeza. Unaweza kuwekeza siyo nyumba za wageni pekee yake hata biashara za kawaida, ufungaji nk ni miradi inayoweza kutekelezeka kwani miji kama hiyo bado kuna fursa nyingi.

Tuangalie jinsi unavyoweza kupata utajiri hadi kuwa milionea ndani ya muda mfupi. Kama utajenga nyumba ya kisasa yenyeye vyumba visivyopungua 10 inayoweza kugharimu mpaka Tshs 80,000,000 unaweza kupata pesa nzuri kwa mwezi. Nyumba ya kulala wageni ikijengwa eneo ambalo lina mzunguko mkubwa wa watu na biashara hasa miji inayochipuka, inaweza kupata wageni kila siku. Nyumba ya wageni (Guest House) ikiwa na vyumba 10 na ikiwa imejengwa kisasa sana yaani ina huduma zote kama vile vyoo/bafu za ndani, runinga, maji, usafi wa hali ya juu, maegesho ya magari, wahudumu wachangamfu na wakarimu, na ulinzi wa kutosha, inaweza kuingiza Tshs 15,000 kwa chumba kila siku. Kama vyumba vyote vimepata wageni itakuwa ni sawa na Tshs 15,000 x 30 x 10 = 4,500,000. Hii ndiyo kusema kuwa kwa mwezi utapata kipato cha Tshs 4,500,000.00. Hata

kama mwezi fulani hali ya biashara ni mbaya hautakosa Tshs 1,000,000 kwa mwezi.

Kwa mjasiriamali mwenye kuthubutu zaidi, anaweza kukopa kutoka Benki fedha za kujenga nyumba nne (4) au zaidi kama hizo ili mradi anaweza kurejesha mkopo wa benki. Benki zinahitaji watu wenyewe ujasili na utashi wa kurejesha mkopo basi. Kama unao ujasili na unaweza kufafanua na kueleza mpango kazi wako na mchanganuo wa jinsi utakavyoindesha biashara kwa faida na kurejesha mkopo wao, mabenki mengi hutoa mikopo bila wasiwasi ili mradi uwe na dhamana ambayo mabenki hawana mashaka nayo.

Benki nyingi zinaweza kutoa mikopo kwa kiwango chochote utakacho au uwezacho wako hata kama ni milioni 400. Kama ukiweza kuwathibitishia benki kwamba ukikopeshwa Tshs 400,000,000 (milioni mia nne) kwa ajili ya kujenga “Guest Houses” tano (5) na ukawathibitishia kwamba nyumba hizo zitaingiza zaidi ya Tshs 3,000,000 kila moja sawa na Tshs 15,000,000 kwa mwezi na kwamba kwa Mwaka utaweza kukusanya zaidi ya Tshs 180,000,000 na kwamba mkopo wao ndani ya miaka michache utawarejeshea bila hofu; benki hazina hiana, zitakukopesha. Kama unaweza kuingiza Tshs 15,000,000 kwa mwezi na unaweza kulipa deni la benki kwa angalau Tshs 6,000,000 kwa mwezi; ndio kusema kwamba deni la benki la Tshs 400,000,000 waweza kulilipa ndani ya miaka 5.5. Hii hoja inatosha kushawishi mabenki yakukopeshe endapo utapata watalaaam wa kukuandikia andiko la mradi na mpango wako wa biashara kwa miaka mitano.

Ili mabenki yakukopeshe, unatakiwa kuwa na vitu vyote vya kisheria kama vile hati za viwanja na nyumba. Naomba nitumie nafasi hii kukushauri wewe unayesoma kitabu hiki ujitalidi kuwa na kiwanja chenye HATI yaani kiwanja kilichopimwa na kupata hati miliki ya kiwanja husika. Epuka kununua mashamba au viwanja visivyokuwa na HATI. Kama unanunua viwanja/mashamba yasiyokuwa na Hati hakikisha kuwa unawasiliana na ofisi za ardhi kwenye Hal mashauri ya Wilaya iliyoko karibu na wewe ili upatiwe utaratibu wa kupewa HATI ya kumiliki kisheria eneo lako. Hata benki zitakuwa hazina mashaka na wewe endapo utataka kupata mkopo wa biashara kama hii ya nyumba za wageni.

Ukiwa na nyumba tano (5) za kulaza wageni kwenye mji wowote, utakuwa na uhakika wa kupata Kipato kwa siku kisichopungua Tshs 15,000 x 10 x 5 = 750,000. Utapata Tshs 750,000 kwa siku. Kwa mwezi itakuwa ni sawa na Tshs 750,000 x 30 = 22,500,000 kabla ya kutoa matumizi ya wafanyakazi, usafi, matengenezo, kodi, umeme na ushuru. Hata kama gharama za uendeshaji ziko juu kiasi gani, bado wewe mwenye mali naamini hautakosa Tshs 10,000,000 kwa mwezi. Kwa Mwaka mmoja utakuwa na uhakika wa kupata zaidi ya Tshs 120,000,000 kutoka kwenye nyumba hizo. Je wewe siyo milionea tayari. Kumbuka Mapato hayo ni makisio ya chini sana. Kumbuka ukifanikiwa kufanya mradi kama huo, utakuwa tajiri asiyefilisika kamwe wala asiyetegemea kula kwa jasho tena.

## 5. Mradi wa Nyumba za Kupangisha

Mpendwa msomaji wa kitabu hiki, mradi mwengine unaoweza kukuletea utajiri wa kudumu na ukapata pesa bila kutokwa jasho, ni mradi wa nyumba za kupangisha. Hata hivyo, uzoefu unaonesha kuwa mradi huu wa nyumba unakuwa na changamoto nyingi Sana ikiwemo tatizo la wapangaji kuwa wasumbufu kulipa kodi, majengo kuharibiwa Na wapangaji, wapangaji kutaka marekebisho kwenye nyumba, nk. Changamoto kama hizo huwakatisha tamaa wamiliki wengi wa nyumba na kushindwa kupata kipato kikubwa kama walivyopanga. Hata hivyo, nyumba imebakia kuwa miradi inayopendwa na wengi kutokana na kwamba usimamizi wake na hatari zinazoikabiri miradi ya nyumba kuwa ni ndogo ikilinganishwa na faida zake.

Ni vyema ukaanza kutafuta maeneo au viwanja vya kufanya ujenzi wa nyumba. Kwa mfano ukiamua kutafuta maeneo pembedi mwa miji, bei za maeneo hayo bado zinakuwa na bei ndogo. Ukitinunua leo utajikuta baada ya miaka kadhaa maeneo hayo yanakuwa ya kibashara na utanufaika kifedha. Kwa mfano ukinunua kiwanja au shamba lenye ukubwa wa ekari moja yaani mita 70 x 70 au nusu ekari yaani mita 35 x 35. Eneo la ekari moja linaweza kutumika kujenga nyumba zaidi ya 12 kama utazijenga kwa mpangilio wa kitalaam. Ukiujenga nyumba 12 kwenye kiwanja chako cha ekari moja, na nyumba moja ukaipangisha kwa angalau Tshs 150,000 kwa mwezi utakuwa na uhakika wa kupata Tshs 1,800,000 kwa mwezi.

Kujenga nyumba 12 kwenye eneo moja (Estate houses) yaweza kuonekana kuwa ni ngumu kwa wengi. Lakini kama mtu akijipangia kujenga nyumba hizo na akajenga nyumba moja moja, ndani ya miaka 10 anaweza kuzimaliza nyumba hizo. Aidha, taasisi za fedha kama benki na mifuko ya hifadhi ya jamii zinaweza kutoa mikopo kwa mtu ambaye anahitaji mikopo na anamiliki eneo lake kisheria. Kama eneo lako la ekari moja unalimiliki kisheria yaani una HATI ya kumiliki eneo lako, taasisi za fedha zinaweza kukupa mkopo unaoutaka. Chukua hatua sasa hivi. Changamka haraka.



Mfano wa Nyumba ya Ghorofa moja ya wapangaji 6

Ukiamua kujenga nyumba za kupangisha hakikisha kwamba unajenga maeneo ambayo yana uelekeo wa kuwa miji mikubwa kibashara au kiserikali hapo baadaye kama ilivyoelezwa katika kipengere cha miradi ya nyumba za kulala wageni. Tukichukua mfano wa mjasiriamali mmoja ambaye akiamua kujenga nyumba sita (6) tu zenye kugharimu Tshs 120,000,000 kwa maana ya Tshs 20,000,000 kwa kila nyumba huyu mjasiriamali anaweza kuwa anapata kipato cha Tshs 1,200,000.00 kwa mwezi kutegemeana na nyakati na mahali nyumba hizo zilizopo. Kila nyumba inaweza kuingiza kipato cha Tshs 100,000 hadi 300,000 kwa mwezi. Kipato kama hicho kwa mtu ambaye amestaafu kazi, ni pato kubwa hasa awapo mzee na hana mshahara tena au hana nguvu tena za kufanya kazi. Mradi wa nyumba unafaa kwa ajili ya maisha ya uzeeni ili kupata kipato cha ziada.

Unapaswa kupanga maisha yako ya uzeeni. Panga kipato chako kitakavyokuwa. Usipange kuwa na maisha ya kimaskini ukifika uzeeni. Panga kuwa tajiri uzeeni. Tatizo la watanzania walio wengi wanapanga

kuishi maisha ya kimaskini uzeeni. Uzeeni ni umri wa kuishi kifahari na kitajiri. Siyo wakati wa kuomba omnia watoto wako wakusaidie fedha. Uzeeni ndio wakati wewe unapaswa kusaidia watu kimawazo na kifedha. Jenga nyumba za kupangisha kwa kadri unavyopata fursa. Acha maisha ya anasa. Tumia pesa yako kwa busara. Kama unakopa pesa benki, hakikisha unakopa pesa kwa ajili ya kuanza kujenga nyumba za biashara zitakazokuwezesha kupata kipato kikubwa uzeeni au watoto wako watarithi endapo utaondoka duniani. Ukiamua inawezekana.

## **6.        Mradi wa Mabweni ya wanafunzi (Student Hostels)**

Miradi ya Hostel za wanafunzi inaendelea kuchukua kasi sehemu mbalimbali za nchi. Miradi hii imeanza kukubalika baada ya vyuo vingi nya elimu ya juu kuwa na uhaba wa hostel za kulaza wanafunzi wote wanaodahiliwa kila mwaka. Changamoto hiyo, watu wengi wameibadilisha kuwa fursa ya kiuchumi. Wengi wamemua kujenga Hostel karibu na vyuo au hata mbali na vyuo lakini wameweka miundombinu ya kuvutia ili wanafunzi waweze kupanga katika Hostel zao. Utafiti wa kawaida unaonesha kwamba watu waliowekeza katika miradi kama hii ya kujenga “Hostel” kila kitanda hutozwa kodi katika Tshs 300,000 hadi 600,000 kwa mwaka.

Kwa mfano Hostel moja yenye vyumba 10 na kila chumba kikawa na uwezo wa vitanda 2, inaweza kuingiza kipato cha kutosha kukufanya usiwe masikini tena kama ifuatavyo; Chumba kimoja chenye vitanda 2 na kila kitanda kama kinalipiwa kodi ya Tshs 300,000 basi pato kwa mwaka itakuwa Tshs  $300,000 \times 2 \times 10 = 6,000,000$  kwa mwaka. Kama mjasiriamali utaweka vitanda vine (4) kila chumba kwa bei hiyo hiyo ya Tshs 300,000 kwa kitanda kimoja pato lako litaongezeka mara dufu yaani Tshs  $300,000 \times 4 \times 10 = 12,000,000$  kwa mwaka. Kama mjasiriamali utakuwa na nyumba mbili za mfano huo, utakuwa na uwezo wa kujipatia kipato kipatacho Tshs 24,000,000 kwa mwaka.

Changamoto zilizopo kwenye miradi ya nyumba ni kwamba mapato yake yanaonekana kuwa ni madogo sana ikilinganishwa na gharama zinazotumika kujenga majengo hayo. Watalaam wa uchumi husema kwamba kadri mradi unavyokuwa na hatari nyingi ndivyo mapato yake

yanavyokuwa makubwa na kinyume chake au kwa kimombo, “the higher the risks facing the business the higher the returns and vice versa”. Udogo wa mapato kwenye miradi ya nyumba kama hizo hazipaswi kumkatisha tamaa mjasiriamali anayetaka kuwekeza kwenye nyumba za mabweni ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu. Ifahamike kwamba ukishafanikiwa kujenga majengo kama hayo utaendelea kupata kipato chako bila kutumia nguvu nyingi tena. Miradi ya nyumba inaweza kuendelea kukuungizia kipato kila mwaka hadi kifo kitakapokuchukua. Watoto wako wataweza kuendelea kufurahia kipato hicho ulichowaachia hadi wajukuu wa wajukuu zao.

## 7. Mradi wa Ufugaji Nyuki

Mradi huu ni mradi makini sana. Ni mradi wa matajiri siku hizi. Kwa Tanzania, Mzee Mizengo Kayanza Peter Pinda, ambaye ni Waziri Mkuu wa sasa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mtoto wa mkulima, amekuwa mstari wa mbele kuhamasisha ufugaji wa nyuki. Mzee huyu anahamasisha watu wengi vijana kwa wazee wafuge nyuki baada ya kupembua mradi huu na kuona kuwa kuna utajiri sana uliojificha ndani yake. Ufugaji nyuki waweza kukupa fedha maisha yako yote. Unaweza kutajirika baada ya muda mfupi. Kwa mfano kama unalo shamba lako la ekari moja tu, waweza Kufuga nyuki kwa kutumia mizinga zaidi ya 600. Hapo ni endapo utafuga kwa kufuata ushauri wa kitalaam au kupanga mizinga yako kwa kila mzinga wa nyuki kuchukua umbali wa mita 3 kila baada ya mzinga mmoja. Tuchukue mfano huo kwamba sasa una ekari moja lenye mizinga 600. Kama Kila mzinga unaweza kutoa Lita 10 za asali, na kama kwa Mwezi unaweza kuvuna au kulina asali kutoka kwenye mizinga 60 utakuwa unapata lita 600 za asali kwa mwezi. Kama kila lita utauza kwa Tshs 10,000 utakuwa na uhakika wa kujipatia siyo chini ya Tshs 6,000,000 kwa mwezi. Je, utaendelea kuwa masikini? Kipato hicho hata Meneja wa shirika kubwa, huenda asikifikishe, kwa Kufuga nyuki tu kwani hayo ni maksio ya chini.

Kwa mfano ukisema uvune mizinga 3 kila siku kwa mwezi utalina mizinga 90. Kama kila mzinga unatoa lita 10 za asali, utapata lita 900 kwa mwezi. Kama kila lita utauza kwa Tshs 10,000 utakuwa na uhakikia wa kupata Tshs 9,000,000 kwa mwezi. Huu ndio utajiri uliojificha karibu yako, shambani

mwako. Watu wa vijijini wanaweza kabisa kufanya miradi kama hii, kwani wao wanayo mashamba makubwa. Hata watu waishio miji mikubwa nao wanaweza ili mradi tu mtu analo eneo lake kubwa angalau la ukubwa wa nusu ekari au ekari moja tu. Watu wenye maeneo kama hayo mijini wapo, na wengine maeneo hayo wameyatelekeza tu hata hawayaendelezi. Fursa ndiyo hii. Changamka leo, chukua hatua. Je, ni ajira gani utapata hapa Tanzania yenyе mshahara wa Tshs 9,000,000 kwa mwezi, tena uzipate pesa hizo bila jasho au kutumikishwa sana? Hapa Tanzania, kama kuna watu wenye mshahara unaofikia Tshs 9,000,000 kwa mwezi watakuwa hawazidi 100. Wewe kwa Kufuga nyuki kwenye eneo lako la ekari moja tu, waweza kuwa mionganoni mwao na ikiwezekana ukawazidi. Kazi yako wewe ni kulina asali tu, tena mizinga 3 tu kwa siku.

Kazi nyingine utakayokuwa nayo, ni kutafuta wanunuzi maalum, wanaweza wakawa mashirika au watu binafsi. Ukipata watu au mashirika wanaochukua asali kila mwezi itakuwa raha sana kwako. Kwa mfano ukipata wanunuzi/wateja wa kuaminika (na ukweli ni kwamba wateja wa asali ni wengi) wapatao 10 tu wenye kuchukua lita 90 kila mwezi kila mmoja, utakuwa umeshinda kwa kishindo. Utapaswa kusajili kampuni yako na kuitumia zaidi kusambazia bidhaa yako ya asali kila kona ya dunia.

## **8. Mradi wa kuku wa Mayai**

Mradi huu unaweza kuwa hitimisho la umaskini wa fedha ulionao kama utaufanya kwa kufuata ushauri wa kitalaam. Mradi wa kufuga kuku wa mayai ya kisasa unaleta utajiri mkubwa. Watu wanaopenda kula mayai ni wengi hasa kupitia ulaji wa chipsi ambao kwa Tanzania, chipsi ni chakula kinacholiwa sana siku hizi. Kila kona zenyе watu wengi au makutano ya watu wengi wanaosafiri au kukusanyika tu kwa shughuli za kiuchumi siku hizi utakuta wapishi wa chipsi wamejaa. Wapishi wengi wa chipsi hutumia si chini ya tray mbili la mayai kwa siku. Sehemu nyingi za Tanzania yai moja huuzwa kwa Tshs 200 hadi 300. Hii ina maana kwamba tray moja la mayai linauzwa kuanzia Tshs 6000 hadi 9,000 au zaidi kutegemea eneo husika.



Kwa mfano kama utafuga kuku wapatao 350 wa mayai, utakuwa na uhakika wa kupata mayai yapatayo 300 au zaidi kwa siku. Hii ni sawa na tray 10 kwa siku. Kama kila tray utaiuza kwa Tshs 6,000 tu utakuwa na uhakika wa kujipatia Tshs 60,000 kwa siku au Tshs 1,800,000 kwa mwezi. Hii ni kwa mfugaji mdogo kabisa na ambaye hana eneo kubwa la kufugia au mwenye mtaji mdogo. Ufugaji wa kuku 350 wa mayai unahitaji mtaji mdogo tu si zaidi ya Tshs 1,500,000 kama tayari unalo banda imara la kufugia. Kwa mtanzania anayetaka kuinuka kiuchumi, haitakuwa ngumu kwake kupata Tshs 1,500,000 au zaidi kama ataamua kuchukua mkopo toka kwa ndugu, marafiki, mabenki au SACCOS.

Ufugaji wa kuku wa mayai unaweza kukuondoa kwenye umaskini hadi kuwa milionea. Kumbuka kama ukifuga kuku 350 wenyewe uwezo wa kukupatia Tshs 1,800,000 kwa mwezi, kuku hao wanawenza kutaga mayai hayo kwa zaidi ya miaka 3 mfululizo kabla ya kuamua kuwauza na Kununua kuku wapya. Kama unalo eneo kubwa na ukaamua Kufuga kuku wapatao 1200 wa mayai, utakuwa na uwezo wa kupata zaidi ya tray 30 za mayai. Kama utauza tray hizo 30 kila siku kwa bei ya Tshs 6,000 utakuwa na uhakika wa kupata Tshs 5,400,000 kwa mwezi.

Fikiria kama ukiamua Kufuga kuku wapatao 2100 ambapo utakuwa na uwezo wa kuvuna trey zipatazo 70 kwa siku!!! Kama kila trey utaiuza kwa Tshs 6000 tu utakuwa na uhakika wa kukusanya pesa ipatayo Tshs 420,000 kwa siku. Kwa hakika utapata zaidi ya Tshs 12,600,000 kwa mwezi. Huu ni mradi ambao watu wenyewe kuona mbali huufanya. Ni mradi unaoweza kutekelezeka hasa kama unalo eneo lisilopungua robo ekari. Kumbuka kuwa kuku wakiishaanza kutaga wewe ni kuvuna mayai tu kila siku. Ukiamka asubuhi wewe ni kuokota mayai na kuwauzia wafanyabiashara.

Waweza kuingia mkataba na wauza chipsi uwauzie kila mmoja tray anazohitaji kwa siku. Ukipata pesa unayotaka kwa siku kutoka kwao. Kuku wakiishaanza kutaga, wewe utakuwa na uhakika wa kupata kipato chako kila mwezi. Ukumbuke kuwa kwa zaidi ya miezi 24 mfululizo kuku wako wataendelea kutaga kila siku. Kazi yako wewe ni kuwalisha na kuwapa dawa za kinga na tiba kwa kuzingatia ushauri wa kitalaam.

## **9. Mradi wa Ufugaji wa kuku**

Kama ilivyoelezwa kwenye ufugaji wa kuku wa mayai, ufugaji wa kuku wa kienyeji nao unatoa utajiri mkubwa sana kwa wafugaji. Ili kuku wako wasipatwe na maradhi sana, yakupasa pia ufuate ushauri wa kitalaam. Ukipata kuku wa kienyeji ambao watakuwezesha kuuza kuku wapatao 20 tu kila siku kwa bei ya Tshs 8000 kwa kuku mmoja, utakuwa na uhakika wa kujipatia kipato kisichopungua Tshs 160,000 kwa siku. Utakuwa na uhakika wa kujipatia kipato kisichopungua Tshs 4,800,000 kwa mwezi. Utakuwa na uhakika wa pesa na kitoweo kwa pamoja. Familia yako itapata mayai, nyama na mbolea. Kwa hiyo utakuwa na uhakika wa utajiri ili mradi ufuate kanuni za utalaam.

Kama mtaji wako umekua vyta kutosha waweza sasa kuamua Kununua shamba kubwa kama la hekari tano au zaidi na ukafuga kuku wa kienyeji au wa kisasa wapatao 7000 hadi 10,000. Ukipata kipato kisichopungua Tshs 800,000 kwa siku moja tu. Kwa mwezi utakuwa na uwezo wa kuuza kuku 300 tu kwa thamani ya Tshs 24,000,000. Maana yake ni kwamba utakuwa na uwezo wa kujipatia milioni 24 kila mwezi. Kuku elfu kumi wanawezekana kabisa kufugwa ukiamua. Kama mtu anawenza kufugwa ng'ombe elfu moja kwa nini Kufuga kuku ambao hawahitaji eneo kubwa kama ng'ombe isiwezekane? Kumbuka kwamba kuku wapatao elfu kumi wanawenza kufugwa hata katika eneo la hekari moja au mbili tu.

Kama unawenza kwa upande mwengine kufuga kuku wa kisasa wa mayai wapatao 5000 tu. Ukipata kuku wa mayai wa kiasi hicho utakuwa na uhakika

wa kujipatia mayai yasiyopungua 4500 kwa siku. Kama umejipanga vyema kuyauza mayai hayo kila siku kwa bei ya shilingi mia mbili tu kwa kila yai (Tshs 200) utakuwa na uwezo wa kukusanya pesa ipatayo Tshs 900,000 kwa siku. Kwa mwezi ukipiga hesabu utakuta unakusanya si chini ya Tshs 27,000,000.



Mfano wa Banda la Kuku wa kienyeji

Kumbuka kuku wapatao 5000 unawenza kuwafugia hata katika eneo dogo tu la nusu heka kwa kujenga mabanda matano yanayofuga kuku 1000 kwa kila banda. Huu ni ufugaji wa kuku wengi na ndio ufugaji wa kibashara (large scale chicken farming). Ukiamua inawezekana kabisa. Je, hupendi Kupata mshahara wa milioni ishirini na saba kwa mwezi? Kama unapenda unangoja nini sasa kuchukua hatua ndugu yangu?

Aidha, waweza kuamua kufanya biashara ya Kununua na kuuza kuku wa kienyeji kutoka vijijini kwenda kuuza mijini kwa faida zaidi. Badala ya wewe Kufuga kuku unachofanya ni kwamba wewe unanunua kwa wafugaji wa vijijini kisha unaenda kuuza mijini kwa faida zaidi. Kwa mfano kama ukinunua kuku 40 vijijini kwa bei ya Tshs 7,000 kisha ukawaleta kuku hao 40 kuwauza mjini kwa bei ya Tshs 10,000 maana yake ni kwamba utakusanya Tshs 400,000 ambapo wewe faida yako itakuwa Tshs  $3000 \times 40 = 120,000$  kwa siku moja. Mtaji wa kufanya biashara hiyo utaona kwamba ukiwa na Tshs 280,000 unawenza kuanza biashara hii. Hata tukisema tuongeze gharama ya nauli kwenda vijijini na kurudi ukaongeza gharama ya matenga ya kubebea kuku; hapa ina maana kwamba utaanza na Mtaji wa Tshs 350,000 tu.




Hebu fikiria biashara ya kuanza na mtaji wa Tshs 350,000 na ukapata faida ya Tshs 120,000 huu siyo muujiza? Kwa mwezi tufanye kwamba wewe utaenda safari zipatazo 20 tu na kila safari ulete kuku 40 tu na uuze kwa bei hiyo ya Tshs 10,000 kila kuku, ni dhahiri kwamba kwa mwezi huo unaweza kujipatia Tshs 2,400,000. Hebu ona muujiza huu unaokusubiri? Kipato cha shilingi milioni mbili na laki nne kwa mwezi!!!???? Sasa hapo mtaani bado unasubiri nini kijana mwenzangu? Kwa nini unashinda unazunguka tu huku na kule bila pesa mkononi wakati pesa zimejaa kijiji cha jirani? Ili kufanikisha biashara hii ya Kununua na kuuza kuku inabidi ufanye mbinu zifuatazo: tafuta migahawa au hoteli kama tatu tu ambazo utaingia nazo mkataba wa kuwauzia kuku kila siku. Kila hoteli uwauzie kuku wasiopungua 13 au kwa kadri watakavyokuwa wanataka.

Hatua ya pili; kwa upande wa vijijini unaweza kumweka mtu wako mmoja akawa kama wakala(Agent) wako ambaye wanavijiji wanaofuga kuku watakuwa wanaleta kuku kwake kila siku ili wewe kila siku uwe unaenda kuchukua kuku 40 kwa Wakala wako kwenye kijiji hicho. Hatua ya tatu wewe ni kuhakikisha kwamba kila siku unaleta kuku 40 kwa wateja wako ambao ni hoteli au migahawa uliyoingia nao mikataba ya maandishi au mdomo tu. Kama mtaandikishana mkataba ni vema zaidi. Hakika ukifanya hivyo, hautakuwa maskini kamwe, utakuwa milionea muuza kuku. Naam, milionea aliyetajirishwa na kuuza kuku tu!!! Chukua hatua leo leo!!

## **10. Mradi wa Kufuga Mbuzi**

Kama ilivyoelezwa kwenye kipengere cha ufugaji wa kuku, mradi huu wa Kufuga mbuzi unaweza kukufanya tajiri bilionea. Ukitaka kufanikiwa sana unatakiwa ununue shamba kubwa nje ya mji kama hekari kumi au zaidi. Ukishanunua hekari kumi au zaidi unaweza kujenga mabanda ya kufugia mbuzi wako. Jenga mabanda ya kutosha kulaza mbuzi angalau 8000, kama umeamua kufanya ufugaji mkubwa kabisa wa kibiashara (large scale livestock keeping).




Ukifuga mbuzi wapatao 8000 utakuwa na uhakika wa kuteka soko la nyama ya mbuzi kwa mwaka mzima. Hata kama utaamua kuuza mbuzi wapatao 20 kila siku kwa mwaka utakuwa umeuza mbuzi wapatao 7,200 tu. Kumbuka kwamba mbuzi watakuwa wanazaliana kila mara. Kama utakuwa na lengo la kuuza mbuzi 20 tu kwa siku kwa bei ya Tshs 40,000 kwa kila mbuzi utakuwa una uhakika wa kujipatia kiasi cha Tshs 800,000 kwa siku. Kwa mwezi utakuwa na uhakiwa wa kujipatia siyo chini ya Tshs 24,000,000. Hakikisha kwamba unakuwa ndio mradi wako.

Hakikisha kwamba unaajiri watu wenye kusimamia mradi wakiwa na ufahamu na ujuzi wa kile wanachofanya. Usajiri watu hovyo au kwa kutazama udugu tu bila ujuzi unaotakiwa. Walipe mshahara mzuri na uwasiimamie vyema hakika utafurahia mradi wako. Hakika baada ya miaka mitatu wewe ni milionea na baada ya miaka kumi wewe ni bilionea mkubwa Tanzania.

## **11. Mradi wa Kilimo cha matikiti maji**

Kusema ukweli kilimo cha matunda haya ya Tikitimaji (watermelon)

kinaweza kumpatia mkulima fedha za uhakika kwa muda mfupi kabisa. Katika nyakati za sasa, matunda haya yanapendwa sana na watu wengi. Tikitimaji zinapata soko kwa haraka. Isitoshe ni matunda ambayo ni tofauti na zao kama la nyanya au matunda yanayoharibika mapema baada ya kuvunwa. Ukilima matikitimaji hautabaki maskini kamwe. Kwa mfano kama unalo eneo lenye ukubwa wa ekari moja tu, ukalitumia lote kulima matikitimaji, utapata miche ya matikiti ipatayo zaidi ya 1200. Kama kila mche utatoa tikitii zipatazo 6 utakuwa na uhakika wa kupata tikitii zipatazo 7200.



Kama kila tikitimaji utaliuza kwa Tshs 1000 shambani utakuwa na uhakika wa kupata Tshs 7,200,000 kwa msimu mmoja. Kwa jinsi tikitii zilivyo, kwa mwaka unaweza kuvuna mara mbili. Hii ni kwa sababu, tikitimaji hukomaa ndani ya miezi 3. Kama umetumia ushauri wa watalaam wa kilimo, na kutumia mbolea za kukuzia na kuimarishia mazao utavuna siyo chini ya mara mbili kwa mwaka na waweza kujipatia zaidi ya Tshs 14,400,000 kwa mwaka ambayo ni takribani Tshs 1,200,000 kwa mwezi. Mahesabu haya siyo ndoto za usiku wala za mchana, bali ni maelezo yaliyo ya uhakika, ukiyafanyia kazi hautabaki maskini maishani mwako.

## **12. Mradi wa Kulea watoto wadogo (Day care centre)**

Kutokana na utandawazi, siku hizi wazazi wote wa kike na kiume wanakimbizana kutafuta riziki. Hapo kale, mzazi wa kiume tu ndiye aliyekimbia huku na kule kitafuta riziki ya familia. Siku hizi wote wanakimbia kutafuta riziki kuanzia asubuhi hadi jioni. Athari hizi za utandawazi na usawa wa kijinsia zimeleta fursa nyingine kwa wajasiriamali. Wazazi wengi ambao ni vijana ambao bado wanazaa watoto wanahitaji mtu makini ambaye anaweza kuwalelea watoto asubuhi hadi jioni wanaporejea nyumbani.

Ukianzisha kituo cha kulelea watoto na ukakitangaza vyema utapata wateja wa kukutosha hasa kwa wanaoishi mijini hasa miji mikubwa. Kama ukiweza kujenga kituo cha kutosha kulea watoto wasiopungua 30 kwa siku wenye umri wa kuanzia miezi 3 hadi miaka 5 unaweza kujipatia kipato kizuri zaidi. Kama kila mtoto atatunzwa kuanzia saa moja asubuhi hadi saa 12 jioni kwa gharama ya Tshs 5000 kwa siku, utakuwa na uhakika wa kujipatia zaidi ya Tshs 150,000 kwa siku sawa na Tshs 4,500,000 kwa mwezi. Kwa Mwaka utakuwa na uhakika wa kukusanya pesa isiyopungua Tshs 54,000,000. Wazazi wengi wanaweza kulipa pesa hiyo endapo tu watahakikishiwa usalama wa watoto wao kuanzia asubuhi wanapoenda kazini hadi jioni wanaporudi nyumbani. Wengi wanaweza kupenda mfumo huu kuliko wa kuajiri msichana/mvulana wa kazi kwani siku hizi watu wengi hawawaamini tena wafanyakazi wao wa majumbani. Mtoto akishafikisha umri wa miaka 5 sasa anaweza kuanza shule ya awali ambapo sasa mzazi atamhamishia shulenii mtoto wake na akaendelea kusoma sasa akitunzwa na shule.

### **13. Mradi wa Kuuza Chakula**

Mradi wa kuuza chakula kwenye Mgahawa wako waweza kukutoa kwenye umaskini endapo utaufanya kwa umakini na ushindani. Kwa mfano kama unafungua mgahawa kwenye mijji mikubwa sana hata ile inayochipukia kama vile Nzega, Tinde, Bariadi, Kakonko, Uvinza, Tunduma, Gairo, Runzewi, Tarime, Ronya, Kyaka, Katoro, nk unaweza kuuza chakula kwa wateja wasiopungua 20 kwa siku. Kama kila miteja utamuuzia chakula kwa bei ya Tshs 2,000 utaweza kupata siyo chini ya Tshs 40,000 kwa siku. Na endapo utakuwa na wateja wanaofikia 40 kwa siku utaweza kupata Tshs 80,000 kwa siku. Kama mgahawa wako utazingatia viwango vya usafi wa hali ya juu, ushindani, viwango vikubwa vya kuwajali wateja; utakuwa na uhakika wa kupata kipato zaidi ya hicho kwa siku. Je, kama utafanya kazi kwa siku 7 kila kila wiki utakosa Tshs 2,400,000 kwa mwezi? Je utakosa Tshs 28,800,000 kwa Mwaka? Kama mugahawa wako utakuwa kwenye mijji mikubwa ambapo kuna idadi kubwa ya watu na ukawa na uhakika wa kuuza sahani angalau 150 za chakula kwa maana ya wateja 150 wanaokula kwa bei ya mijini ya Tshs 3000 au 4000 kwa sahani moja ya wali/ugali kwa nyama, utakuwa na uhakika wa kuuza zaidi ya Tshs 450,000 au 600,000

kwa siku. Kama kwa mwezi utafanya kazi kwa siku 24 tu utakuwa unaweza kufikia mauzo ya Tshs 10,800,000 hadi 14,400,000. Tafakari kisha uende ukayatende.

#### **14. Mradi wa Ushonaji Nguo**

Ushonaji wa nguo na sare za makundi au watu binafsi waweza kukutoa katika lindi la ufukara. Ili kufanikisha mradi huu, unaweza kukodi chumba au kujenga chumba chako eneo lolote unaloona la kibashara. Ni vyema chumba hicho kikawa na uwezo wa kuwa na cherehani Zipatazo 10 au zaidi. Tufanye mfano wa cherehani 10 kama kianzio chako cha mradi. Kwanza Cherehani 10 zitakuwa na uwezo wa kutoa ajira kwa watu 10 na kisha kwako wewe utakuwa na kipato pia.

Kama kwa mfano, utapata nafasi ya kushona nguo za sare za wanafunzi wapatao 300 kwa bei ya Tshs 10,000 kwa kila nguo utawezza kupata fedha isiyopungua 3,000,000 kwa muda wa siku 10 tu. Kama utaweka juhudu kubwa zaidi za kutafuta masoko na kupata shule au vyuo vya kuingia nao mkataba wa kuwashonea sare za wanafunzi, na ukapata taasisi angalau 10 tu zenye wateja wasiopungua 300 na kila nguo ukaishona kwa Tshs 10,000 uwezekano wa kupata Tshs 30,000,000 kwa Mwaka mmoja utakuwa mkubwa zaidi. Ili mradi huu uufanye vizuri lazima uwe na vifaa vya kazi na watendakazi waliofuzu mafunzo ya kushona. Je, umaskini utaendelea kukukamata?

#### **15. Mradi wa Mafuta ya Taa**

Mradi huu unafaa pande zote za mijini na vijijini. Endapo utaamua kuwa mfanyabiashara wa mafuta ya taa tu, unaweza kujiondoa kwenye umaskini wa kipato. Hii ni kutokana na mafuta ya taa kutumiwa na watu wengi sana kote mijini na vijijini. Mijini mafuta yanatumika kwa kazi kuu mbili yaani kupikia na kuwashaa taa hasa wanaishi kwenye nyumba zisizokuwa na umeme. Kwa upande wa vijijini mafuta ya taa yanatumika zaidi kwa ajili ya kupata mwanga kwa kutumia vibatari. Ili kufanikiwa katika biashara ya mafuta ya taa, ni vyema kuwa na wazo la kuuza mafuta mengi zaidi angalau kwa kuanzia uwe na lita zipatazo 200 yaani pipa moja.

Kama lita moja utainunua kwa bei ya Tshs 1700 na ukauza kwa Tshs 2200 kwa lita moja, utakuwa na uwezekano wa kuza takribani Tshs 440,000 ambapo faida yake itakuwa kama Tshs 100,000 kwa kila pipa moja. Kama pipa moja utaliuza kwa wiki moja, utaweza kupata faida ya Tshs 400,000 kwa mwezi. Ukishazoeleka mtaani kwako kwamba wewe ni maarufu kwa kuza mafuta ya taa watu wote hata wafanyabiashara wadogo watakuja kununua kwako na utajikuta unaweza kuza pipa mbili kwa wiki moja au hata pipa tatu kwa wiki moja. Kwenye vijiji vyenye watu wengi na kibashara anayefanya biashara hii anaweza kuza sana kwa mwezi. Ukitaka kufanya biashara hii kwa uzuri zaidi, nakushauri ufanye uchunguzi wa kina zaidi kulingana na eneo unaloishi au unalotaka kufanya biashara hiyo.

## **16. Mradi wa Mafuta ya Magari (Petroleum Station)**

Dunia itaendelea kutumia mafuta kwa miaka mingi sana ijayo. Dunia inatembea juu ya mafuta. Bila mafuta dunia haitembei. Iwe kwa ndege, meli, magari, pikipiki, bajaji, na vyombo vyote vya moto kama mashine za kusaga, mitambo, nk vyote vitaendelea kuhitaji mafuta ya kuendeshea mashine hizo au mitambo yake. Hivyo basi kwa mtu anayefanya mradi huu anaweza kutajirika sana ingawa mradi kama huu umekuwa ukionekana kama ni wa watu matajiri sana. Ukweli ni kwamba hata wewe unaweza kuufanya na ukapata utajiri mkubwa. Mradi huu unapendelewa kufanya kandokando ya barabara kuu ambapo magari mengi yanapita. Hata hivyo siyo lazima iwe kando ya barabara kuu. Kama ukipata eneo zuri mjini au hata nje ya mji ili mradi panafikika na panaonekana na waendesha magari au unapatangaza vyema, wenyе magari watakuifuata.

Mradi wa mafuta ya magari (petroleum and diesel fuels) unaweza kuuanzisha hata kama wewe unajiona huna utajiri. Ni kuamua tu na kuanza kufanya utafiti na kuuliza waliokutangulia. Mradi huu kama unaufanya kwa hakika huwezi ukamaliza siku nzima bila kuza mafuta kwa wenyе magari madogo na makubwa. Kwa siku huwezi kukosa kuza zaidi ya lita 300 sawa na wateja 30 tu wenyе Kununua lita 10 tu kila mmoja kwa wastani. Endapo utauza lita 300 kwa siku kwa wastani, utakuwa umeuza kiwango kisichopungua Tshs 660,000 kwa siku kama lita moja ya mafuta utaiuza kwa Tshs 2200. Kama ulinunua lita moja kwa bei ya jumla ya Tshs 1700

utakuwa umepata faida ya Tshs 150,000 kwa siku. Mradi huu ni mkubwa sana hivyo nashauri mtu mwenye ndoto ya kufungua mradi kama huu afanye juhudzi zaidi za kuuliza wengine, aulize watu zaidi ya 3 wanaofanya biashara hii kabla ya kuanza kutekeleza wazo lake.

## **17. Mradi wa Kuagiza bidhaa toka nje ya nchi**

Inashauriwa kwamba ili uchumi wa nchi ukue, ni vyema bidhaa na huduma zinazoagizwa kutoka nje ya nchi zisizidi zile zinazokwenda nje ya nchi hiyo. Kwa mfano kama nguo zinazovaliwa na watanzania nyngi zimetoka nje ya nchi kuliko zile zinazoshonwa au kuzalishwa nchini na mfano huo ukiuweka kwenye kila bidhaa, matokeo yake thamani ya fedha ya Tanzania itazidi kushuka kila kukicha. Hata kama mfumko wa bei utashuka, kama wananchi bado wanatumia bidhaa nyngi kutoka nje ya nchi kuliko wanazopeleka nje, uchumi wa nchi utazidi kuyumba sana.

Ili kanuni hiyo ifanye kazi vyema, unapotaka kufanya mradi wowote wa kuagiza bidhaa toka nje, inashauriwa kwamba uagize bidhaa au huduma ambazo kimsingi hazipatikani nchini. Kwa mfano siyo busara kuagiza samaki kutoka Japan wakati samaki kama hao hao wanapatikana Tanzania. Siyo busara kuagiza vitanda, meza na viti vya maofisini kutoka nchini China au Marekani wakati meza kama hizo zinapatikana VETA ya Tanzania. Siyo busara hata kidogo kumtafuta mshauri kutoka Ulaya, Urusi, Japan au China ili aje kukupa ushauri wa kutengeneza barabara au madaraja ya barabara zetu wakati mtalaam kama huyo yupo Tanzania.

Kwa hiyo hakikisha kwamba unaagiza bidhaa ambazo ni adimu hapa nchini na uwe umefanya utafiti kama zinapendwa hapa nchini kabla ya kuziagiza. Endapo utaziagiza hakikisha pia kwamba umepata vibali vyote vya mamlaka husika kutoka serikalini na ujilidhishe kwamba bidhaa hiyo imekidhi vigezo vyote vya kisheria. Ukitanya hivyo, utapata faida kubwa sana na kujipatia utajiri mkubwa sana.

## **18. Mradi wa Biashara ya Vipodozi**

Kama ukifanya utafiti zaidi wa biashara hii, utagundua kuwa ni biashara inayolipa. Hata hivyo, biashara hii imeingiliwa na bidhaa bandia kwa wingi

na hivyo kuhatarisha afya ya watumiaji wengi hasa wanawake ambao ndio watumiaji wakubwa wa vipodozi. Katika kitabu hiki ni vyema nikakutaka ufanye biashara ya vipodozi visivyo na madhara kwa watumiaji.



**Kutunza ngozi**

- Kuhifadhi unyevu wa asili wa ngozi
- Kurudisha uimara wa ngozi
- Kurudisha upya wa muonekano wa ngozi
- Sekta yenyewe mauzo ya thamani ya trilliuni 4

Vipodozi vyenye madhara kwa watumiaji haviruhusiwi hata kidogo na mamlaka za nchi na ujue kuwa endapo utakamatwa na mamlaka husika utafilisiwa biashara yako na utarudi katika umaskini. Kama hujui vipodozi vyeye madhara kwa afya za watumiaji ni vyema ukawatafuta watalaaam kutoka mamlaka ya dawa na Vyakula yaani Tanzania Foods and Drugs Authority (TFDA) wakushauri kuhusu vipodozi kabla ya kuanza biashara. Aidha, kumbuka kwamba ni lazima uwe na leseni halali ya kuendesha biashara kama hiyo au biashara yoyote. Epuka kufanya biashara ukiwa huna leseni halali kutoka kwenye mamlaka husika za nchi, utapata hasara ambayo hutaisahau milele.

Biashara ya vipodozi hasa visivyokuwa na madhara, inaweza kukulipa na ukawa tajiri hapo mjini ulipo. Inashauriwa tena kwamba ni vyema ukafanya upelelezi, uchunguzi, na utafute elimu zaidi kuhusu biashara hii kabla hujaianza. Uliza na upeleleze taarifa kuhusu taratibu za kisheria, taratibu za manunuza na mauzo ya bidhaa, bei na faida inayotokana na biashara hii. Ukweli ni kwamba kama eneo ulilopo ni la kibiashara au lina watu wengi ni hakika utapata kipato cha kukutosha wewe na familia yako. Ni hakika utapata utajiri wa kukutosha sana.

Vipodozi asilia siku hizi ndivyo viko kwenye ushindani zaidi. Watu wengi wanapenda vipodozi visivyokuwa na madhara hasa vile vyenye kurudisha

---

afya ya mtumiaji. Changamoto zake tu ni bei kubwa sana ikilinganishwa nq vipodozi vya kawaida. Kwa mfano, vipodozi kama vile vinavyosambazwa na kampuni za bidhaa asilia kwa kutumia mfumo wao wa soko mtandao (Mult Level Martketing companies) ni vipodozi vilivyodhihirika kuwa na matokeo mazuri kwa watumiaji. Vipodozi kutoka kampuni kama vile Forever Living Products Ltd, Dynapharm International Ltd, GNLD, nk ni vipodozi ambavyo watumiaji wengi wamevisifia zaidi na wengi wanaovifanyia biashara wamefanikiwa. Ukifanya biashara ya vipodozi vya asili hakika vinalipa. Hata hivyo, kama utaamua kufanya biashara ya vipodozi vya kawaida bado pia utapata malipo makubwa. Hautajuta kufanya biashara au mradi wa vipodozi. Fanya utafiti na upelelezi wa kutosha kutoka kwa wengine walioikutangulia kabla ya kufanya biashara hiyo.

## **19. Mradi wa Biashara ya Mapambo**

Watu wanaofahamu biashara ya mapambo watakubaliana na mimi kwamba biashara ya mapambo ya msimu na yale yasiyokuwa ya msimu yanapendwa na watu wengi sana. Mapambo yanaweza kuwa yale ya asili, kama vile; vinyago, maua mabichi au maua pori na mapambo makavu yaani mapambo ya kutengenezwa. Mapambo mengine ni kama vile; mapambo ya vito vya thamani kama pete, heleni, mikufu, shanga, kofia, mitandio ya wanawake, viatu, nk. Mapambo ya makanisani, mapambo ya kwenye mikutano ya hadhara kama vile mikutano ya Injili, siasa, harambee, nk nayo ni mapambo yanayoweza kukupatia kipato. Ukifanya kuwa ndiyo mradi wako wa kudumu na ukawa na mtandao mkubwa wa wateja waweza kupata utajiri wa kukutosha kabisa. Kama kila wiki utapata zabuni ya kupamba ukumbi angalau mmoja kwa malipo ya zaidi ya Tshs 300,000 huenda kwa mwezi ukajikusanya kitita cha Tshs 1,200,000 kutoka kwenye kazi hiyo.

## **20. Mradi wa Duka la Dawa za Binadamu (Pharmacy)**

Dawa za kutibu magonjwa ya mwanadamu zinafahamika sana. Kuendesha mradi wa dawa hizi kunaweza kabisa kumaliza matatizo yako ya kipato huku ukiimarisha afya za wananchi. Hata hivyo, kumbuka kwamba biashara ya kuuza dawa za kutibu maradhi ya binadamu inalindwa na

sheria za mamlaka ya chakula na dawa TFDA chini ya Wizara ya Afya na Bodi za Famasia nchini. Hivyo lazima uhakikishe kwamba mamlaka hizo zote umezitembelea ili kupata mwongozo wa biashara hiyo kabla hujaanza lolote. Kutokana na hali ya afya za watanzania, mfumo wa maisha, ukosefu wa maisha ya kiafya (unhealthy living style) na mifumo mibovu mingi ya maisha yetu watanzania, afya zetu zitaendelea kuhitaji tiba za kisasa pamoja na zile za asili pia.

Kutokana na hali hiyo, biashara ya dawa za kutibu maradhi ya binadamu itaendelea kuwa kubwa zaidi. Kwa uhakika kabisa kama utazingatia taratibu zote za kisheria katika kuendesha biashara hii, hautabaki kuwa maskini kwa kuendesha biashara hii. Kumbuka kuwa siyo lazima uwe na elimu ya afya ndipo uweze kufanya mradi wa duka dogo, la kati au kubwa la dawa za binadamu. Kinachotakiwa ni wewe kuwa na vibali halali kisheria. Kama wewe unataka kufanya biashara hii unachotakiwa ni kujiamini na kuhakikisha kuwa wazo hili umelipenda na unataka ulifanyie kazi. Jambo la pili, kama wewe hujasomea maswala ya afya na wala hauna hata chetichochote cha maswala ya dawa wala afya wewe usiwe na wasiwasi songa mbele na wazo lako. Ukweli ni kwamba ukiamua utapata wafanyakazi waliosomea fani hiyo. Wewe jiandae kuajiri watalaam waliosomea na ukubali ushauri wao na uwasililize wao katika uendeshaji. Wewe unachotakiwa kufuatilia ni faida au hasara ya biashara yako. Waweza kuanzisha duka kubwa la Famasi, duka kubwa la Dawa, duka dogo la Dawa kijijini au mjini, nk.

Kama umesomea fani hii ya afya wewe unayo fursa nzuri zaidi kuliko ambaye hajasomea fani hiyo. Kama wewe umesomea fani ya afya nakushauri usifikirie hata kutafuta ajira. Fikiria kujajiri zaidi kuliko kuajiriwa. Wewe fikiria kuanzisha biashara yako. Fikiria wazo hilo vyema na kisha tafuta mtaji. Usitafute mtaji wa kufanya duka la dawa au Famasi kabla ya kufanya utafiti na upelelezi wa taarifa muhimu za uendeshaji wa biashara hiyo. Jifunze kwanza kwa waliotangulia. Watafute waliofanikiwa au walioshindwa uwaulize kwa nini wamefanikiwa au kwa nini hawakufanikiwa. Sababu watakazokupatia uzitumie kuanzisha biashara hiyo ukiwa na tahadhari au ukiwa na ujasili zaidi wa kufanikiwa. Kumbuka Biashara ya dawa za binadamu ni biashara ya ubinadamu naam ni biashara ya kitajiri pia.

## **21. Mradi wa Dawa za Tiba Asili**

Dawa za asili (herbal natural medicine) zimekuwa kimbilio la watu wengi siku za hivi karibuni. Yawezekana imetokana na matangazo mengi ambayo yamekuwa yakinolewa na watoa huduma wenyewe. Watoa huduma wametumia mbinu nyingi kutoa elimu ikiwemo kutumia mbinu za biashara ya mtandao, televisheni, radio, mitandao ya kijamii na magazeti.

Dawa za asili zimeendelea kuchukua nafasi kubwa sana ya dawa za hospitali zilizoletwa na wakoloni. Ikumbukwe kwamba kabla ya ujio wa wakoloni waafrika wote walitumia njia za asili kujipatia matibabu. Mfumo wa hospitali za sasa (conventional medicine) uliletwa na wakoloni na ukaendelezwa na serikali zetu zilizofuatia. Kufumka kwa dawa za asili na kuchukua nafasi kubwa hata kuwa kimbilio la wananchi wengi inatafsiriwa kuwa ni ishara ya kushindwa kwa mfumo wa hospitali za asili ya Ulaya au Magharibi. Hali hii inafanya biashara ya dawa asilia izidi kuwa kubwa sana hapa Tanzania.

Kwa wale wanaoifanya biashara hii hapa Tanzania hasa wale wanaoitangaza wameweza kuwa matajiri wakubwa hapa Tanzania. Dawa asilia zinazosemwa hapa siyo kupiga ramli au kupunga pepo na mizimu bali ni dawa asilia kutokana na matunda, mbogamboga, magome ya miti, mizizi ya miti na majani yake. Kwa mfano mboga za majani au matunda kama machungwa, limao, mapera, tikitimaji, matango, aloevera, parachichi au avocado, nk ni mazao ya miti ambayo yakinengenezwa vyema kitalaam huwa tiba ya magonjwa mbalimbali. Hii ndiyo tiba asilia inazungumzwa hapa.

Si lazima wewe uwe mtengenezaji wa dawa. Wewe waweza kuwa mnunuzi wa dawa hizo na kuziwa kutoka kwa watengenezaji. Unaweza kuwa Wakala wa watengenezaji wa dawa hizo za asili. Kwa kuwa wakala wa makampuni ya dawa za asili, hakika unaweza kutajirika sana. Waweza kuingia mkataba wa kuwa wakala wa watengenezaji wa dawa hizo. Yapo makampuni mengi sana yanayotengeneza dawa asilia kama kampuni za Dynapharm International ya Malaysia, Forever Living Products ya Marekani, Tians ya China, na makampuni mengine mengi ya humu nchini na yanayotoka nje ya nchi.

Dawa za asili zipo za kutibu magonjwa mengi sana. Zipo zinazotibu hata magonjwa yaliyoshindikana hospitalini. Magonjwa mengi yanayowasumbua watu wengi ni pamoja na matatizo ya uzazi, utasa/ugumba, maambukizo ya njia za uzazi hasa kwa wanawake, upungufu wa nguvu za kiume, kisukari, presha, magonjwa ya tumbo, ngozi, na mengine kama hayo. Kwa kuza dawa zinazotibu magonjwa hayo utajikuta wewe ukitajirika sana. Endapo utakuwa umependa kufanya biashara hii unashauriwa kuwafuata wanaofanya ili upate habari zaidi kuhusu biashara hii. Na ukweli ni kwamba hautakuwa maskini kwa kufanya biashara ya dawa za asili. Kumbuka kuwa na vibali vyote vya lazima kabla ya kuanza biashara hii. Utajiri unakusubiri kama utafanya biashara hii kwa kufungua duka kubwa, au kituo cha kuhudumia watu wenyе mahitaji ya dawa hizo. Waweza kuanza na mtaji mdogo wa milioni moja tu (1,000,000.00) na matokeo yake utayapata ndani ya muda mfupi. Wapo wanaofanya miradi hii kwa kutumia uongo au kutafuta kujipatia pesa tu. Wewe unapaswa kuwa mkweli na ufanye biashara hii kwa nia ya kusaidia afya za watumiaji. Ni lazima usukumwe na kutatua tatizo la afya. Usisukumwe na kutafuta pesa, sukumwa na matatizo ya afya za watu. Kwa kutatua matatizo ya afya za watu, wewe utatua matatizo huku ukitajirika. Ukiamua leo, mwakani hautakuwa kama ulivyo leo kifedha.

## **22. Mradi wa Kutoa na Kuweka Pesa (M-PESA, TIGO PESA, AIRTEL MONEY, nk)**

Huduma au Biashara ya kutoa au Kuweka fedha kwa kutumia simu imepamba moto kote nchini kuanzia miaka ya 2005 kuelekea miaka ya 2015. Kwa sasa huduma hii imetapakaa karibu kona zote za Tanzania. Huduma hii imekuwa mkombozi sana kwa watanzania wengi wenyе kipato kidogo hata wenyе kipato kikubwa katika kusafirisha fedha kutoka upande mmoja kwenda mwingine ndani na nje ya nchi. Ni huduma ambayo itaendelea kuwa ya manufaa na ya kukimbiliwa na watu wengi kote duniani katika kusafirisha fedha hata kufanya manunuzi ya bidhaa na huduma. Kwa Tanzania huduma hii ni maarufu sana kwa sasa na hivyo watu wengi wataendelea kuitegemea na kuifanya kila kona ya nchi.

Kama ukiifanya kazi hii kwa umakini na kwa mpangilio mzuri, ukweli ni kwamba ni huduma inayoweza kukupatia kipato cha kukutosha kabisa

kuondoka kwenye umasikini. Kwa siku unaweza kuingiza kipato kuanzia Tshs 10,000 hadi 50,000 kutegemeana na eneo ulilopo na ushindani ulivyo eneo hilo. Kwa mwezi unaweza kujipatia hadi Tshs 1,500,000 kwa kazi hiyo. Endapo utakuwa umeipenda huduma hii kama kawaida peleleza vyema taarifa muhimu, chunguza wanaoindesha, tafuta taarifa za upande wa mafanikio na matatizo wanayokumbana nayo kwenye biashara hiyo. Usitafute habari za upande mmoja wa faida tu bali pande zote za faida na hasara kwa biashara hiyo. Ukichachunguza faida na hasara za biashara ndipo uamue kuifanya ukiwa umejipanga vyema kukabiliana na changamoto za biashara hiyo.

### **23. Mradi wa Kuuza Vitafunwa**

Kupata utajiri ni kuamua. Kubakia maskini maisha yote ni kuamua pia. Ukihamua akilini mwako, moyoni mwako, nafsini mwako na kwenye fikra zako kwamba unataka uondokane na umaskini kwa kuuza chapati tu, inawezekana kabisa. Mradi wa kuuza Chapati tu waweza kukufanya bilionea. Chapati ni moja ya vitafunwa vinavyopendwa sana hapa Tanzania. Sehemu nyingi nchini chapati huuzwa kati ya Tshs 300 hadi 500. Mjini Kigoma kwa mfano chapati au sambusa moja huuzwa kwa Tshs 500 kwenye migahawa mingi ya mjini. Mjasiliamali akiamua kuwekeza kwenye mradi wa vitafunwa aina ya chapati peke yake anaweza akamaliza umaskini wa kipato kwa muda mfupi. Kama imewezeekana kwa Said Bakharesa ambaye kwa sasa ni bilionea Tanzania, kwa nini kwako isiwezekane? Amua leo, kesho utaona ajabu.

Kwa mfano mjasiliamali anayeamua kuuza chapati 500 tu kwa siku kwa bei ya Tshs 300 anaweza kujipatia pesa ipatayo Tshs 150,000 kwa siku. Chapati 500 ni sawa na wateja 250 kwa siku wenye uwezo wa Kununua chapatti mbili mbili kwa siku au ni sawa na familia zipatazo 50 zenye Kununua chapatti 10 kila familia. Ukihamua kufanya kazi ya kuuza chapati kwa kufuata kanuni ya kuteka soko inawezekana.

Wateja kama hao au zaidi ya hao unaweza ukawapata hasa kwenye miji mikubwa kama Dar es salaam, Mwanza, Mbeya, Arusha, Tanga, Morogoro au karibu na vyuo vya elimu ya juu ambapo wanafunzi wengi

asubuhi watakuwa wanahitaji kupata vitafunwa na chai. Hata maeneo yenye wafanyakazi wengi hasa kwenye maeneo ya machimbo ya madini, maeneo ya ujenzi wa nyumba kama maghorofa, maeneo ya Wizara za Serikali au Halmashauri, wateja 250 kawapata ni jambo linalowezekana. Kama utapata kipato cha Tshs 150,000 kwa siku ni hakika kwamba kwa mwezi utapata zaidi ya Tshs 3,000,000 hapa ikiwa ni hesabu ya mapato baada ya matumizi ya wasaidizi, nishati, mafuta, na usafirishaji.

Kwa Mwaka utakuwa na uhakika wa kipato kisichopungua Tshs 36,000,000. Je hapo hujaanza kuwa milionea. Je utawekwa tena kwenye kundi la watu wenye kuishi chini ya dola moja kwa siku yaani chini ya pato la Tshs 1600 kwa siku? Hapana hapa unakoelekea ni kwenye umilionea kwanza kisha ubilionea.

## **24. Mradi wa Majani ya Rossela**

Zao la majani haya ya Rosella lina soko kubwa ndani na nje ya nchi. Rosella sasa hivi ni zao linalopendwa sana sehemu nyingi hapa Tanzania kutokana na virutubisho vilivyomo ndani yake. Ni majani mekundu yanayofaa kwa afya ya mtumiaji. Majani hayo huongeza damu kwa wingi mwilini. Wagonjwa wenye matatizo ya upungufu wa damu hasa watoto, wajawazito, na wazee hushauriwa kutumia juice ya majani haya. Hospitalini wakigundua kuwa una tatizo la kupungukiwa damu, ushauri wao wa kwanza ni kutafuta majani hayo ya rossela uchemshe majai yake kisha unywe juisi yake.

Kibiashara majani haya yanalipa sana. Mfano; robo kilo ya majani makavu ya rossela yanauzwa kwa Tshs 3500 katika maduka makubwa (supermarkets) Tanzania. Hii ina maana kwamba kilo moja huuzwa kwa Tshs 14,000. Hii ni bei ya Mwaka 2009 hadi 2012 kwa taarifa zilizokuwepo katika maduka mengi jijini Mwanza na sehemu nyingi nchini. Unaweza kufanya biashara hii kwa kuamua kulima zao hili, ukafungasha vyema na ukasambaza wewe mwenyewe kwenye maduka makubwa nchini au kwa wenye viwanda vidogo vya kutengeneza wine, jam ya mikate, juisi na majani ya chai. Kwa ufupi ni kwamba zao la rossela litaendelea kuhitajika kwani lina manufaa makubwa kiafya na kiuchumi. Kwa mfano ukipata kilo 2000 kwa msimu mmoja na ukauza kilo moja kwa Tshs 9000 utakuwa na uhakika wa kupata Tshs 18,000,000 kwa msimu mmoja.

Kiwango kama hicho cha mapato ya mamilioni kinaweza kuwa kikubwa sana ambacho mkulima wa tumbaku mkoani Tabora, Ruvuma au Kibondo Kigoma hajawahi kupata tangu alime tumbaku maishani mwake. Lakini mkulima wa Rossela anaweza kulima hekari tano tu akapata zaidi ya kilo 3000 na akiuza mwenyewe sokoni anaweza kupata zaidi ya Tshs 18,000,000 bila tatizo lolote. Endapo utapenda kuifanya biashara hii, unashauriwa kunitafuta mimi mwandishi wa kitabu hiki kwa namba zilizoko mwanzoni mwa kitabu hiki au tafuta watalaam wa kilimo wakuelekeze zaidi. Aidha, unaweza kwenda maduka makubwa ya biashara (supermarkets) ili ufanye utafiti bei na taarifa nyingine muhimu kadri utakavyohitaji ili ufanye kitu kwa uhakika zaidi.

## **25. Mradi wa Kilimo cha Uyoga**

Mradi wa kulima uyogalishe unaleta utajiri mkubwa sana. Wote waliofanya mradi huu hawakubaki maskini maishani mwao. Uyoga una soko sana kila kona. Ukilima kwa kufuata utalaam na ukapata soko la uhakika kwenye Hoteli kubwa na supermarket wewe utasahau umaskini ndani ya mwaka mmoja. Uyoga lishe unauzwa kwa kilo. Kama kilo moja itauzwa kwa bei ndogo kwenye Hoteli za kitalii au Supermarket itakuwa ni Tshs 5,000 kwa kilo.

Unaweza kulima uyoga-lishe hata ukiwa na eneo dogo tu kama chumba chako cha kulala. Uyoga lishe unalimwa chumbani penye giza totoro. Ukiwa na nyumba yako unaweza kuamua chumba kimoja ukitumie kulima uyoga. Uyoga unalimwa kwa kutumia uchafu au mabaki ya mpunga, mabaki ya mbao, mabaki ya mahindi, nk. Kilimo cha uyoga lishe ni kilimo rahisi ukiamua unaweza. Ukipenda kulima uyoga nakushauri uwatafute maafisa Kilimo wakushauri na wakupe mbinu na ujuzi zaidi. Nakuhakikishia ukilima uyoga hautabaki kuwa maskini wa kipato.

Kama unaweza kuvuna kilo 1000 tu kila mwezi ukauza kwenye Hoteli kubwa au za kati kwa bei ya Tshs 5,000 tu ni wazi kwamba utajipatia kipato kizuri sana kinachofikia Tshs 5,000,000 kwa mwezi. Kipato hiki unaweza kukipata kutoka chumbani mwako. Ukitumia chumba kimoja tu cha nyumba yako chenye ukubwa wa mita 3 za mraba, iwe mjini au vijijini unaweza kujipatia kipato hicho.

## **26. Mradi wa Ng'ombe wa Maziwa**

Endapo mjasiriamali ataamua Kufuga ng'ombe wapatao 5 tu wa maziwa na akafuata taratibu zote za kitalaam, atanufaika na mradi huu kwa kiwango cha juu sana. Ng'ombe wa maziwa akifugwa vyema anaweza kutoa hadi lita 20 kwa siku. Ushahidi huu nimeupata kwa mama mmoja ambaye ni mwalimu katika jiji la Mbeya ambaye amefuga ng'ombe kwa kutumia utalaam wa kawaida tu na anapata lita 10 asubuhi na 10 jioni kutoka kwa ng'ombe mmoja tu. Huyu mama anao ngo'mbe wapatao 6 na ametajirika kwa hakika ukiona maisha yake utayatamani na kumwonea vivu.

Kwa hiyo kama mjasiriamali akifuga ng'ombe 5 na kila mmoja akatoa kwa uchache lita 15 tu za maziwa kwa siku atakuwa na uwezo wa kupata lita 75 za maziwa kila siku. Kama lita moja itauzwa kwa Tshs 1000 tu ni dhahiri mtu huyu atakuwa na uwezo wa kupata pesa zisizopungua Tshs 75,000 kwa siku. Hii ndiyo kusema atakuwa na kipato kisichopungua Tshs 2,2500,000 kwa mwezi. Kumbuka hapa tumefanya hesabu ndogo tu ya ng'ombe wasiozidi watano, je kama ukifuga ng'ombe wapato 10 tu na wote wakawa wa maziwa? Huoni kwamba utapata zaidi ya Tshs 4,000,000 kwa mwezi? Kama wewe unalo eneo la ardhi ipatayo nusu ekari au robo ekari ambalo hulitumii kwa sasa; jaribu kutafuta mtaji kwa hali na mali ufanye mradi huu na ninakuahidi kwamba mwakani utakuwa tofauti.

## **27. Mradi wa Maji ya Kunywa**

Mradi huu wa kuuza maji ya kunywa kwenye madumu ya lita 20, ulianzia jijini Dar es Salaam miaka ya 1995. Vijana wengi jijini Dar es Salaam walikuwa wakiufanya mradi huo kwa kusomba maji kutoka maeneo ya mbali na kuwauzia watu wenye uhitaji wa maji ya kunywa majumbani mwao.

Kwa sasa dumu moja la maji linauzwa Tshs 1000 kwenye miji mingi hapa Tanzania. Kama mjasiliamali anaweza kuwa na wateja (familia) wapatao 20 kwa siku anaowauzia madumu angalau 20 kwa siku atakuwa na uhakika wa kupata Tshs 20,000 kwa siku. Mradi huu wengi huufanya kwa kutumia baiskeli au mikokoteni. Mtaji pekee unaohitajika ni nguvu zako na baiskeli au mkokoteni na madumu ya lita 20 ili kuyatumia kusambazia

maji kwa wateja. Hapa kuna matumaini ya kupata Tshs 600,000 kwa mwezi kwa kijana anayeamua kufanya mradi huu. Mjasiriamali wa kazi kama hii, anapaswa kuzingatia usafi, uaminifu na ukweli kuhusu maji anayoyasambaza kwani wakati mwininge inatakiwa kuwa na vibali nya mamlaka husika kama EWURA, au mamlaka za maji mijini. Aidha, kama wateja watagundua kwamba unawasambazia maji yasiyokuwa safi wala salama hawataendelea kuwa wateja wako. Kumbuka maji ni uhai. Unapaswa kutunza vyanzo nya maji kwa kupanda miti na usafi maeneo ya kuchotea maji kama ni kwenye chemichemi au visima au bomba ili uweze kuendelea kusambazia watu maji.

Kumbuka kuwa unaweza kuamua kufanya mradi huu wa kusambaza maji safi ya kunywa kwa upana zaidi na kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Kama una mtaji mkubwa zaidi unaweza kutumia gari kubwa aina ya TANKER. Kama utagundua kuwa kuna maeneo hawana maji majumbani wala ya kunywa ni fursa yako sasa kuamua kutumia hata tankers kubwa kusambazia maji kwa wananchi. Hakikisha unacho kibali cha mamlaka husika za maji na usalama wa chakula na dawa. Kwa mfano kwa wale wanaoishi jijini Dar es salaam wanajua jinsi swala la maji lilivyo tete maeneo mengi ya jiji.

Kwa wajasiliamali wenye kutumia fursa kama hizo wanaweza kuanzisha kampuni za kusambaza maji kwa wananchi kwa kutumia tankers. Kama kila lita watauza kwa Tshs 20 tu na tanker linabeba maji safi yapatayo lita za ujazo kama 20,000 kwa siku, wataweza kuuza maji hayo kwa Tshs 400,000 kwa siku. Kwa mwezi anaweza kujipatia zaidi ya Tshs 400,000 x 30 = 12,000,000.00. Kwa maeneo yenye tatizo la maji sana kuuza lita za maji zaidi ya 20,000 ni jambo la kawaida kabisa. Kumbuka kuwa lita elfu ishirini ni kama takribani madumu ya maji 1000 tu yenye ujazo wa lita 20 kila moja. Madumu ya maji yapatayo 1000 ni sawa na matumizi ya familia 100 tu kwa siku zenyenye uwezo wa kutumia madumu 10 kwa siku. Hapa mjasiliamali anaweza kutumia mtandao wa familia 100 katika mtaa mmoja tu na akawa anawasambazia maji majumbani mwao kwa bei ya Tshs 400 kwa ndoo moja ya maji. Kwa watu wanaoishi miji mikubwa ambapo pana shida kubwa ya maji, fursa kama hii inapaswa kuwa ya kwao.

## **28. Mradi wa Maji ya Chupa**

Kunywa maji ya chupa hapo awali ilionekana kama swala la anasa. Mtu aliyeonekana akinywa maji yaliyotiwa kwenye chupa alitafsiriwa kwamba ni mwenye maringo na mwenye pesa nyingi. Aidha, kuuza maji au Kununua maji ilionekana kama swala lisilokubalika kabisa. Siku hizi hasa kuanzia miaka ya 2005 na kuendelea kutumia maji ya chupa siyo tena swala la anasa bali limekuwa swala la afya. Watu wengi hunywa maji ya chupa kila mahali. Kila sehemu siku hizi watu wanakunywa maji ya chupa. Mikutanoni, kwenye semina, kwenye vikao, kwenye sherehe kubwa na ndogo, kwenye safari, kwenye mabaa, nk kila mahali watu hunywa maji ya chupa. Kutokana na fursa hii, watu wengi wanaanzisha miradi ya maji ya kunywa kwenye chupa za plastiki katika ujazo wa lita tofauti kuanzia mililita 200, mililita 300, Lita 0.5, lita 1, Lita 1.5, Lita 2, Lita 3, na lita 5. Miradi ya kuuza maji ya kunywa kwenye chupa ni miradi ambayo inafanywa na matajiri. Kama unataka uwe tajiri mkubwa, mradi wa kuuza maji ya chupa ni furasa ambayo inaweza kukupa utajiri mkubwa sana.

Kwa kuwa kitabu hiki kinaeleza kwa mifano na kwa mchanganuo ni vyema nikakupa mchanganuo mdogo tu ambao utakupa picha kamili. Kama utaanzisha mradi huu na kwa uchache ukawa unasambaza chupa za ujazo wa lita 1,000,000 kwa mwezi na kila lita moja ukawa unauza kwa Tshs 600 tu utaweza kukusanya zaidi ya Tshs 600,000,000 kwa mwezi. Kumbuka kwamba mradi unaoingiza shilingi milioni 600 kwa mwezi siyo mradi mdogo. Kama utaweza kusambaza na kuuza lita 10,000,000 kwa mwezi kutegemeana na uwezo wako, tarajia kwamba kwa mwezi huo utajipatia si chini ya Tshs 6,000,000,000 kwa mwezi kama mauzo ya jumla. Yaani utapata shilingi bilioni sita kwa mwezi. Hata kama gharama za uendeshaji na usambazaji zitakuwa takribani 50% bado wewe mwenye mradi lazima utabakia na nusu ya mauzo yaani bilioni tatu kwa mwezi zitakuwa zako. Je hujawa bilionea? Anza sasa na wewe uitwe bilionea. Kumbuka kuwa ni ukweli ulio wazi kwamba kuuza lita milioni kumi kwa mwezi inawezekana kabisa. Haupaswi kushangaa ukisikia kwamba kuna mabilionea hapa Tanzania kama akina Reginald Mengi, Said Bakhera, na wengineo. Kama unataka uwe bilionea muuza maji ya kunywa, anza mchakato leo

wa kufungua kampuni ya kuuza maji ya kunywa kwenye chupa na wewe utashangaa.

Hata hivyo, biashara ya kuuza maji ya kunywa kwenye chupa za plastiki ni lazima iwe na vibali vyote vya mamlaka husika kisheria na kijamii. Kwa upande wa upatikanaji wa maji safi ni lazima uwe na chanzo cha maji kisichokauka kamwe ili mradi wako uweze kuwa endelevu. Kama kuna sehemu unajua kwamba kuna chanzo cha maji safi yanayokidhi viwango vya kimataifa na kitaifa unaweza kuanza mradi wa kuuza maji. Hakikisha kwamba maji utakayoyatumia hayawi na ukakasi mkubwa yaani pH 7.0 ndio inayopendekezwa duniani kote. Kwa mfano maji ya Chupa ya Kilimanjaro yana madini ambayo yanakubalika kimataifa na kitaifa. Hii inayafanya yaweze kupata vibali vyote vinavyohitajika bila kipingamizi.

## **29. Mradi wa Kuandika Vitabu**

Ukiamua kuwa mwandishi wa vitabu vyenye kugusa watu wengi, vyenye mada motomoto, vitakutajirisha sana mpaka utashangaa. Watu wengi wanamfahamu mzee Ngugi wa Thiong’O. Huyu ni mwandishi mahiri sana wa nchini Kenya. Ametajirishwa sana na vitabu alivyoandika tangu enzi za wakoloni na baada ya ukoloni. Upande wa Tanzania wengi wanamfahamu mbunge mmoja wa Tarime anayeitwa Chacha Nyambari Nyangwine. Huyu ameandika vitabu vingi sana na Vimemtajirisha sana. Pia watanzania wengi watakuwa wanamfahamu kijana mmoja anaitwa Erick Shigongo, huyu amekuwa mwandishi mzuri sana wa vitabu vya riwaya za mapenzi na ujasiliamali. Kwa sasa ni tajiri mkubwa jijini Dar es Salaam. Pia anamiliki kampuni za magazeti mengi yanayopendwa na kusomwa sana nchini kote Tanzania kama vile gazeti la Champion, UWAZI, Ijumaa, nk. Kusema ukweli huyu bwana Erick Shigongo ameshatajirika sana kutohakana na uandishi wa vitabu na riwaya za kila aina.

Kwa mfano kama wewe unao ujuzi wa jambo fulani, au unahisi una kipaji cha kuandika riwaya zenyé kusimua wasomaji, ukiandika kitabu na kikauzwa sana kikapendwa sana kote nchini, unaweza ukawa milionea baada ya muda mfupi. Kwa mfano Kama ukiandika kitabu na ukatoa nakala zipatazo 20,000 tu na kitabu hicho ukakiwa sokoni kwa Tshs 5,000 tu

utakuwa na uhakika wa kupata zaidi ya Tshs 100,000,000 kwa mzunguko mmoja tu wa kuuza kitabu hicho. Na endapo utakiuza kwa Tshs 10,000 utakuwa na uwezo wa kupata mauzo ya pesa zipatazo Tshs 200,000,000 kwa mwaka mmoja au miwili tu ambapo kitabu chako kitakuwa kimeuzwa maeneo kadhaa.

Na kama utafanikiwa kuchapisha nakala zipatazo 100,000 na zote zikauzwa sokoni kwa muda tufanye wa miaka miwili, ukauza kwa bei ya Tshs 10,000 kwa kitabu kimoja; utaweza kukusanya kiasi cha pesa zipatazo Tshs 1,000,000,000 (bilioni moja). Je, kama kitabu chako kimependwa nchini na nje ya nchi na ukauza nakala kama laki tano tu itakuwaje? Si utakuwa bilionea wa nguvu hapa Tanzania? Hebu tazama utapata pesa kiasi gani ukiuza nakala  $500,000 \times 10,000 = 5,000,000,000$ . Hapo ndiyo kusema kuwa utapata shilingi 5 bilioni kwa kuza nakala laki tano tu. Duniani kote waandishi wengi wa vitabu ni mabilionea wakubwa. Mabilionea wengi Amerika na Ulaya wamepata ubilionea kutokana na uandishi wa vitabu. Ungana na matajiri wakubwa wa dunia kwa kuandika vitabu vingi zaidi. Kama wewe ni daktari andika vitabu, nawe utatajirika zaidi. Kama wewe ni mtalaam wa kilimo, mtalaam wa uhasibu, mtalaam wa mazingira, mtalaam wa usafirishaji, nk unashauriwa kuandika vitabu vitabu vitabu mpaka ufikie ukomo wa utajiri unaoutaka.

### **30. Mradi wa Maduka Makubwa (Supermarkets)**

Maduka makubwa au maarufu kama “Supermarket” ni maduka ambayo yanauza sana mijini. Maduka hayo hupendwa sana na watu wenyе kipato cha kati na kikubwa au kwa ufupi wenyе kipato kikubwa katika jamii. Waweza kufungua “supermarket” yako hasa maeneo ya mijini hata nje ya mji ilimradi eneo hilo unaona lina watu wenyе kipato kikubwa. Kumbuka watu wenyе kipato kikubwa hawapendi kwenda kwenye maduka ya uchochoroni au maduka yasiyokuwa na ustaraku au yasiyokuwa ya hadhi yao kimapato. Hivyo, wengi wao hupenda kwenda kwenye maduka makubwa ambapo watanunua kila kitu kwa pamoja na kuondoka. Siyo kwamba wanajivuna bali ni mfumo wa maisha yao. Kumbuka wengi wao wanakosa muda wa kuzunguka madukani au kwenye masoko ya kawaida kutokana na kazi zao nyingi. Matajiri wengi hawana muda wa kuzunguka huku na kule

kutafuta bidhaa wanazohitaji kama wafanyavyo watu wa kawaida. Hali kama hii huwafanya wapende kwenda kwenye maduka makubwa kama “supermarkets” ambapo wanajua watapata kila bidhaa wanayoihitaji. Wanajua watapata bidhaa zote ndani ya jengo moja na ndani ya kapu moja tofauti na kama wangeenda kwenye masoko au maduka ya kawaida. Kwa mfano kwenye “supermarket” mtu anaweza kupata bidhaa kama sukari, majani ya chai, kahawa, dawa ya mbu, mayai, mikate, mchele, nyama, samaki, vitafunwa vya chai asubuhi, nk. Vitu vyote anavyovihitaji anavipata ndani ya duka moja kwa muda wa dakika chache tu na akaondoka hadi nyumbani bila kupoteza muda wake kwa kuzunguka maduka mengi.

Kutokana na hali hii, ndipo maduka makubwa kama “supermarkets” yanafanya biashara kubwa. Sababu nydingine ni kwamba “supermarkets” nydingi huwa wazi saa nydingi za kazi, wakati mwengine huwa wazi kwa saa 24 kwa siku na siku 7 za wiki. Hii ndiyo sababu kubwa maduka hayo hupendwa zaidi na watu wenye kipato kikubwa kwani huwasaidia kuokoa muda wao. Mtu anajua kwamba hata kama atatoka kazini kwake muda wa saa 4 usiku atakuta duka liko wazi na atanunua bidhaa muhimu kwa mahitaji yake ya siku hiyo au nyumbani kwake. Yeye anajua kwamba akiegesha gari lake mbele ya “supermarket” atanunua kila kitu hapo hapo na atawasha gari lake na kuondoka bila kuwa na mashaka ya usalama wa gari lake wala mali zake.

Ukianzisha “supermarket” yako na ukaiwekea bidhaa zote muhimu kwa matumizi ya wanamtaa wako au watu wa mijini kwako, uwe na uhakika wa kuufuta umaskini wako wote. Ukipenda kufanya biashara hii, hakikisha unawasiliana na wengine wanaofanya biashara kama hiyo upate habari zake kwa usahihi, changamoto zake na jinsi ya kuvuka changamoto hizo ili uweze kutajirika. Kama umejipanga vyema kwenye duka lako, uhakika wa kuwa na mauzo zaidi ya Tshs 500,000 hadi 1,000,000 kwa siku utakuwa nao ambapo hautakosa faida zaidi ya Tshs 250,000 kwa siku.

### **31. Mradi wa Daladala za Abiria (Hiace, Coaster Bus)**

Huu ni mradi wa kusafirisha abiria mijini, maarufu kama daladala. Watu wengi hasa wale wanaolipwa viinua mgongo kwenye mifuko ya pensheni

wanapolipwa mafao yao hukimbilia sana miradi hii. Hata hivyo wengi huikimbilia bila kuwa na utafiti, ujuzi wala uzoefu. Tatizo hilo huwafanya wengi kuishia kupata hasara ya mafao yao na wanalazimika kurudi kwenye umasikini wa kutupwa. Ukitaka kuufanya mradia huu wa magari ya abiria mijini ni vyema kwanza kutafuta uzoefu kwa wanaofanya biashara hiyo. Uliza mambo mengi kwao kama wazoefu wakueleze ni wapi pa kupitia na ni wapi hapafai upite. Hii itakusaidia kuepuka kupata hasara. Wazoefu watakwambia mbinu za ushindi nawe utashinda. Usikurupuke kufanya mradia wowote bila kufanya uchunguzi wako binafsi. Na hii ni kanuni kuu kwa miradi yote inayoeleza ndani ya kitabu hiki.

Mradi wa magari ya abiria unaweza kukutajirishaa endapo utakuwa na magari yasiyopungua mawili yanayotembea. Ukitaka kufanya vyema zaidi itafaa ukinunua magari ambayo hayajachakaa sana. Kwa mfano kama ukinunua Hiace iliyokwishatembea umbali wa kilomita 60,000 hadi 100,000 utakuwa angalau umepata HIACE yenye uwezo wa kukuhudumia kwa muda mrefu usiopungua miaka miwili bila kupata shida ya matengenezo makubwa. Ukipata Hiace iliyokwishatumia chini ya kilomita hizo kwa mfano Km 3000 hadi 10,000 tu itakuwa bado ni HIACE yenye uwezo wa kukuhudumia kwa angalau miaka 3 hivi bila shida kubwa ya matengenezo. Hata hivyo, itategemeana na mji au route ya njia yako itakayokuwa inafanya kazi.

Kwa ufupi ni kwamba mradia wa Hiace zipatazo 4 kwa siku zote zikiwa zinatembea vyema na zinafanyiwa huduma zote za kiufundi (Engine services) unaweza kukupatia Tshs 240,000 kwa siku. Kama kila siku hakuna matatizo kwenye magari yako yote utapata Tshs 240,000 kwa siku utakuwa na uhakika wa kupata Tshs 7,200,000 kwa mwezi sawa na Tshs 86,400,000 kwa mwaka. Fedha kama hizo ukizipata na kuzifanya mipango mingine ya maendeleo, unaweza ukafanya miradi mingine zaidi kutokana na Hiace peke yake. Jitahidi kufanya mradia huu kwa malengo ya kuanzisha miradi mingine ya kudumu zaidi kama vile majengo ya biashara, mahotelii, mashule, mashamba, nk. Aidha, hakikisha kuwa gari lako likiisha rudisha gharama zote za ununuzi wake pamoja na faida uliuze ununue jingine angalau kila baada ya miaka 3 au 4 ili kuepuka kupata hasara zitokanazo na matengenezo ya gari hasa linapokuwa limeanza kuchakaa.

## **32. Kuanzisha Mradi wa Kanisa**

Pamoja na kwamba kitabu hiki siyo cha dini ya Kikristo, wala hakiwalengi wakristo peke yake; naomba nikiri na kuwa wazi kwamba hoja hii ni ngumu. Ni ngumu kwa sababu inahusu maswala ya Imani. Maswala ya imani na pesa huwa magumu sana. Huwa ngumu sana kwa sababu itatafsiriwa kwamba kuanzisha kanisa siyo kutafuta pesa. Hapa ndipo penye utata lakini penye utamu kwa wale wanaoanzisha makanisa. Ni kweli kwamba mradi wa kuanzisha kanisa unapaswa kuanzishwa kwa umakini. Ni kweli kwamba ukitaka kuanzisha kanisa ni lazima uwe na tahadhari kwamba kama huna msukumo wa kusaidia jamii kwa mambo ya imani kanisa unaloanzisha halitakuwa na tija kwa jamii. Hoja yangu hapa ni kwamba msukumo unapaswa usiwe kupata pesa. Msukumo unapaswa uwe ni kuwatoa watu kwenye matatizo walionayo kiimani, kiafya, kiuchumi na kifedha. Nashauri sana kwamba msukumo wa kuanzisha kanisa uwe wa kuwaelekeza njia ya uzima wa milele. Aidha, naomba kusisitiza kwamba kipengere hiki kinawahuusu wakristo tu. Kwa hiyo, mradi huu unawapasa wale wenyе wito na kazi ya Mungu hasa walioko katika imani ya Kikristo. Kama wewe siyo mkristo na hauna wito mkubwa moyoni mwako wa kueneza neno la Mungu nakushauri usijiingize kwenye mradi huu. Kama kisaikolojia, kielimu na kiuchumi unadhani huwezi kuanzisha kanisa na kukabiliana na changamoto za kuanzisha kanisa, mradi huu haukufai.

Katika sehemu hii, nazungumza na watu wenyе wito wa kueneza neno la Mungu na walio katika imani hiyo ya Kikristo. Kama wewe huna imani hiyo, kipengere hiki hakikufai kuendelea kukisoma. Kuanzisha kanisa kunakosemwa katika kitabu hiki ni kule kunakotokana na nia ya kuwaleta watu kwenye imani ya Kikristo tu. Mantiki hapa ni kwamba kuwaleta watu kwa kristo ni moja ya kazi kubwa. Kazi kubwa kama hii mtu anapoifanya ajue anafanya mradi mkubwa sana hapa duniani. Tunapaswa kujua kuwa kueneza Neno la Mungu ni mradi mkubwa sana unaogharimu pesa nyingi. Ni mradi muhimu kwa ustawi wa wananchi kwani wananchi huacha njia mbaya na kugeukia maadili yanayotakiwa katika jamii. Kuanzisha kanisa kunapaswa kufanya kwa umakini mkubwa pamoja na ari ya hali ya juu vinginevyo mradi utashindikana na hakuna matokeo makubwa yatapatikana.

Unapotaka kuanzisha kanisa ujue huo ni mradi wako wa maisha yako yote. Unatakiwa uwe umeiva kimaandiko na kiuelewa wa maswala ya kawaida ya maisha hasa elimu ya dunia. Aidha, mini nashauri wanaotaka kuanzisha mradi wa kanisa kama elimu yao ya juu ni darasa la saba, ingekuwa vyema wakajiendeleze zaidi mpaka angalau wahitimu kidato cha nne. Hivyo, nashauri mradi wa kanisa uanzishwe na mtu mwenye elimu ya kidato cha nne na kuendelea. Ukianzisha kanisa bila elimu ya kutosha itakuwa vigumu kwenda na mabadiliko ya wakati na teknolojia inayokua kwa kasi. Hata kama kanisa unalianzisha vijijiini, wanakijiji hao wanapenda wachungaji au viongozi wa makanisa wenye uelewa mpana wa mambo ya kawaida. Utakuwa msaada zaidi kwa watu wako. Watakupenda zaidi na kuleta watu wengi zaidi kanisani kwako kwa kuwa una elimu ya kutosha na maandiko unayajua sana. Hakuna jambo duniani litatokea ukawa huna uwezo wa kulifafanua kwa muumini wako endapo litaulizwa na muumini wako. Ukiwa na elimu itakusaidia kujibu maswali karibu yote utakayoulizwa na wapendwa kanisani.

Ukianzisha kanisa kwa lengo jema la kupeleka watu kwa Mungu wa kweli ndipo na wewe utapata pesa zaidi kama ruzuku kutoka kwa Mungu. Hakikisha unaanzisha kanisa kwa lengo jema ili zawadi yako wewe ije ikiwa ni pesa au vitu toka kwa watu wa Mungu. Kuleta watu waovu kwa Mungu ni mradi mkubwa ambao kwa hakika ukiufanya watu wa Mungu nao wataleta pesa kwako. Ukianzisha kazi ya Mungu kwa nia njema na lengo jema na si vinginevyo, mradi huo utakupa mapato makubwa. Usianzishe kanisa kwa lengo la kuwapata wake za watu au binti za watu. Usianzishe kanisa kwa nia ya kufanya ngono na waumini wako. Ukianzisha kanisa kwa nia hiyo, ujue hautafika mbali, utakataliwa na watu na ndio utakuwa mwisho wa kazi yako.

Lengo lako kuu na wito wako mkuu uwe kuwafundisha watu wako neno la wokovu watu wako. Fundisha kwa ufasaha, fundisha bila kubabaisha, elekeza watu njia njema na bora za maisha ya kawaida na hata ya kiroho nao watakupenda. Waumini wakikupenda hakika watachangia mradi wa maendeleo ya kanisa na kukuletea siyo pesa tu hata vitu pia. Watakuletea; chakula, mifugo, nguo, pesa, gari, na hata nyumba. Fanya kazi ya Mungu

ukiwa hulengi kupata vitu bali kupata watu wema na wamchao Mungu. Ukweli ni kwamba kazi ya Mungu inatajirisha endapo utaifanya kwa uvumilivu tena wa hali ya juu, ukiwekeza kwenye mafundisho sahihi na ya ukweli kwa muda wa kutosha baada ya muda kama wa miaka 3 hadi 5 ndipo utakapoanza kuona Mungu akikuletea matunda mema kutoka kwa watu wako hata wasiokuwa waumini wako. Kama utafanya kazi njema Mungu akakupa watu wazima wasiopungua 150 wenye uwezo wa kutoa sadaka Tshs 1000 kwa kila Jumapili au siku yoyote unayopanga muwe mnasali, ujue utakusanya Tshs 150,000 kila mkusanyikapo wa Ibada kuu ya kila wiki.

Endapo utapenda kuanzisha mradi wa kanisa na ungependa kujifunza zaidi usimamizi bora wa makanisa nakushauri ujiunge na vyuo vya elimu ya Biblia kabla hujaanzisha kanisa. Chuoni utajifunza mengi zaidi yahusuyo uongozi wa kanisa, saikolojia ya waumini, saikolojia ya watoto, historia ya Ukristo duniani, usimamizi wa pesa za kanisa, nk. Katika dunia hii tunao wahubiri mamilionea walijatirika siyo kwa sababu walianzisha makanisa ili wawe mamilionea, bali msukumo wao mkubwa haukuwa kutafuta pesa bali watu. Na kwa kufanya hivyo watu walikuja na pesa zao wakawapa wahubiri hao na kwa sasa wamekuwa mamilionea na mabilionea. Wapo ambao wameweza kumiiliki vituo vya redio, televisheni na magazeti makubwa. Wapo wanaomiliki ndege zao binafsi. Wapo wanaomiliki mashamba makubwa na makampuni makubwa kabisa. Vyote hivyo vikiwa vimetokana na kazi ya kutangaza ufalme wa Mungu na Mungu naye akawapatia utajiri wa kuwafanya wazidi kueneza ujumbe wake kwa dunia.

Kwa Tanzania tunao wahubiri waliokwishatajirika na kuwa mamilionea au mabilionea kutokana na kazi ya kueneza Neno la Mungu na Injili ya wokovu. Tunao watumishi wa Mungu wengi Tanzania kama akina Anthony Lusekelo, Zakaria Kakobe, Dr. Getrude Lwakatare, BG Malisa, Onesmo Ndegi, Josephat Mwingira, Sylvester Gamanya, na wengineo wengi. Hawa watumishi wa Mungu wamefanya mambo makubwa sana ya injili na ukienda makanisani mwao utagundua kwamba Mungu alishawapa watu wengi sana. Na ijulikane kwa nia njema kabisa kwamba Mungu anapokupa watu wengi maana yake amekupa na pesa nydingi sana. Ifahamike

kwamba watumishi wa Mungu hao niliowataja ni mifano tu na wala sina nia ya kufuatilia utajiri wao kama wameupata kwa njia sahihi au la, mimi ninachokielewa ni kwamba kazi yao ni kueneza Injili na neno la Mungu. Nami natumia mifano yao kuhamasisha watu wenye wito wa kazi hiyo wasonge mbele na Mungu atawasaidia haja za miili na mioyo yao.

Kwa mfano Mungu akikupa watu wapatao 2000 wenye uwezo wa kiuchumi kutoa sadaka kwenye ibada kila mmoja Tshs 2000 kila ibada ya wiki, maana yake ni kwamba kwa wiki hiyo Mungu atakuwa anakupa ruzuku ipatayo Tshs 4,000,000 kwa wiki moja. Huu ni mfano tu tena mdogo ambao ninautoa kwako ili kukupa picha ndogo tu kuhusu ninalolisema hapa. Kumbuka kwamba watumishi wa Mungu niliokutajia awali kwa sasa walikwisha kuwa matajiri wakubwa wa watu kwanza kisha wakawa matajiri wa pesa. Makanisani mwao unakuta anazungumzia kufanya mambo au matukio yenye thamani ya mamilioni ya pesa. Wanamiliki magari, majumba, miradi mikubwa ya Televisheni, redio, magazeti, nk. Ukweli ni kwamba Mungu akikupa watu atakupa na pesa pia. Wewe kama unao wito, usiogope, anza kazi sasa.

Napenda kuhitimisha kipengere hiki kwa kutahadharisha kwamba imani ya Kikristo imeingiliwa na watu wasio na nia njema ya kuwatoa watu kwenye maasi na kuwapeleka kwa Mungu. Hivyo, ijlukane kwamba siyo kila mtu anayeanzisha kanisa atakuwa na nia njema. Hata hivyo, kuwajua wenye nia njema ni vigumu sana.

### **33. Mradi wa Nyimbo za Injili**

Kwa kuwa watanzania wanapenda sana nyimbo za dini siku hizi, mradi wa albamu ya nyimbo za Injili unaweza ukakuweka kwenye utajiri mkubwa sana. Hakikisha unapofanya biashara hii, usiweke mbele fedha kwanza kama msukumo wako. Kinachokusukuma kisiwe fedha, bali kueneza ujumbe wa Mungu kwa watu. Sukumwa kufanya vyema zaidi katika soko la nyimbo za Injili. Kwa kufuata kanuni hiyo na fedha zitakufuata.

Hapa Tanzania kwa sasa hakuna mtu asiyemjua Rose Mhando au Bony Mwaitege. Hawa na wengine wengi ni waimbaji maarufu Tanzania kwa nyimbo za injili. Walianza kwa kuimba kama huduma kwa jamii, hawakuanza

wakiwa wanalenga kupata fedha, lakini kwa kufanya hivyo, Mungu aliwapa fedha. Kwa mfano kama utafanikiwa kutoa nakala za albamu yako zipatazo laki mbili tu (nakala 200,000) za albam na kwenye kila albam ukapata Tshs 1000 tu, ni dhahiri kwamba utapaswa kupata Tshs 200,000,000 kwa toleo moja tu la albam.

Mambo ya kufanya ili ufanikiwe katika mradi huu hakikisha kwamba unaifuata hatua zifuatazo ili kufikia hatua ya kuweza kuuza hadi nakala laki mbili: kwanza, uwe mcha Mungu wa kweli, pili, uwe na ufahamu mpana sana kuhusu Imani ya Kikristo, maandiko yake na maadili yake; tatu, uwe na kanisa maalum unalosali na kulelewa kiimani; nne, uwe na bidii ya kusikiliza nyimbo za watu wengine waliokutangulia; tano, hakikisha unatafuta ushauri kwa waliokutangulia ikiwemo wachungaji wako; sita, fanya maombi kila siku kwa Mungu ikiwemo hata kufunga na kuomba kila inapowezekana yaani mwombe Mungu akupe nyota ya kupendwa, kukubalika, kuuzika, na kusikika; saba, hakikisha kwamba unafanya zoezi la kuimba kila mara bila kujihurumia, ikiwezekana nenda ukajichimbie mahali pa peke yako na waimbaji wako muimbe sana ili Kuweka sawa maswala yote ya sauti kabla ya kwenda kurekodi nyimbo zako; nane, fanya utafiti zaidi kuhusu studio nzuri, msambazaji wa albamu zako, peleleza taratibu za kisheria, na mengineyo yote muhimu yahusuyo kazi ya uimbaji na uuzaaji wa albamu za nyimbo za injili.

### **34. Mradi wa Filamu za Maigizo**

Watu wengi Tanzania watakuwa bado wanamkumbuka kijana aitwaye Steven Kanumba. Kijana huyu alikuwa ndiyo nembo ya filamu za Tanzania hadi alipotwaliwa na mauti Mwaka 2012. Wale wanaomkumbuka watakubaliana nami kwamba alikuwa kijana aliyejewa ameanza kuyaona mafanikio ya kifedha kupitia filamu alizokuwa amecheza au kutunga na kushiriki. Kama wewe unahisi kuwa na kipaji cha kuigiza maigizo na ukatoa filamu, nakushauri utafute waigizaji waliokwishafikia hatua fulani uwaone na uongee nao. Utakuwa tajiri mwenye kipato cha juu endapo utadhamiria. Usiogope wala kuwaza utanzie wapi, wewe kama hujui uanzie wapi waulize hata wasambazaji wa DVD za filamu hao watakuelekeza jinsi ya kufika hapo.

Kama unaweza kutunga hadithi nzuri yenyе mvuto na iwe ya kweli au isiyokuwa ya ukweli lakini yenyе kueleza maisha ya ukweli, wewe jitose na uanze kazi ya maagizo. Ukweli ni kwamba inalipa vizuri sana. Hebu tazama kwa mfano mmoja tu; kama filamu yako ikiwa yenyе kupendwa sana kote nchini na nje ya nchi ukafanikiwa kuuza nakala za DVD au CD zipatazo milioni moja (1,000,000) kwa bei ya Tshs 1000 tu kuna uwezekano wa kupata zaidi ya shilingi bilioni moja (Tshs 1,000,000,000). Kama unacho kipaji changamka sasa hivi, fanya kila unaloweza uweze kupiga hatua. Hata kama itakuchukua miaka mitatu au zaidi kufikia lengo lako, wala usikate tamaa. Songa mbele mpaka jambo lieleweke.

### **35. Mradi wa Muziki wa Bongofleva**

Kama ilivyoelezwa kwenye kipengere cha nyimbo za injili na kwenye filamu, hali kadhalika muziki wa nyimbo kizazi kipyä maarufu kama Bongofleva nao unalipa sana kwa wale wanaoufanya kwa bidii na kwa weledi unaotakiwa. Kama unacho kipaji cha kuimba na unahisi moyo wako wachemka kuelekea uimbaji wa nyimbo za bongofleva, unashauriwa ujitalidi kuwaona wale waliokwishakutangulia kwenye soko la muziki. Tafuta maelezo yao wakueleze njia ya kuingia kwenye uwanja huo. Hakika hautabaki maskini. Bila shaka utakuwa unawafahamu wanamziki wengi Tanzania ambao hapo awali walikuwa mafukara kabisa wao na familia zao, lakini kwa sasa maisha yao yamebadilika kabisa hata kuwa mamilionea kutokana na muziki. Mfano wa wanamziki waliofanikiwa kifedha ni pamoja na Judith Wambura (Lady Jeydee), Dimond Platinumz, Banana Zoro, na wengine wengi. Pamoja na wizi mkubwa uliopo wa kazi za wasanii hao, bado wameweza kupiga hatua fulani kifedha ambapo bila shaka siyo maskini tena. Wameshakuwa mamilionea wakiwa bado vijana.

### **36. Mradi wa Kutengeneza Bustani**

Unaweza kujiajiri kwenye kutengeneza bustani za majumbani na ukawa tajiri kabisa. Waweza kujiajiri katika eneo hili kwa kuanza kutafuta tenda kwa watu wanaojenga majengo ya kisasa katika mtaa wako au katika mji wako. Unapoona mtu yuko anajenga nyumba eneo lolote unapaswa kumwendea na kumweleza mambo mazuri ya Kuweka mazingira mazuri ya nyumba

yake. Hakikisha unazo sampuli za picha za bustani unazotengeneza ili mteja aweze kuziona na kuchagua mojawapo. Ukiona sehemu inajengwa hoteli au nyumba ya wageni (Guesthouse) unapaswa kuchangamka na kumwona mhusika mkuu wa jengo hilo na umweleze uwezekano wa kumwekeea mapambo ya maua na bustani nyumbani mwake. Ukiwa na picha za mifano ulizowahi kuwafanya wengine, wateja wengi watakubaliana na bei zako. Hakikisha kwamba unakuwa na bei ya kuanzia kutegemeana na hali halisi anayotaka mteja wako.

### **37. Mradi wa Kufuma Vitambaa**

Wanawake wengi huupenda sana mradi wa ufumaji wa vitambaa. Nikiwa mjini Kigoma siku moja niliwahi kuongea na mtu mmoja anayefuma mapambo kwenye vitambaa na mashuka akanambia kwamba, shuka moja akilifuma huliiza kwa Tshs 35,000 hadi Tshs 45,000. Mama mwingine wa jijini Mwanza niliyewahi kumtembelea kwenye kituo chake cha kufuma vitambaa vya mapambo ya majumbani alinieleza kuwa ana wateja wengi sana hadi wengine anawakimbia. Hii maana yake ni kwamba vitambaa na mashuka yaliyofumwa hupendwa sana na inaonesha kwamba vina soko sana.

Tatizo kubwa lililopo Tanzania mradi huu ni kwamba, wajasiliamali wengi hawana lengo la wapi wanataka kufika. Kwa mfano kama ukiamua kuwa na cherehani za kufuma na kudarizi zipatazo tano tu na ukaajiri watu wanne na wewe ukiwa wa watano na ukachukua chumba cha kutosha kuendesha mradi wako, kila siku mkafuma vitambaa au mashuka yasiyopungua jozi 10 na kila jozi ukaiiza kwa bei ya Tshs 35,000 utakuwa na uwezo wa kukusanya mapato yasiyopungua wastani wa Tshs 350,000 kwa siku. Unaweza kupata zaidi ya Tshs 10,500,000 kwa mwezi, ndiyoooooooo, huu ni ukweli unaowezekana kabisa. Kwa Mwaka unaweza kuingiza pesa nyingi sana hatu zaidi ya Tshs 126,000,000. Naam waweza kuwa milionea mfuma vitambaa kwa Mwaka mmoja tu.

### **38. Mradi wa Kusherehesha Matukio (MC)**

Kwa wale ambao wamewahi kuhudhuria matukio mengi kama sherehe za harusi, kipaimara, send-off, kitchen party, misiba yenyewe watu wengi,

mikutano mikubwa ya kisiasa, mikutano mikubwa ya injili, semina kubwa, makongamano, nk watakubaliana nami kwamba kusimamia matukio kama hayo kunahitaji mtu mwenye uelewa mkubwa sana wa uongozi na uendeshaji wa mambo ya sherehe. Waendeshaji wa sherehe na tafrija huitwa kwa majina mengi lakini linalojulikana sana ni “Master of Ceremony” au kwa kifupisho ni “MC”. Wengine humwita “Mssema Chochote”, wengine humwita “Mshereheshaji”. Kama unajisikia kuwa wewe unacho kipaji cha kuendesha au kusheheresha mikutano na matukio kama hayo ya harusi, nk unashauriwa kuwatafuta wengine wanaofanya kazi hizo ili upate uzoefu kwao. Anza kutafuta kazi hiyo kwa watu wenaofanya maandalizi ya shughuli hizo. Jieleze kwao kwa ufasha. Tafuta vitendea kazi kama vile suti zeny mvuto, mashati yenze mvuto zaidi, nguo za kipekee, vyombo vya kutumia kwenye sherehe kama vile vipaza sauti, nk. Kwa ufupi waliopo kwenye soko hilo ukiwapata watakupa mwongozo mzuri ikiwemo bei ya kuwatoza wateja wako kwa kila sherehe.

### **39. Mradi wa Kuongoza Watalii**

Kwa wale wanaoishi miji ya kitalii kama vile Arusha, Manyara, Mugumu, Ngorongoro, Mikumi, Mwanza, Kigoma na Tanga watakubaliana na habari kwamba uongozaji wa watalii unalipa. Wanaopata mapato mazuri ni wale ambao humiliki magari ya kuongozea watalii kwenda mbuga za wanyama na kurudi mijini. Ukiwa na magari ya kuongozea watalii ndipo utafanikiwa zaidi. Ukipenda ufanye mradi huu, ni vyema kuwaona wazoefu, au kufanya utafiti kabla hujaanza mradi wenyewe. Unaweza kujipatia zaidi ya Tshs 200,000 kila siku kwa kuongoza watalii. Unaweza kujipatia zaidi ya Tshs 6,000,000 kwa mwezi kwa kutembeza watalii peke yake. Ni vyema kusajili kampuni yako kwa ajili ya kazi hii ili kuifanya kwa ufanisi zaidi.

### **40. Mradi wa Kufundisha Matumizi ya Kompyuta**

Vijana wanaomaliza masomo ya teknolojia kama vile ICT na “Computer Science” ni wakati mzuri wa kujiajiri kwenye sekta hii. Vijana wanaweza kujiajiri kwa kuanzisha vituo vya mawasiliano ya mitandao, vituo vya kufundishia kompyuta, na huduma nyininge nyinyi zitokanazo na matumizi ya kompyuta. Kwa mfano kama vijana wawili wakijipanga wakaanzisha kituo

cha mafunzo ya kompyuta, wakafungua darasa lenye kompyuta zipatazo 30 tu na wakawa wanaendesha darasa hilo kwa ada ya Tshs 20,000 kwa kila programme, wataweza kujipatia kipato kikubwa kabisa kwa mwezi. Mradi kama huu hautaji mapesa mengi saaana bali ni uamuzi tu. Waweza kuanza na mtaji wa pesa ambazo hazizidi Tshs 5,000,000 tu kama mtaji. Mtaji kama huo ukiuandikia mpango mkakati (Business Plan), ukapeleka andiko lako hilo kwa wanaotoa mikopo kama SACCOS au Benki, unaweza kupatiwa bila wasiwasi.

#### **41. Mradi wa Kuuza Vifaa vya Shule**

Mahitaji ya elimu ni swala la kila mzazi au mlezi anayejua umuhimu wa elimu kwa watoto wake. Kwa sasa wazazi wengi wamekuwa na bidii ya kuwasomesha watoto wao siyo tu katika shule za umma bali hata katika shule za watu na mashirika binafsi. Kutokana na hali hiyo, vifaa vya shule kama vile madaftari, kalamu, kalatasi, sare za shule, viatu, mabegi ya shule, masweta, socks, chaki, vitabu, wino, nk vyote hivyo vinahitajika sana. Kwa mtu anayeanzisha mradi wa vifaa vya shule hakika hawezi kubakia masikini kamwe.

#### **42. Mradi wa kuuza Chipsi**

Kila kona utakayokwenda Tanzania utakutana na watu wanaokaanga viazi mviringo maarufu kama chipsi. Viazi hivyo vimejipatia umaarufu sana nchini kote Tanzania na ndivyo vinavyoongoza kwa kuliwa sana siku hizi vikifuatiwa na ugali na wali kwa makabila mengi ya Tanzania. Katika miji mikubwa kama Dar es salaam, Mwanza, Arusha, Tanga, Mbeya, Morogoro, Dodoma na Iringa viazi hivyo huliwa sana kwenye maeneo yote yenye mikusanyiko ya watu kama vile; baa, sokoni, stendi za magari, nk. Vijana wengi mashulen i hupendelea kula chipsi mayai. Kila kona utakayokwenda kupumzika ukiwa na watoto wako utaona kwamba watoto wako watapendelea kula chipsi zaidi kuliko kula ugali au wali. Hali hiyo ipo pia kwa wanawake wengi. Wengi wao hupendelea kula chipsi kuku au chipsi mayai.

Kwa sababu viazi hivyo (Chipsi) hupendwa sana Tanzania, ni fursa ya pekee ambayo ukiamua kuitumia kwa kuufanya mradi huu kwa juhud, kwa

kuajiri wasaidizi kadri uwezavyo inalipa sana sana. Unaweza kuwa milionea muuza chipsi. Kama uko mahali penye makutano makubwa ya watu kama vile kwenye stendi za mabasi, au sehemu yoyote yenye mikusanyiko ya watu wengi, usishangae kwa siku ukiuza chipsi zaidi ya gunia moja la viazi. Usishangae kama utakusanya zaidi ya Tshs 300,000 kwa siku. Usishangae kama kwa mwezi utapata zaidi ya Tshs 9,000,000. Usije ukastaaajabu kama ndani ya Mwaka mmoja tu utajikuta umekusanya zaidi ya Tshs 108,000,000 (milioni mia moja na nane). Watu wasikushangae kabisaa kama utanunua gari la kifahari lenye zaidi ya Tshs 20,000,000 kwa mradi wa chipsi tena ndani ya Mwaka mmoja. Wala usije ukaduwaa moyo wako ukiitwa milionea muuza chipsi mwenye nyumba nzuri na ya kifahari mitaa ya watu wanene mjini. Fanya utafiti zaidi uone kama ninachokieleza hapa ni uongo. Kutajirika na kuwa milionea muuza chipsi hakika inawezekana kabisa!!!!!!

#### **43. Mradi wa Nguo za Watoto**

Watoto ni fahari ya wazazi. Watoto wakivaa nguo nzuri wazazi hujisikia raha sana. Wazazi wanaowajali watoto wao huwanunulia nguo nzuri. Katika nyakati za hivi karibuni, wazazi wengi wamekuwa wakijisikia vyema kuwanunulia watoto nguo nzuri siyo tuu wakati wa sikukuu za kidini bali hata siku za kawaida. Kwa mjasiliamali hapa pana fursa ya kupata pesa. Ukiwekeza kwenye nguo za watoto ziwe za mitumba au za kutoka viwandani bado utapata kipato kutoka kwa wazazi wenye watoto na hakika hautabakia masikini kamwe.

#### **44. Mradi wa vifaa vya Uselemara**

Vijana wanaomaliza vyuo vya ufundi Tanzania maarufu kama vyuo vya VETA, wanaweza kujajiri kwa kuanzisha mradi wa kutengeneza samani za majumbani na kuziwa zikiwa tayari (ready made furnitures). Kwa mfano Vijana Wakihitimu fani ya uselemara wanaweza wakawa wanatengeneza stuli za kukalia au viti vya kukaa wakati wa chakula. Mkiamua kutengeneza stuli pekee yake na Mkawa Mnauza kila stuli kwa Tshs 15,000 kutegemeana na mahali ulipo, na ubora wake; kama kwa siku mwaweza kutengeneza stuli Zipatazo nane (8), utagundua kwamba kwa siku mwaweza kupata siyo chini ya Tshs 120,000 kwa wastani. Kama umejjipanga vyema kimkakati hakika waweza kupata zaidi ya Tshs 3,600,000 kila mwezi.

## **45. Mradi wa kuuza vifaa vya umeme**

Vifaa vya umeme vitaendelea kuwa na soko kubwa kwani wahitaji wa umeme wa gridi ya taifa na ule wa nguvu ya jua maarufu kama umeme wa sola wataendelea kuongezeka kote nchini. Ukiamua kufanya miradi ya kuuza vifaa vya umeme iwe miji mikubwa au midogo inayochipukia hakika hautabakia masikini. Hakikisha kuwa unafanya utafiti au upeletelezi wa kutosha kuhusu mradi huu kabla ya kuanza ili ujiridhishe faida utakayoipata.

## **46. Mradi wa vifaa vya majumbani**

Nyumba nyingi kote nchini zinahitaji vyombo vya matumizi ya nyumbani. Vyombo vya majumbani kama sahani, vikombe, sufuria, chupa za chai, visu, vyungu,nk vitaendelea kuhitajika sana majumbani mwa watu wengi. Kufanya mradi wa uuzaji wa vifaa vya majumbani hakika utainuka kiuchumi na kifedha.

## **47. Mradi wa mabasi ya Abiria**

Mradi huu wa mabasi ya abiria yaendayo kutoka mji mmoja kwenda mji mwingine hapa nchini ni mradi ambao kwa hakika unawaacha wamiliki wa mabasi hayo wakiwa matajiri wakubwa. Kwa basi lenye ukubwa wa kubeba abiria wapataao 60 lenye kufanya safari zake kwa mfano; kutoka Mwanza kwenda Dar es Salaam kwa kutoza nauli ya Tshs 40,000 kwa kila abiria, basi hilo likifika salama liendako mmiliki wa basi hilo atakukusanya kiasi cha Tshs 2,400,000 kwa safari moja ya kwenda tu, endapo litakwenda likiwa limejaza abiria. Kama ukitoa matumizi ya mafuta ya gari, posho ya dreva, kondakta, mawakala na malipo ya ushuru, nk ukafanya iwe Tshs 1,000,000 utakuta mmiliki anabaki na kiasi kipatacho Tshs 1,400,000 kwa safari moja. Tuchukue mfano mwingine wa mwekezaji mwenye mabasi manne yafanyayo safari zake kutoka Kigoma mjini kwenda Jijini Mwanza ambapo nauli ni Tshs 31,000 kwa kila abiria. Kwa mfano kama mtu akiwa anamiliki mabasi manne kila siku yaende barabarani mawili yaende Mwanza na mengine mawili yatoke Mwanza kwenda Mjini Kigoma (kwa mfano) na ikiwa mabasi haya yataenda yakiwa yamejaa abiria 60 kila moja

toka mwanzo wa safari mpaka mwisho, mwekezaji huyo atakusanya pesa zipatazo 7,440,000 kwa siku moja tu. Hata kama tukijaribu kutoa makisio ya matumizi ya lazima kama vile kodi, ushuru, mafuta ya dizeli, matengenezo, malipo ya mawakala, posho ya madreva na makondakta, n.k ikawa kiasi cha Tshs 2,440,000 utaona kwamba mwekezaji atabakiwa na Tshs 5,000,000 kwa mabasi hayo manne ya abiria kila siku yanapokwenda safari zake. Kama kwa mwezi yatafanya safari zipatazo 15 tu maana yake ni kusema kwamba mwekezaji huyo kwa safari hizo 15 za mabasi yake atapata kiasi cha Tshs 75,000,000 kwa mwezi mmoja. Na kwa mwaka mmoja atakuwa ameweza kujipatia fedha zisizopungua Tshs 900,000,000. Huu ndio ukweli wa mambo. Wamiliki wa mabasi ni kundi moja la wawekezaji wenye pesa nyingi sana. Ni mabilionea.

Hata kama mtu anamiliki basi moja tu lenye kufanya safari zake kati ya Mwanza na Bukoba, au Kigoma na Mwanza, au Dar es salaam na Arusha, au Dar es Salaam na Mbeya, nk mtu huyo anaweza kuwa tajiri mkubwa sana kama atafuata kanuni zote za usalama wa gari na abiria. Kwa mfano kama unalo basi moja linalosafirisha abiria kutoka Kigoma mpaka Mwanza kwa nauli ya Tshs 31,000 maana yake ni kwamba kwa safari moja tu utakusanya Tshs 1,860,000. Kama tukiamua kuamini kwamba Tshs 860,000 ndiyo matumizi ya ghamama za uendeshaji wa basi hilo, basi mwekezaji huyu atabakiwa na Tshs 1,000,000 kwa kila safari moja. Kama basi hilo litakwenda safari 15 tu na siku 15 nyingine za mwezi akalipumzisha kwa ajili ya kulifanya huduma (i.e engine services) basi mwekezaji huyu atawenza kujipatia zaidi ya Tshs 15,000,000 kwa mwezi huo. Na kama basi hilo ni imara zaidi na barabara ikiwa ya lami safi, na dreva anaendesha kwa umakini, basi hilo likafanya safari zake angalau mara 20 kwa mwezi, basi mwekezaji huyo atawenza kuvuna pesa si chini ya Tshs 20,000,000 kwa mwezi. Kwa Mwaka mmoja mwekezaji huyo mwenye basi moja tu, lenye kubeba abiria 60 na kutoza nauli ya Tshs 31,000 basi litaingiza kati ya Tshs 180,000,000 na 240,000,000 kwa Mwaka mmoja tu. Je, hapo hujawa milionea? Ukitaka kufanya mradi wa mabasi ya abiria ni vyema ukawaona pia wanaoifanya miradi hiyo ili uweze kujifunza kwao kwa undani zaidi kuhusu uendeshaji na changamoto zilizomo kwenye miradi hiyo. Kabla hujaaamua kwenda Dubai au Japani au Afrika Kusini Kununua basi lako

la UTONG au MARKOPOLO hakikisha kwanza umejitafutia taarifa za kutosha kuhusu mradi huu ili usikurupuke na ukapata hasara njani. Naam, umilionea unakusubiri.

#### **48. Mradi wa ufügaji wa samaki**

Mradi huu unalipa vizuri sana kama ukiufanya kwa kufuata maelekezo ya watalaan wa samaki. Kama wewe unalo eneo la kuweza kujenga bwawa la samaki lenye ukubwa hata wa mita za mzunguko 10 kwa 5 unaweza Kufuga samaki wengi na wakakupatia kipato kizuri sana. Samaki ukiwafuga vizuri kwa mwaka unaweza kuvuna mara mbili au mara tatu. Kwa mfano kama bwawa lako lina samaki wapatao 15,000 tu na kila samaki ukamuza kwa Tshs 4000 siku ya kuvuna utapata pesa nzuri isiyopungua Tshs 60,000,000 kwa msimu mmoja. Mpendwa, nakushauri uende idara ya mifugo na uvuvi kwenye Halmashauri iliyoko karibu yako uombe kuonana na mtalaam wa uvuvi akupe mwongozo wa kufuga samaki, hakika utakuwa milionea. Kama kuna mtu unayemjua ana fuga samaki tafadhalii ukamwone akupe uzoefu na habari kamili kuhusu changamoto na jinsi ya kuzikabili changamoto hizo. Kama umedhamiria, wala usiogope anza kazi leo hakika utakuwa bilionea kwa Kufuga samaki.

#### **49. Mradi wa duka la jumla**

Bila shaka unaishi sehemu ambako kuna maduka madogo madogo ambayo kila siku unawaona wamiliki wake wakitoka na kwenda mijini kati kununua bidhaa zinazopendwa hapo mtaani kwako. Au umewahi kusikia wafanyabiashara wakisema kwamba wameendea mzigo labda Dubai, China, Nairobi, Dar, Kampala, Mwanza, Kahama, Zanziba au kwingineko. Kama umewahi kuwasikia, ujue wanachofuata ni bidhaa zinazopendwa hapo ulipo ambapo wanazinunua kwa bei ndogo na kuja kuziwa kwa bei kubwa hapo ulipo. Hawa ni wafanyabiashara wanaoitwa matajiri na wanahehimika mtaani kutokana na safari zao za mara kwa mara hasa za nje ya nchi kama Dubai au China.

Wewe pia waweza kuifanya biashara kama hiyo. Siyo lazima uende China au Dubai, lakini waweza kuwa unanua bidhaa kutoka maduka makubwa

ya mjini na ukawa unauza kwa bei ya jumla hapo kijijini kwako au mtaani kwako. Fungua duka la jumla tu na uuze bidhaa zako kwa bei ya jumla tu. Kwa mfano kama ni huisi, maji, sukari, chumvi, sabuni, mafuta ya taa, mchele, unga, maharage, nk vyote hivyo nunua na uuze kwa bei ya jumla hapo mtaani kwako au kijijini kwako. Utakuwa milionea kwa muda mfupi. Hakika ukifanya hivyo utakuwa milionea hapo mtaani mpaka wewe mwenyewe utashangaa. Naam, Siku moja utapaa kwa ndege mpaka China kwenda kuleta bidhaa zaidi. Kumbuka kwamba wanaoenda Dubai au China walizaliwa wakiwa hawana kitu kama wewe, walichokuvanacho wakati wanazaliwa hata wewe ulizaliwanacho.

## **50. Mradi wa Usafi wa Majumba/Maofisi**

Ukitaka mradi huu ukuendee vyema anza kwanza kusajili kampuni ya kutoa huduma za usafi maofisini na kwenye majengo makubwa (Cleanliness and Sanitation Enterprises). Kampuni hiyo ukishaisajili kwenye mamlaka husika kama vile BRELA, unapaswa kutafuta leseni kutoka Halmashauri husika na kisha uende mamlaka ya mapato (TRA) upatiwe namba ya mlipa kodi (TIN) na usajili wa malipo ya kodi yaani VAT. Hatua inayofuata zaidi ni kufungua ofisi ya kampuni yako, ununue vifaa vya kufanya usafi, uajiri wafanyakazi wasiopungua 10 hivi au kulingana na ukubwa wa kampuni yako na wingi wa kazi za kampuni yako.

Baada ya hatua hiyo, uhakikishe kwamba unatafuta zabuni (tender) kwa bidii kwenye majengo makubwa hasa yenye ghorofa mijini. Kazi ya kusafisha majumba au maofisi kwenye miji hakika inalipa sana. Kwa mfano ukipewa kufanya usafi kwenye jengo moja tu lenye ghorofa 10 hasa katika miji kama ya Dar es salaam, Mwanza, Arusha, Morogoro,nk utakuwa umeshamaliza umasikini wako wote kwa mwaka mmoja tu. Kampuni yako yaweza kulipwa hata zaidi ya Tshs 20,000,000 kwa mwezi kufanya usafi wa jengo hilo. Je, kampuni yako ikilipwa pesa kama hiyo wewe utabakia kuwa masikini? Hata kama gharama za uendeshaji wa kampuni zitafikia zaidi ya Tshs 8,000,000 wewe bado utabakia na pesa zisizopungua Tshs12,000,000 kwa mwezi kama Mkurugenzi wa kampuni. Hakika ukianzisha kampuni ya usafi inalipa sana. Anza kampuni yako leo na hautajuta.

## **51. Mradi wa Kuuza vinywaji baridi na Juisi**

Katika miji mikubwa kama Dar es Salaam na Mwanza ukifungua kituo chako cha kuuza vinywaji baridi na juisi za matunda kama maembe au parachichi, nanasi, n.k, hakika utapata kipato ambacho utachekelea sana kama siyo moyoni basi mdomoni. Kwa mfano kama utauza juisi ya matunda fleshi lita 40 kwa siku na kila lita unaiuza kwa Tshs 3000, kwa siku utakuwa na mauzo yasiyopungua 120,000.

Hapa tunazungumzia juisi peke yake. Ukijumlisha na maziwa mgando lita 20 kwa siku na lita moja unauza Tshs 3000, ukajumlisha na vitafunwa hapo kama chapatti au keki. Ukajumlisha vinywaji kama soda na maji baridi. Hakika wewe kijiwe hicho hautakisahau. Hima hima nakuomba usikae. Anza mkakati wa kufanya kazi hii, hautabakia maskini kamwe. Mwezi mmoja tu ukiisha wakati wengine wanalia njaa na kusema kuwa pesa ni ngumu kupatikana, wewe utakuwa unachekelea ukiwa na zaidi ya Tshs 3,000,000 kwa kila mwezi.

Hebu tazama mfano huu wa mtu anayeuzza glasi za juisi zipatazo 500 tu kwa siku kwa bei ya Tshs 500 tu. Akiiza juisi yote atapata zaidi ya Tshs 250,000 kwa siku. Kama kijiwe kimechangamka kila siku kwa mwezi atajipatia si chini ya Tshs 7,500,000. Je, kama mtu huyo anauza kwa bei ya Tshs 1000 kwa glasi moja atakusanya kiasi gani cha pesa kwa mwezi? Kumbuka mradi mmoja huanzisha mradi mwингine. Usikubali kuzeekaa kwenye mradi mmoja. Usikubali kubweteka na mradi mmoja. Hakikisha kila mradi unaouanza unazaa mradi mwингine, hivyo hivyo mpaka kufa kwako. Hii ndiyo kanuni ya utajiri. Kitabu hiki kimejaa mifano ya miradi mingi unayoweza kuifanya. Chukua hatua sasa.

## **52. Mradi wa Kununua na kuuza Ng'ombe**

Jamaa yangu mmoja alinitembelea ofisini kwangu siku moja ya mwezi Januari 2014 akawa ananisimulia kuhusu kazi hii ya Kununua na kuuza ng'ombe kwamba inalipa. Mimi awali sikumwelewa kabisa mpaka aliponifafanulia zaidi jinsi biashara yenyewe ilivyo ya uhakika na inalipa. Baada ya kufutilia sana, ndipo niligundua kweli kwamba biashara hiyo inalipa hasa siyo mchezo.

Ukiamua kuifanya kazi hii, unachofanya wewe hauwi mfugaji wa ng'ombe bali unakuwa mununuzi na muuzaji. Haukai na mzigo kwa kipindi kirefu. Unachofanya wewe ni kama nilivyoeleza kwenye mradi wa ufugaji wa kuku wa kienyeji (soma tena kipengere hicho ujikumbushe). Kwa mfano ukienda vijijini wanakofuga ng'ombe au kwenye minada ya kila wiki maeneo wanakofuga ng'ombe, utakuta kwamba ngo'ombe huuzwa kwa bei kat i ya Tshs 200,000 hadi 400,000. Kila ng'ombe akifikishwa mjini unaweza kumuuzza kat i ya Tshs 400,000 hadi 800,000. Hii ina maana ya kwamba kila ng'ombe anaweza kukupatia faida mara mbili ya bei uliyonunua.

Kama utakuwa umeanza na mtaji wa Kununua ng'ombe wapatao 20 tu kwa mzunguko wa mara tano tu kwa mwezi, utakuwa na uwezo wa kujipatia kipato kisichopungua Tshs 20,000,000 kwa mwezi huo. Hapa ina maana kwamba kwa mwezi wewe utakwenda vijijini kukusanya ngo'ombe mara tano tu. Na utanunua ngombe 20 tu kwa kila safari yako ambapo itakuwa sawa na ngo'ombe 100 tu kwa mwezi. Huu ni mfano tu mdogo amba o ninautoa kwa mtu ambaye anataka afanye biashara hii akiwa hana mtaji mkubwa. Mradi huu waweza kuuanzisha kwa mtaji wa kuanzia kima cha chini cha Tshs 5,000,000 tu.

Kama una kiasi hicho cha Tshs 5,000,000 nakushauri kabisa uanzishe mradi huu wa Kununua na kuuza ngombe mjini, hakika hautabakia masikini. Kwa mwezi utakuwa na uhakika wa kupata siyo chini ya Tshs 15,000,000 kama faida. Siyo lazima ununue na kuuza tu bali pia waweza kuamua kufuga kabisa ngombe wa biashara. Una fuga kwa muda mfupi na kuuza baada ya miezi kama mitatu. Unanunua kwa bei ndogo unauz a kwa bei kubwa baada ya miezi mitatu au mitano.

### **53. Mradi wa kuchaji simu za Mkononi Vijijini**

Vijiji vingi Tanzania vimefikiwa na minara ya simu za mkononi na hivyo kuwafanya wanavijiji wengi kuwa na simu za mkononi. Pamoja na makampuni ya simu kuweka minara ya simu katika vijiji vingi Tanzania, hali ya umeme wa gridi ya Taifa au mifumo mingine ya utoaji nishati ya umeme siyo njema kabisa. Bado vijiji vingi zaidi ya 80% havina umeme wa uhakika kabisa. Hali hii inakuwa fursa kubwa ya kujipatia fedha nyingi kwa

wajasiliamali wenyе mwamko wa kujikusanya utajiri kwa kutatua matatizo ya watu.

Kama kijiji chenu kina mtandao wa simu ni wakati mzuri na muafaka wa kwenda kuwekeza kijijini kwenu. Kuna vijiji vingine ukiamua kuwekeza katika mradi wa kuchaji simu unaweza kujipatia hadi Tshs 20,000 kwa siku. Kwa mfano vijiji vyenye wavuvi wengi, au wakulima wengi kama vile wakulima wa chai, kahawa, tumbaku au alizeti, nk vijiji hivyo vina mzunguko mkubwa sana wa fedha. Ukiwekeza katika vijiji kama hivyo, hakika hutabaki masikini.

Uwekezaji wa kuchaji simu ninaousema hapa ni ule wa kutumia nguvu ya umeme wa jua. Kama ukiamua kuwekeza kwa kutumia vifaa vya umeme wa jua (Solar energy) na katika kijiji hicho ukawa na uwezo wa kuchaji simu zipatazo 50 kwa siku kwa Tshs 300 kwa simu moja, utakuwa na uwezo wa kujipatia Tshs 15,000 kwa siku. Kama utaweka vifaa vyenye kuchaji simu 100 au zaidi hasa kwenye vijiji vyenye watu wengi utaweza kujipatia pesa zaidi ya Tshs 30,000 kwa siku. Kwa mwezi unaweza kukusanya katи ya Tshs 450,000 na Tshs 900,000.

Kijijini haya ni mapato makubwa sana. Yaweza isiwe kila siku kupata kiasi hicho, lakini itoshe tu kusema kwamba ukiwekeza kijiji kwenu katika mradi huu wa kuchaji simu hakika hautakosa mapato ya kutosha kukuweka kwenye hali bora ya kiuchumi. Unaweza kuamua kuwekeza katika mradi huu hata kwa ajili ya wazazi wako kama bado wanaishi kijijini. Wekeza kwenye mradi huu kwa ajili ya ndugu yako aliyeko kijijini. Wekeza kwenye mradi huu kwa ajili ya kuwezesha wanakijiji wa kijiji chako waweze kuishi maisha mazuri kwa kuwashakishia kuwa simu zao zinakuwa na moto kila siku. Kwa kufanya hivyo, wewe utatajirika huku wananchi wakipata maisha bora kwa sababu ya uimara wa mawasiliano.

#### **54. Mradi wa Hoteli kubwa**

Mradi mwингine wa mabilionea, ni pamoja na hoteli. Hakuna tajiri duniani ambaye ni makini asiyekuwa na mradi wa hoteli. Siyo lazima iwe hoteli ya kitalii au kubwa sana. Hapa ninachokisema ni kwamba matajiri wengi huwekeza kwenye miradi ya hoteli angalau hata ya vyumba 30 au

zaidi. Ukiwekeza kwenye mradi wa hoteli, hakika wewe na watoto wako hamtakuwa katika kundi la watu maskini milele.

Ukitaka ujenge Hoteli ya kitalii au ya kawaida itafaa sana ukitafuta maeneo katika miji mikubwa kama; Arusha, Dar es salaam, Mwanza, Tanga, Zanziba, Morogoro, Kigoma, Kilimanjaro na katika miji mingine yenye vivutio vya kitalii. Kama unao mtaji wa kutosha kujenga hoteli ya nyota moja, mbili, tatu, nne, tano nakadhalika, hoteli hiyo itakuletea kipato wewe, watoto wako, wajukuu zako, wajukuu wa watoto wa watoto wako. Kizazi chako chote hakitakuwa masikini tena milele. Tuchukue mfano wa Hoteli yenye vyumba 40 ikiwa na ghorofa nne tu na kila ghorofa ikiwa na vyumba 10, kama hoteli yako hiyo utauza chumba kimoja kwa Tshs 40,000 kwa siku ni dhahiri kwamba kwa siku utakusanya pesa isiyopungua Tshs 1,600,000.00 na kwa mwezi kama Hoteli yako imekaa vyema na ni katika mji ambao kupata wageni 40 wa kujaza hoteli ni jambo la kawaida, ujue kuwa utakusanya si chini ya milioni 48 kwa mwezi.

Kwa mfano, hata kama gharama za uendeshaji zitafika Tshs 20,000,000 bado wewe mmiliki utabakiwa na salio lisilopungua Tshs 28,000,000 kwa mwezi. Kama umetumia mtaji wa Tshs 1,500,000,000 kujenga hoteli hiyo, ni wazi kwamba pesa yako unaweza kuirudisha ndani ya miaka minne au mitano tu. Nakushauri kabisa kama unayo ploti au kiwanja cha kutosha kujenga hoteli, tafuta mtaji hata kwa kukopa kwenye mabenki, ujenge hoteli haraka. Inalipa sana. Narudia, hakika huu ni mradi wa kimataifa unaotajirisha sana.

Hata hivyo, Kama unayo ndoto ya kuanzisha hoteli ya kitalii au ya kawaida nakushauri ufanye utafiti kwanza. Uwatembelee wamiliki wa hoteli kama hiyo unayotaka kujenga ili upate uzoefu kwao, maarifa, taarifa na uelewa wa jinsi ya kuendesha na kusimamia mradi kama huo. Hakika utafarijika na utatajirika sana. Baada ya miaka mitatu waweza kuwa na utajiri zaidi ya Tshs 1,008,000,000 yaani wewe ni bilionea tayari. Baada ya kipindi cha miaka saba unaweza kujipatia utajiri wa zaidi ya bilioni mbili (Tshs 2,016,000,000). Hivyo, ni wazi kwamba mradi wa Hoteli unaweza kukufanya kuwa bilionea. Usipoteze fursa hii. Anza mipango. Nunua ploti zakutosha Hoteli kuanzia hekari moja au zaidi. Nunua ramani ya Hoteli unayotaka ndotoni mwako.

Anza ndoto ya Hoteli ya ghorofa tatu, ghorofa nne, hadi ghorofa kumi. Anza kununua nondo na matofari na mabati. Anza kutafuta mkopo ikiwezekana kokote kule. Anza ujenzi sasa. Naamini kwamba ukianza kujenga leo tena taratibu hata kwa kutumia kipato chako cha sasa kila Mwaka ukaweka lengo la kufanya kitu, baada ya miaka 3 au 6 tayari utakuwa na hoteli ya vyumba zaidi ya 40 yenye ghorofa 4 au zaidi.

## **55. Mradi wa kusafisha Vyoo**

Miji mingi kwa sasa hasa jiji la Dar es salaam, Mwanza na Arusha inaendelea kuongezeka idadi ya wakaazi wake. Changamoto ya ukuaji wa idadi ya watu katika miji kama hiyo ni kwamba miundombinu yake haikui kwa kasi sawa na ile ya ukuaji wa idadi hiyo ya watu. Kwa mfano jiji la Dar es salaam linakua kwa kasi kubwa sana ambapo sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 ilionesha kuwa jiji hilo lilikuwa na idadi ya watu zaidi ya milioni tano.

Dar es salaam ndilo jiji lenye watu wengi sana Tanzania ikilinganishwa na majiji mengine Tanzania. Ukianzisha kampuni ya kusafisha vyoo vilivyojaa taka hakika hautakosa mapato kwa mwezi. Mradi huu unaweza kukupatia wateja wasiopungua 20 kwa mwezi. Na kama kila mteja anaweza kulipa Tshs 150,000 hadi 200,000 kwa kazi hiyo, kampuni yako yaweza kupata mapato mazuri sana. Kwa mfano Kama kila mwezi utapata wateja wasiopungua 20 wenye kukulipa Tshs 200,000 kwa kazi hiyo utaweza kukusanya zaidi ya Tshs 4,000,000 kwa mwezi. Hii ni makisio ya chini. Na hii ni kwa kampuni ndogo tu inayofanya kazi kwenye ngazi ya mtaa au kata tu. Lakini kama ni kampuni kubwa yenye vifaa na wafanyakazi wa kutosha, kwa mwezi unaweza kupata wateja hata zaidi ya 90.

Kinachotakiwa ni kuwa na bidii ya kuitangaza kampuni yako na kujitahidi kutafuta wateja zaidi. Waweza kujipatia hadi Tshs 180,000,000 kwa mwezi kama kampuni yako itapata wateja 90 kwa mwezi na kwa bei ya Tshs 200,000 kwa kazi moja. Kumbuka kuwa katika miji mikubwa kama Dar es salaam hao ni wateja wachache. Tena hiyo ni pesa ndogo kwa mwezi. Kupata pesa hiyo 180,000,000 kwa mwezi inawezekana kabisa.

## **56. Mradi wa Shule au Chuo**

Ukumbuke kwamba ongezeko la watoto mashulenii katika shule za serikali limekuwa haliendani na uwezo wa serikali kiuchumi. Hali hii inazifanya shule na vyo viliyoko chini ya umiliki wa serikali kutofanya vizuri katika utoaji wa elimu kwa watoto wetu. Kutohana na hali hii, wazazi na walezi wengi kwa sasa hawajisikii raha kuwapeleka watoto wao kusoma kwenye shule za serikali. Hali hii inakuwa ni fursa sasa kwa wajasiliamali kuwekeza katika elimu.

Kujenga majengo ya shule ya msingi, sekondari au chuo yaweza kuwa ni gharama kubwa sana. Ujenzi wa shule huhitaji mtaji mkubwa sana wa kuanzia mamia ya mamilioni. Kwa mfano kama unao mtaji wa shilingi mia moja milioni au mia mbili milioni unaweza kufanya mradi huu. Ukiwekeza katika elimu hakika wewe utaimarisha hali ya elimu ya watu wa nchi yako huku ukijipatia mamilioni ya pesa. Hakuna aliywewekeza kwenye elimu akabakia maskini toka zama za kale. Kwa mfano kama wewe ukiwekeza kwenye shule au chuo ukawa na shule yenye wanafunzi wasioupungua 350 tu, taraja kujipatia sifa ya kutoa elimu kwa kizazi kijacho huku ukikusanya maelfu ya mamilioni ya pesa. Ukiwa na shule yenye uwezo wa kupata wanafunzi hao 350 kwa ada ya shule ipatayo Tshs 1,200,000 kwa mwaka, ni hakika utaweza kukusanya ada za wanafunzi zipatazo  $350 \times 1,200,000 = 420,000,000$ . Pesa hiyo ukiigawa vyema kwenye matumizi ya lazima ya shule kama vile mishahara ya walimu, wafanyakazi wasio walimu, chakula cha wanafunzi, umeme, maji, usafiri na mengineyo ya muhimu kwa shule kwa mwaka; wewe kama mmiliki wa shule hautakosa kubaki na zaidi ya Tshs 144,000,000 kwa Mwaka.

Maeleo haya siyo hadithi. Ni maeleo yaliyofanyiwa utafiti wa kina na ninaandika vitu ambavyo nina uhakika navyo. Katika nchi kama Tanzania ambapo elimu imeachwa iendeshwe na sekta zote mbili; umma na binafsi, ukiwekeza katika elimu hautabakia fukara kamwe. Je, ukiwa na shule mbili kama hizo utapata pesa kiasi gani? Kumbuka kiasi hicho cha malipo ya ada nimetolea mfano wa ada ya chini au ya kawaida ambayo wazazi/walezi wengi wanaimudu. Kumbuka kuna shule nyingine hapa Tanzania hutoza ada ya hadi shilingi 1,700,000 kwa Mwaka. Kuna shule nnyingine hutoza

ada ya hadi Tshs 5,000,000 kwa mwaka. Pamoja na kwamba kuna haja ya serikali kuingilia swala la ada za shule binafsi kuwa na ukomo, bado shule binafsi zitaendelea kutoza ada si chini ya shilingi 1,000,000 kwa mwaka.

## 57. Mradi wa Ufyatuaji tofali

Tofali zitaendelea kuwa za muhimu sana katika miji mingi ya nchi yetu ya Tanzania. Tofali zitaendelea kuwa za muhimu kwa sababu watu wanaohitaji makazi mapya, ujenzi wa kuta za fensi kwa ajili ya nyumba zao, ujenzi wa majengo makubwa kwa madogo, wanaendelea kuongezeka kila mwaka. Miji yetu mingi Tanzania inakua kwa kasi sana. Mji uliouacha miaka 5 tu ukirudi unaukuta umeshabadilika kabisa kwa wingi wa nyumba na watu.

Kuna matofali ya block, ya kuchoma na yale ya kutikiswa kwa umeme (vibrated blocks) na yale ya kushikana kwa meno maalum. Unaweza kuamua kufanya mradi huu hata kama uko kijijini siyo lazima iwe mijini. Vijijini wapo watu wengi hufyatua matofali ya kuchoma na wameweza kutajirika kabisa. Ukiamua kuwekeza katika mradi huu, kwa mwaka wewe hautakuwa mtu anayeishia kulialia kwamba hana pesa.

Kwa mfano tofali moja la block lenye unene wa inchi nne hadi sita kwa tisa katika miji kama wa Mwanza linauzwa Tshs 1000 hadi 1400. Kwa kutumia mashine za kisasa zitumiazo umeme ukifanya upelelezi wa kukusanya taarifa utagundua kwamba wanaowekeza katika mradi huu wanapata faida sana. Ukifyatua tofali zipatazo 10,000 ukauza kwa Tshs 1,000 utakuwa na uwezo wa kukusanya Tshs 10,000,000. Hata hivyo itategemeana matofali hayo mzunguko wake utakuwa wa miezi mingapi na wingi wa kazi za ujenzi katika mji husika.

Hapa ielewewe kwamba katika miji inayokua haraka kama vile Mwanza, Dar es salaam, Arusha, Mbeya, Morogoro, Dodoma na Tanga idadi hiyo ya matofali ni ndogo sana na inaweza kuisha ndani ya mwezi mmoja tu kwa wateja wanne tu wanaonunua tofali 2500 kila mmoja. Kwa hiyo hata ukifyatua tofali zipatazo 20,000 ujue kuwa zawea kuisha ndani ya mwezi mmoja. Endapo utakuwa umevutiwa na mradi huu, nakushauri kama kawaida uwaone watu wanaoufanya mradi kama huu ili upate ushauri na maarifa ya vitendo zaidi. Lakini itoshe tu kusema kwamba huwezi ukawa fukara kwa kufyatua tofali za kuuza kwa wanaojenga majumba yao.

## **58. Mradi wa Kampuni ya Ulinzi**

Kutokana na hitaji la usalama katika miji yetu, uhitaji wa walini kwenye ofisi na nyumba zetu umekuwa ukiongezeka kila mwaka. Ofisi nyingi siku hizi hazipendi kuajiri walini, badala yake zinatafuta makampuni huru na kuingia nayo mikataba ya kuwalindia maofisini na majumbani mwa wafanyakazi maafisa waandamizi wa mashirika na serikali.

Hali hiyo inakuwa ni fursa kwako wewe mjasiliamali. Ushauri muhimu kwako ni kwamba ukitaka upate pesa nyingi sana kupitia fursa hii, ni lazima ufungue kampuni ya Ulinzi na uajiri vijana wengi waliomaliza darasa la saba hadi kidato cha nne waliofuzu mafunzo ya jeshi la mgambo au Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Kama kampuni yako itakuwa imejipanga vyema kwa maana ya kuwa na vibali vyote vya kisheria kumiliki silaha au kuwa na walini wenye kutumia silaha za moto na baridi, hakika wewe utajipatia pesa za kukutosha. Kwa uzoefu nilioupata kutoka kwenye mashirika mengi yanayochukua kampuni za ulinzi ikiwemo shirika ninalofanyia kazi kwa sasa, ni kwamba kwa kila mlinzi kampuni yako italipwa kati ya Tshs 177,000 hadi 350,000.

Mashirika mengine hulipa hadi Tshs 500,000 kwa mlinzi mmoja kutegemeana na usalama wanaoutaka wenye mali au kulingana na mali zilizopo kwenye biashara yao. Kwa uzoefu wa kampuni nyingi hadi sasa (Mwaka 2014) kila mlinzi hulipwa mshahara wa kati ya Tshs 80,000 na 150,000 kwa mwezi. Hata hivyo mimi huwa sikubaliani na makampuni ya ulinzi yanayowalipa walini wafanyakazi wao kiasi cha chini ya Tshs 150,000 kwa mwezi. Pamoja na hayo, tuchukulie mfano wa kiwango cha chini ili kupata picha ya kufanya maamuzi ya kiuwekezaji. Kwa mfano kama kampuni yako utaa jiri vijana 100 wanaolinda vituo 30 kwa wastani wa walini 3 kwa kila lindo, na kama mteja wa kampuni yako atakulipa Tshs 250,000 kwa kila mlinzi, na wewe ukawa unawalipa walini wa kampuni yako kiwango kizuri cha Tshs 150,000 kwa mwezi, hii ina maana kwamba kampuni yako itaingiza Tshs 250,000 x 100 sawa na Tshs 25,000,000 kwa mwezi. Ukitoa matumizi ya kuwalipa mishahara wafanyakazi wako ambao utapaswa uwalipe Tshs 15,000,000 utabaki na Tshs 10,000,000 kila mwezi. Kwa hiyo wewe kama mmiliki utapata pesa zipatazo milioni kumi. Ukipanga vyema kwenye mradi huu hautabaki maskini kamwe.

## 59. Mradi wa Kuchapisha Magazeti

Katika miradi iliyompa utajiri mkubwa kaka mmoja anaitwa Eric Shigongo mmiliki wa kampuni inayochapisha magazeti ya UWAZI, IJUMAA, CHAMPION, nk ni kuchapisha magazeti. Huyu ndugu kulingana na maandiko yake, alianza akiwa maskini wa kutupwa yeye na familia yake na sasa ni mtu tajiri mkubwa Tanzania. Kwa sasa Eric Shigongo anamiliki makampuni makubwa mengi yanayopatia pesa nyingi sana. Alianza kwa kuhangaiaka sana akiwa hana hata mtaji kabisa. Aliwaendea wachapaji wa magazeti akiwa na nakala ya chapisho lake kuu (master copy) na akawasihi mara tatu wamchapishie gazeti lake wakakataa kabisa. Mara ya nne alipowaomba wakakubali kwa shingo upande. Yeye mwenyewe katika ushuhuda wake; Erick Shigongo anasema, walipomkubalia kuchapa gazeti lake kwa mara ya kwanzা wakawa wamefanya kosa. Tokea siku hiyo mwaka 1998 hadi leo siyo mtu maskini tena.



Mfano wa magazeti ya Tanzania

Mradi wa kuchapisha magazeti unaweza kukupa fedha nyingi sana hadi ukawa milionea kama siyo bilionea. Ni kweli kwamba Tanzania kuna magazeti mengi sana. Huenda Tanzania ikawa ndio nchi inayoongoza kwa kuwa na wingi wa magazeti katika ukanda huu wa Afrika mashariki. Hata hivyo, kama wewe ni mbunifuf sana unayeweza kuja mtaani na ubunifuf wa kipekee, ukabuni gazeti lenye mwonekano na maudhui tofauti na wengine hakika utakuwa tajiri bilionea. Kama ukichukua mfano mdogo tu, ukifanikiwa kuchapisha gazeti hilo zuri ukaliuza kwa shs 500 au 700

mtaani na ukachapisha nakala zipatazo 200,000 za magazeti ukazisambaza nchini kote unaweza kujipatia utajiri mkubwa sana. Hebu zidisha uone utapata kiasi gani kama wewe utakuwa unapata Tshs 400 kwa kila nakala inayouzwa mtaani. Ukizidisha Tshs 400 x 200,000 = 80,000,000. Unaona? Utapata Tshs 80,000,000 kwa kuuza nakala 200,000 tu nchi nzima. Pesa hizo unaweza kuzipata kwa wiki moja tu kama gazeti lako litakuwa linatoka kila wiki. Hapo ukumbuke nimetoa gharama za usambazaji na uwakala. Gharama ambayo sijaitoa ni kodi ya serikali.

Kwa hiyo kama unamiliki gazeti moja tu na gazeti hilo unatoa nakala laki mbili tu kila wiki na kwa kila nakala wewe unatakiwa ujipatie Tshs 400, hakika wewe kwa wiki moja tu utakuwa na uwezo wa kujipatia kitita cha Tshs 80,000,000. Hata kama kutakuwa na gharama nydingine ambazo zimefichika bado wewe hautakosa Tshs 40,000,000 kwa wiki. Yaani hapa nimeamua kabisa nitoe gharama zote utakazozifikiria ikiwemo kodi, mishahara ya waandishi wa habari, wahariri, wenyе mitambo ya uchapaji, nk. Bado wewe utapata siyo chini ya Tshs 40,000,000 kwa wiki. Kwa mwezi wewe tayari utakuwa unaweza kukusanya kitita kikubwa cha zaidi ya Tshs 160,000,000 kama mmiliki wa kampuni. Je, unayo ndoto ya kumiliki gazeti? Unataka Mshahara wa Tshs 160,000,000 kwa mwezi? Anzisha gazeti lako pendwa. Anzisha gazeti makini. Nawe utashangaa jinsi mabilioni ya pesa yatakavyokufuata.

Kumbuka kuwa Kanuni ni ile ile niliyoisema kwenye miradi mingine. Hakikisha umewatafuta wamiliki wengine wa magazeti unayoyajua akiwemo kaka Erick Shigongo wakupe uzoefu na changamoto walizokutana nazo au wanazokutana nazo na wakupe njia wanazotumia kukabiriana nazo. Usikurupuke. Usijifungie ndani ya chumba chako ukaamua kuanza gazeti kesho bila kuwatafuta waliokutangulia. Kumbuka kuwa kitabu hiki hakifundishi watu mbinu za kujipatia utajiri wa harakaharaka. Kama wewe unataka utajiri wa haraka haraka kitabu hiki hakikufai. Kitabu hiki ni cha wachapa kazi, wenyе nia ya kuendeleza nchi yetu kwa kutoa mchango wa mali au vipaji vyao kuleta maendeleo ya jamii na familia zao binafsi kizazi hadi kizazi.

## **60. Mradi wa Redio ya FM**

Kituo cha redio kinaweza kukutoa kwenye umaskini wako mpaka ukashangaa sana. Vituo vingi vya redio tofati na magazeti vinaendeshwa na matangazo ya wafanyabiashara na huduma mbalimbali katika jamii watu wanaotaka huduma na biashara zao zifulikane. Bila matangazo vituo vya redio havipati pesa ya uendeshaji ukiacha vituo vya redio isipokuwa vile vinavyomilikiwa na serikali. Matangazo mengi ya redio huwa ya urefu wa sekunde 15, 30, 45 au 60. Yapo matangazo marefu yanayochukua hadi dakika 3. Kusema kweli tangazo linalochukua dakika 3 huwa ni refu sana. Na linalipiwa pesa nyingi.

Kwenye redio gharama ya matangazo siyo chini ya Tshs 40,000 kwa tangazo fupi la sekunde 15, 30 au 45. Hapa ni kwa mifano ya redio ambazo siyo za kitaifa hasa zile za masafa ya FM ambazo nyingi huwa zinasikika kwenye ngazi ya mkoja tu. Kwa redio zinazosikika kwenye zaidi ya mkoja mmoja, tangazo moja hugharimu zaidi ya Tshs 100,000 kwa tangazo la urefu wa sekunde 30. Kwa ufupi mradi wa redio unaweza kukulipa vyema hadi ukawa milionea mkubwa sana.

Kwa mfano kama wewe unamiliki kituo cha redio hata kama redio yako inasikika kwenye mkoja mmoja tu na ukapata matangazo 50 kwa siku na kila tangazo ni Tshs 100,000 utapata Tshs 5,000,000 kwa siku unaweza kukusanya Tshs 5,000,000. Haya ni makisio ya kiwango cha chini tena kwenye kituo cha redio ndogo tu. Je kwa mwezi utakusanya pesa kiasi gani? Inakisiwa kuwa waweza kukusanya hadi Tshs 150,000,000 kwa ajili ya uendeshaji wa redio hiyo. Ukweli unabakia kwamba kituo cha redio ukikiendesha vyema, utapata utajiri sana. Hakikisha kwamba unakiendesha kituo hicho kwa weledi na umakini ili uwe na kituo chenye kujitofautisha na vituo vingine.

## **61. Mradi wa kituo cha Televisheni**

Kama unao uthubutu wa kutosha na kama wewe unataka uwe milionea hadi bilionea tafuta ujanja wote uanzishe kituo cha televisheni. Unaweza kuomba masafa ya TV kutoka mamlaka ya mawasiliano (TCRA).

Kosa watakalofanya watu wa mamlaka ya mawasiliano (TCRA)itakuwa kukupatia masafa. Ukipata masafa ya TV ujue tayari kampuni yako imeshaumaliza umaskini. Kama nilivyoeleza kwenye mradi wa redio, kituo cha TV hupata mapato yake kwenye matangazo. Kwenye TV gharama ya matangazo ni kubwa zaidi ya redio. Tangazo moja la urefu wa sekunde 30 au 60 laweza kugharimu zaidi ya Tshs 500,000 kwa kurushwa mara moja tu. Kama tangazo linaludiwa mara tatu litatakiwa kulipiwa si chini ya Tshs 1,500,000.

Kuna matangazo mengine hugharimu hadi zaidi ya Tshs 1,000,000 kwa tangazo moja lenye ukubwa wa sekunde 60 au kutegemeana na tangazo liliyvo. Kama tangazo lina mbwembwe nyingi kama yale matangazo ya Coca Cola, Vodacom, Airtel, Tigo, Bia, nk tangazo hilo laweza kugharimu zaidi ya Tshs 1,000,000 kwa tangazo moja la dakika moja yaani sekunde 60. Hebu tufanye kwamba kituo cha TV kinapata matangazo yapatayo 10 kwa siku yenye urefu wa dakika moja maana yake ni kwamba utakusanya Tshs 10,000,000 kwa siku. Ukweli ni kwamba unaweza kukusanya zaidi ya Tshs 300,000,000 kwa mwezi kama matangazo kutoka kwa wateja. Na kama kituo chako cha TV kimekaa sawa na kinaendeshwa kwa weledi na kinavutia watazamaji wengi hakika wateja wengi wataleta matangazo yao kwa wingi. Kituo kinawenza kukusanya zaidi ya pesa hiyo kwa mwezi. Pamoja na kwamba kuna gharama za kulipia leseni TCRA, serikalini, wafanyakazi, umeme, simu, nk bado wewe kama mmiliki wa kituo bado utabaki na fedha nyingi sana.

Ukitaka kujifunza jinsi ya kuendesha kituo cha TV ili uwe bilionea watafute watananzia wanaomiliki vituo vya TV kama akina Dr. Reginald Mengi anayemiliki vituo vya ITV, EATV, CAPITAL TV, na wengineo wanaomiliki vituo vya TV. Huyu mzee Mengi ni mionganoni mwa matajiri wakubwa sana wa Tanzania ambaa wanapaswa kuwa mifano kwa watananzia wengine. Tafuta kila njia uweze kuonana naye kabla ya kuanza chochote. Hakikisha pia kuwa unawaona watu wa mamlaka ya mawasiliano TCRA kabla hujafanya lolote wao watakuwa ushauri wa kitalaa zaidi. Je, unataka uwe na mshahara zaidi ya Tshs 100,000,000 kwa mwezi? Anzisha kituo cha televisheni nawe hautakuwa maskini kamwe.

## **62. Mradi wa Bodaboda**

Kwa miaka ya hivi karibuni, usafiri wa watu wengi umekuwa ni pikipiki maarufu kama “bodaboda” pamoja na zile pikipiki za miguu mitatu maarufu kama “bajaji”. Usafiri huu umetwaa nafasi kubwa ya usafiri wa taxi uliokuwepo siku za nyuma hasa mijini. Lakini siku za hivi karibuni usafiri wa bodaboda umeenea kote nchini mijini na vijiji. Umekuwa usafiri unaotegemewa na kukimibiliwa na watu wote hasa wenyewe kipato kidogo na cha kat. Sehemu nyingi nauli za mizunguko ya mijini huwa kat. ya Tshs 1,000 hadi 5,000.

Kwa uzoefu wa sehemu nyingi na miji mingi waendesha bodaboda hupata kipato kuanzia Tshs 10,000 hadi 40,000 kwa siku. Kama mtu anaendesha pikipiki ya mtu kwa mkataba wa kuleta mapato jioni, mwendeshaji bodaboda huyo atapaswa kupeleka kwa tajiri huyo angalau Tshs 40,000 kwa wiki kwa uzoefu wa walio wengi katika miji mingi niliyowahoji vijana waendesha bodaboda. Kama ungependa kuwekeza kwenye mradi kama huu, ukaamua Kununua pikipiki zipatazo 10 tu na ukawaajiri vijana 10 kwa mkataba wa kulipwa angalau Tshs 40,000 kwa wiki; utakuwa na uhakika wa kukusanya Tshs 400,000 kwa wiki moja. Kwa mwezi unaweza kukusanya Tshs 1,600,000. Kwa hiyo kama wewe unaweza kufanya mradi kama huu na ukausimamia vyema na kwa weledi, utakuwa na uhakika wa kupata zaidi ya Tshs 1,600,000 kwa mwezi.

Hata hivyo, ukumbuke kwamba mradi huu unazo changamoto nyingi sana. Ni vyema ukazifanyia utafiti mkubwa ukajifunza vikwazo, vizuizi, na matatizo ili uanzapo usikwame njiani. Ukiamua kuendesha mradi huu kwa kuusimamia kila siku unaweza akawaajiri vijana 10 na ukawa unawasimamia kila siku ikawa ndiyo kazi yako au ukamweka meneja wako akawa anawasimamia wafanyakazi wako. Kwa kufanya hivyo, kila siku unaweka lengo la kukusanya Tshs 10,000 kwa kila bodaboda kwa siku ili kwa pikipiki zote 10 upate Tshs 100,000.00 na mwisho wa mwezi upate Tshs 3,000,000. Hakikisha umejifunza na kujiridhisha kukabiliana na changamoto zote zinazoambatana na mradi kama huu. Kumbuka mradi huu unaweza kukufaa endapo tu utakuwa na usimamizi wa karibu.

### **63. Mradi wa Stationery (Sajala)**

Kama ilivyo kwa miradi mingine mingi iliyoelezwa katika kitabu hiki, mradi wa kuuza sajala maarufu kama “stationeries” nao waweza kukutoa sana kwenye ukosefu wa pesa na ukakuweka kwenye utajiri mkubwa. Ukitifungua mradi wa kuuza Sajala za maofisi na mashulenii na kutoa huduma za kutoa nakala maarufu kama fotokopi (photocopy) inaweza kukupa faida kubwa.

Hata hivyo, mradi huu wafaa sana mahali penye huduma nyingi za shule, vyuo au maofisi ya kutosha. Kama utapata sehemu iliyoko karibu na shule au chuo hasa vyuo vya elimu ya juu, mradi wako utapata pesa nyingi. Hii ni kwa sababu wanafunzi wa elimu ya juu wanakuwa na kazi nyingi za kutoa nakala, na kuchapisha kazi nyingi. Kama hujapata eneo lenye watu wengi wanaotumia sajala hasa maofisini na vyuoni siwezi kukushauri uanzishe mradi huu mahali popote. Endapo utapata eneo la kibashara lenye kukufanya uwe na kazi nyingi (busy) asubuhi hadi jioni ukiiza sajala, kuchapa kazi za wateja, kutoa ‘copy’ za wateja hakika utajikuta una pesa nyingi sana kwa siku. Kwa mfano kama wewe una mashine ya kutoa nakala (photocopier machine) na kwa siku unatoa nakala sizizopungua 2000 kwa bei ya Tshs 100 tu, utaweza kujikusanya zaidi ya Tshs 200,000 kwa siku. Kwa mwezi waweza kukusanya hadi Tshs 6,000,000. Hapo tunazungumzia kazi ya kutoa nakala tu. Bado hatujasema kuhusu kuchapa kazi za wateja, kuuza sajala kama vile madaftari, rula, kufunga makablasha (binding of pamphlets), nk. Hii ndiyo kusema kwamba kwa mwezi waweza kukusanya zaidi ya Tshs 8,000,000 kama umejipanga na kama umepata eneo zuri kwa biashara ya sajala.

### **64. Mradi wa mashine ya Kusaga/kukoboa Nafaka**

Mradi huu unawafaa watu wengi hasa waishio maeneo ambayo yana wakulima wengi wa nafaka kama mahindi na mpunga. Mikoa yenye wakulima wengi wa nafaka hizo kama vile Mbeya, Mwanza, Shinyanga, Rukwa, Kigoma na Katavi wanaweza kufaidika zaidi kwa kuanzisha mradi kama huu. Hata hivyo, kwa watu wanaoishi mikoa ambayo siyo maarufu kwa kilimo cha nafaka bado pia wanaweza kufanya mradi huu kwani wanazo fursa tele za Kununua nafaka kutoka mikoani inakozalishwa nafaka na kuweza kufanya mradi vyema kabisa.

Unachotakiwa kufanya ni Kununua mashine ya kusaga, kukoboa, ghalia ya kuhifadhiya nafaka na mifuko ya kufungashia unga au mchele uliokobolewa tayari kwa kuwauzia wateja. Hakikisha kwamba mashine yako ina uimara wa kutosha. Yaweza kuwa mashine ya kutumia nishaati ya umeme au dizeli kwa wale walioko vijiji ambako hakuna nishati ya umeme wa gridi ya taifa. Kama unataka mradi wako uweze kuzalisha faida ni muhimu sana ukawa unasaga mahindi na kufungasha unga kwenye mifuko ili kuwauzia watu wanaohitaji unga uliokwishatayarishwa kwa matumizi. Aidha, kama unakoboa mpunga, ni vyema ukahakikisha kuwa husubiri wateja wakuletee kazi za kufanya bali wewe unanunua mpunga na kuukoboa na Kuweka mchele kwenye mifuko midogo na mikubwa ili wateja wanapofika wakute tayari mchele uko tayari. Usifanye mradi huu kwa kutumia njia za kizamani za kusubiria wateja walete mahindi au mpunga ndipo wewe uwasagie au uwakobolee. Hiyo imepitwa na wakati.

Uhakika ni kwamba, kama ukifanya hivyo, kwa siku unaweza ukakusanya zaidi ya Tshs 150,000 ambapo utakuwa na uhakika wa kujipatia zaidi ya Tshs 4,500,000 kwa mwezi. Ukiijipanga vyema waweza kujipatia hadi Tshs 200,000 kwa siku sawa na Tshs 6,000,000 kwa mwezi kama utafanya mradi huu kisayansi na kiufundi. Swala hili linawezekana Kama ukijipanga vyema na ukahakikisha kwamba unachochumba cha kuhifadhiya mazao ya mpunga au mahindi yanayosubiri kukobolewa au kusagwa tayari kwa mauzo. Mradi huu unawafaa sana watu waliostaafu, vijana waliomaliza vyuo au waliomaliza mafunzo yoyote ya ujasiliamali.

## **65. Mradi wa studio ya kurekodia Nyimbo au Matukio**

Mradi huu umeanza kuonekana kuwa unaweza kuwa na faida kubwa sana hasa baada ya kuanza kuwepo wasanii wengi wa nyimbo za injili na muziki wa bongofleva. Hata hivyo siyo lazima kurekodi nyimbo peke yake. Ukianzisha mradi huu waweza kurekodi vipindi mbalimbali na ukaviuza kwenye vituo vya redio na televisheni. Unaweza kurekodi picha za harusi, na sherehe mbalimbali na ukajipatia pesa nyingi. Unaweza ukawa na watalaam wa kupiga picha za kawaida, ukawa na vyombo vya kufaa kukodishwa kwenye mikutano mbalimbali. Unaweza ukawa na jukwaa la kukodisha kwa ajili ya mikutano.

Yote hayo ukiwa nayo, unapochukua zabuni kwa mtu unaweza ukawa unakwenda ukiwa kamili yaani, unapiga picha za video, unarekodi matukio, unatoa vyombo na jukwaa la mikutano. Kama unafanya mradi huu kwenye mji mkubwa kama Dar es salaam unaweza kujikuta studio yako inakusanya zaidi ya Tshs 5,000,000 kila wiki kwa kukodisha na kurekodi nyimbo, mahubiri, muziki, mikutano mikubwa na mengineyo. Kama studio yako inaingiza takribani Tshs 5,000,000 kwa wiki wewe na wafanyakazi wa studio yako hamtakuwa maskini kamwe. Kwa mwezi waweza kuingiza hadi Tshs 20,000,000 wewe ni kuamua tu.

Aidha, kama kila wiki unapata wateja 5 wanaorekodi nyimbo zao, filamu, zao vipindi vyao, nk, na kila mteja ili aingie studio lazima alipe angalau Tshs 350,000 utakuta kwa wiki unakusanya pesa zipatazo Tshs 1,750,000 kwa wiki moja. Kwa mwezi waweza kukusanya mapato yanayokadiriwa kufikia Tshs 7,000,000. Kumbuka kuwa ukijenga studio nzuri sana, yenye viwango vizuri na vya kimataifa, kamera nzuri na za viwango vya kimataifa; hakika utapata pesa tele tele kwa mwezi. Mpaka zabuni nydingine utazikimbia kutokana na ukosefu wa muda wa kuwatoshleza wateja wote. Watu wengi hupenda kufika kwenye studio ambazo zina viwango vya hali ya juu katika kurekodi kazi zao.

Kwa ufupi ni kwamba ukianzisha studio ya kurekodia kazi mbalimbali ikiwa na viwango vya hali ya juu kama hivyo, pale ambapo kila kitu kinapatikana kwenye studio hiyo, waweza kuingiza hadi Tshs 27,000,000 kwa mwezi. Fanya utafiti kuhusu mradi huu nawe hakika ujionee. Ni wakati wako wa kuondoka kwenye umaskini. Mradi kama huu unaweza kuwafaa sana watu walio na ujuzi wa maswala ya teknolojia (ICT), na wengine wenye wazo hilo.

## **66. Mradi wa Uwakala**

Unaweza kutajirika sana hadi kuwa bilionea kwa kuwa Wakala wa taasisi au kampuni yoyote duniani. Kwa mfano unaweza kuwa wakala wa kampuni za Bima za Magari, Bima za Afya, Bima za Majengo, Mifuko ya Pensheni, nk. Unaweza kuwa Wakala wa Benki kama CRDB kuititia huduma zake za FAHARI HUDUMA. Unaweza ukawa Wakala wa Kampuni za Coca Cola au Pepsi Cola.

Unaweza ukawa Wakala wa Tanzania Breweries Ltd kuuza vinywaji vyao, unaweza ukawa Wakala wa Mbegu au Pembejeo za Kilimo, unaweza ukawa Wakala makampuni ya Bakheresa kusambaza unga wa ngano au bidhaa za kampuni zake kama vile Azam Tv, Vinywaji vyake vya Malta, Unaweza ukawa Wakala wa kampuni za dawa asilia kama Forever Living, Dynapharm, GNLD, Waweza kuwa wakala wa makampuni ya simu (Vodacom, Tigo, Zantel, Airtel) kama Wakala mkuu wa mkoa au wilaya wa kusambaza vocha za muda wa maongezi, kutoa au Kuweka pesa, nk. Hakika utakuwa bilionea kwa kufanya kazi hiyo. Kwa mfano kama wewe ni Wakala wa kampuni kama ya Coca Cola ukawa unapewa bonasi ya Tshs 100 kwa kila soda unayouza kwenye uwakala wako, ukifanikiwa kuuza soda zipatazo 300,000 kwa mwezi sawa na kreti zipatazo 1000 utapata malipo yasiyopungua Tshs 30,000,000. Kumbuka kama unafanya biashara eneo lenye watu wengi kuuza kreti 1000 kwa mwezi ni jambo la kawaida kabisa.

Mfano mwingine; ukipata fursa ya uwakala wa bidhaa za unga wa Azam yaani Mzee Bakharesa akakupa kuwa wakala wake wa unga wa ngano katika Mji wowote Tanzania au Afrika Mashariki na ukaweka biashara yako maeneo ambayo unga wa ngano unauzika zaidi hasa mijini hakika utatajirika sana. Ukipewa bonasi ya Tshs 300 kwa kila kilo ya unga unayouza kama Wakala na ukafanikiwa kuuza kilo zipatazo 100,000 kwa mwezi, utakuwa na kipato kisichopungua Tshs 30,000,000 kila mwezi. Ukweli ni kwamba biashara ya Uwakala inalipa. Ukitaka kuifanya ni vyema ukatafuta kila linalowezekana ukawasiliana na wenye makampuni au wakurugenzi wa kampuni husika unayotaka uwe wakala wake.

## SURA YA TATU

### **MAMBO 34 AMBAYO NI MWIKO KWA MATAJIRI**

Hongera kwa kukamilisha kusoma sura ya pili iliyokuwa inazungumzia miradi ipatayo 66 yenye uwezo wa kukutoa kwenye umaskini. Sasa ni imani yangu kwamba hata kama hujaanza mradi wowote, hata kama huna senti mfukoni, sasa unayo mawazo chanya kuelekea kuwa tajiri bilionea. Ubilionea huanzia kwenye mtazamo na kwenye mawazo. Kwa sasa baada ya kusoma sura iliyopita ya kitabu hiki ni hakika una mtazamo tofauti na awali. Unapanga sasa jinsi ya kubadilisha viwango vya maisha yako. Bila shaka umebadilika kimtazamo na unapanga kuwa tajiri mkubwa Afrika yote ikiwezekana.

Katika sura hii, utapata kuelewa miiko ya matajiri. Utaelewa ni kipi tajiri hapaswi kufanya katika jamii na kipi anapaswa kufanya. Inabidi ieleteweke kuwa kila jamii ya watu huwa na utamaduni wao wa kuishi kila siku. Utamaduni ni jumla ya miiko, desturi na mienendo ya jamii Fulani katika kuishi na katika kazi zao za kila siku. Kusema ukweli hata Matajiri nao duniani wanayo maadili, miiko, desturi na tamaduni zao zinazowafanya waendelee kuwa matajiri au wajiondoe kwenye ulimwengu wa kuitwa matajiri. Matajiri wanao utamaduni wao ambao kwa kuufuata wanaendelea kuwa matajiri. Watu wasiokuwa matajiri huwa wanashangaa kwa nini matajiri wanaishi kwa namna hiyo. Lakini matajiri wanaishi hivyo ili kulinda utajiri wao wa sasa uendelee kuwepo hadi kwa watoto wa watoto wa watoto wao. Ukifuata mtindo huu wa maisha, ukajiepusha na maswala ambayo matajiri wengine hujiepusha, wewe pia utaendelea kuwa tajiri maisha yako yote. Yafuatayo ndiyo mambo ya kuepuka kama unataka uwe na utajiri usiokwisha:

#### **1. EPUKA KUFANYA MIRADI YA UPATU**

Hakuna matajiri wanaocheza bahati nasibu. Kama unataka uwe tajiri epuka kabisa kucheza michezo ya pesa. Ukishakuwa tajiri wewe siyo mtu wa kuchea pesa tena. Upatu ni michezo ya watu maskini. Achana na michezo hiyo. Usivutiwe kamwe na miradi inayosemekana kwamba inaleta pesa kubwa na kwa haraka. Epuka pesa za haraka haraka au “money faster”.

Miradi ambayo huna utafiti nayo wala kuielewa au inayoletwa kwako na mtu anayetaka mkaifanye haraka haraka kwa hoja kwamba inaleta faida ya haraka achana nayo kabisa. Epuka biashara za upatu. Hazifai kabisa.

## **2. EPUKA KUNUNUA VITU VISIVYO NA FAIDA**

Wataalam wa uchumi wanasema, kama unanunua vitu visivyo na faida kiuchumi na kuvipeleka nyumbani, utaanza kuza vitu muhimu toka nyumbani kwako ili uweze kukidhi haja ya mahitaji yako muhimu. Watalamu wa maswala ya fedha wanashauri kwamba, ikiwa unataka uwe na maendeleo endelevu, unapaswa kuepuka kununua vitu visivyo na faida nyumbani kwako.

Kabla hujanunua kitu na kuvipeleka nyumbani, jiulize kitaleta manufaa gani nyumbani kwako au katika miradi yako. Kama unataka kununua redio, television ya bei ghali, Simu ya bei ghali, nguo za bei ghali, viatu vya bei ghali, nk, jiulize kwanza kama vina manufaa kwako kwa wakati huu au vinaweza kusubiri? Kama kitu kinaweza kusubiri kununuliwa na maisha au mradi wako ukaenda bila kitu hicho, hiyo itakuwa ni sababu tosha kwamba kitu hicho siyo muhimu kwako kwa muda huo.

## **3. EPUKA KUZAA WATOTO WENGI**

Kuzaa watoto wengi hasa zaidi ya wanne, ni tabia au utamaduni wa watu maskini. Wewe kama bilionea hauna sababu ya kuwa na idadi kubwa ya watoto. Unashauriwa kuzaa watoto wasiozidi wanne kama sera ya serikali ya Tanzania inavyosema kwa watumishi wa umma. Hata hivyo, ifahamike kwamba Tanzania hakuna sheria ya kuzuia watu wasizae idadi ya watoto kadri wanavyoweza. Idadi ya watoto kwa kila mzazi imeachwa iwe uamuzi wa wazazi wenyewe. Pamoja na hayo, uzoefu duniani kote hata katika maandiko matakatifu kama Biblia, unaonesha kwamba matajiri wote duniani hawakuzaa watoto wengi mno kama ilivyo kwa familia masikini za Afrika na hususani hapa Tanzania.

Kwa maudhui ya kitabu hiki, nashauri uzae watoto wanne au chini ya watoto yake. Kwa mfano ukizaa watoto wawili au watatu ni njema zaidi. Ukifuatilia duniani kote, ukweli utakaoupata ni kwamba kwa wastani matajiri wengi

duniani hawazai watoto wengi kama ilivyo kwa familia fukara kiuchumi na kifedha. Mamilionea na mabilionea wengi unaoweza kuwataja duniani karibu wote walizaa watoto wachache. Hata katika Biblia, mtu aliyewahi kuzaa watoto wengi sana ni Yakobo ambaye alizaa watoto wapataao 12. Hata hivyo, Yakobo hakuzaa watoto 12 kwa mke mmoja kama ilivyo leo kwenye familia nyingi za Tanzania ambapo unaweza kukuta mwanamke mmoja amezaa watoto wapataao 13 hadi 16. Yakobo katika Biblia alizaa watoto 12 kwa wanawake wapataao wanne ambapo mwanamke aliyezaa watoto wengi kati ya wake zake alizaa watoto SITA tu ambaye ni Lea aliyezaa; Reuben, Simeoni, Lawi, Yuda, Isakari, na Zabuloni. Wake zake Yakobo waliosalia walizaa watoto wasiozidi wawili.

Kwa mfano, Raheli alizaa watoto wawili ambao ni Yusufu na Benyamini. Naye Bilha alizaa watoto wawili tu; Dani na Naftali. Aidha, Zilpa aliweza kumzalia Yakobo watoto wawili ambao ni Gadi na Asheri. Kwa hiyo utaona kwamba Mzee Yakobo wa Biblia alizaa watoto 12 kwa wanawake wafuataao; Lea aliyezaa watoto 6, Raheli aliyezaa watoto 2, Bilha aliyezaa watoto 2, na Zilpa aliyezaa watoto 2. Ukitaka kupata maelezo zaidi kuhusu habari hiyo ya Yakobo waweza kuipata kutoka kitabu cha Mwanzo sura ya 28-35). Kwa hiyo wanaotumia maandiko kutaka kuhalalisha kuzaa watoto wengi kuliko hata uwezo wao kiuchumi na kifedha huenda wanakosea au hawajaelewa maandiko matakatifu. Kuzaa watoto zaidi ya watoto wanne kwa mwanamke mmoja, kwa kisingizio cha Imani ya dini yako huenda ukawa hujachunguza maandiko vizuri.

#### **4 . EPUKA KUZAA KATIKA UMRI MKUBWA**

Jambo la uzazi katika umri mkubwa ni swala lingine ambalo matajiri wengi duniani hujiepusha nalo. Kuzaa ukiwa na umri mkubwa siyo chaguo la matajiri walio wengi kabisa. Katika maudhui ya kitabu hiki ushauri ni kwamba kama umeshatimiza umri wa miaka 42 ni vyema kuacha kuzaa kabisa watoto. Hata kama umebarikiwa kuwa na mtoto mmoja tu hauna sababu ya kuhangaikia swala la kupata mtoto tena. Kama wewe ni mwanamke, unashauriwa kuacha kuzaa watoto ukiwa na umri wa kati ya miaka 35 na 40 ili kuweza kupata muda wa kutosha kutekeleza mipango ya maendeleo.

Kwa upande wa wanaume, kama umri wako ni zaidi ya miaka 42 na unatamani kupata mtoto hadi sasa, ushauri wangu ni kuwa umwone daktari wa maswala ya uzazi akushauri zaidi na uone jinsi unavyoweza kuacha kuzaa watoto. Unashauriwa kuzaa watoto ndani ya umri wa miaka 20 hadi 40 na ukifikisha umri wa miaka 42 huna sababu tena ya kuzaa watoto. Umri wa miaka 42 unatosha sana. Tulia ili ufanye kazi za ujasiriamali hasa kusimamia miradi yako badala ya kushughulikia malezi ya watoto wako wadogo.

Ushauri huu unatolewa kwa sababu endapo utazaa mtoto ukiwa na umri wa miaka 42 unakuwa umebakwa na muda mchache sana wa kuwalea vyema watoto uliowapata kielimu, kiuchumi na kijamii. Mtoto utakayemzaa ukiwa na umri wa miaka 42 yeye ataanza maisha ya kujitegemea akiwa na miaka 18 ambapo wewe kama mzazi utakuwa tayari una umri wa miaka 60 ambao kwa kiasi kikubwa ni umri wa uzee. Kwa mfano; fikiria kama utazaa mtoto ukiwa na umri wa miaka 45, utajikuta unatimiza miaka 60 mtoto wako huyo akiwa na umri wa miaka 15 tu. Umri wa miaka 15 ni mdogo sana kiasi kwamba mtoto huyo atakuwa bado anahitaji malezi yako kama mzazi kwa kiasi kikubwa. Kwa watu ambao wameajiriwa rasmi serikalini au sekta binafsi, ambapo kwa mujibu wa sheria za kazi Tanzania wanapaswa kustaafu kazi itakuwa tatizo kwa mtoto huyo. Mzazi ukiwa na umri mkubwa wa uzee itakuwa vigumu kumtunza mtoto hadi aweze kujitegemea.

Huyu mtoto kama hujaweka msingi mikubwa ya kiuchumi huenda ukashindwa kumsomesha shule ya maana zaidi kwani umri huo ni umri ambao wewe kama mzazi unakuwa umeshazeeka na nguvu za kukimbia huku na kule kutafuta mali zinakuwa zimepungua sana kwa walio wengi.

## **5. EPUKA VYAKULA VYENYE SUKARI NYINGI**

Bilionea anayetaka kuishi miaka mingi yenyе heri duniani, lazima atahakikisha kwamba hatumii Vyakula vyenye sukari nyingi kwa manufaa ya afya yake. Milionea unapaswa kuepuka vyakula kama biskuti na soda zenye sukari kwa wingi. Milionea anashauriwa kula vyakula kidogo sana vyenye mafuta au achana navyo ikiwezekana. Tumia Vyakula vyenye kurejesha afya zaidi kama vile maji ya kutosha kwa siku (lita 2 za maji kwa

siku), mboga na matunda ya kutosha bila kusahau kufanya mazoezi ya viungo vyako.

Kumbuka kwamba ukishakuwa bilionea au milionea utakuwa hutembe i kwa mguu tena mara kwa mara. Mabilionea wengi hutembea kwa magari kwa muda mwingu. Kama utakuwa unatembea kwa gari kila mara bila hufanyi mazoezi ya viungo nyumbani au kwenye viwanja vya michezo kama vile “gym” na viwanja vya mpira, utakuwa unakabiliwa na hatari ya kunyemelewa na magonjwa hatari kama kisukari, Blood Pressure (BP), kansa na upungufu wa nguvu za kiume au za kike na kuhatarisha ndoa yako na utajiri wako.

## 6. EPUKA ULEVI WA KUPINDUKIA

Matajiri wengi duniani wamefanikiwa sehemu kubwa kwa sababu ya nidhamu katika mambo mengi ikiwemo nidhamu ya unywaji wa pombe. Kumbuka kuwa unywaji wa pombe na uvutaji wa sigara na bangi hupunguza uwezo wako wa kufikiri na hatimaye mali zako. Pia hupunguza umri wa kuishi. Kama kuna mtu unamfahamu anavuta sigara sana na kunywa pombe lakini ameweza kuishi hadi miaka 70 au zaidi unapaswa kuelewa kwamba kama angekuwa havuti sigara wala kunywa pombe kwa kiwango kingi angeweza kuishi hadi miaka 120.

Kumbuka kwamba, matajiri wengi duniani hufariki haraka sana kutokana na mifumo yao ya maisha wanayochagua kuishi hasa baada ya kupata mafanikio makubwa kifedha. Jitahidi kuacha kabisa kunywa pombe na kama huwezi kabisa, jitahidi kunywa kiasi kisichozidi glasi moja ya waini (wine) au chupa moja ya bia kila siku unapopata nafasi. Kumbuka kuwa kama unakunywa pombe sana, utakosa muda wa kuwaza na kufuatilia miradi yako, utakosa muda wa kujisomea vitabu vyenye kukuongzeza akili na fikra, utakosa muda wa kutafakari miradi mipy. Utakosa muda wa kufanya uchambuzi wa maswala muhimu ya maendeleo yako na miradi yako. Kama unakunywa pombe bila kipimo maalum unachotaka, kamwe hautafika mbali kifedha.

## **7 . EPUKA KUTOJIENDELEZA KIELIMU**

Kila mtu ambaye amekuwa tajiri mpaka kiwango cha bilionea maishani mwake ukimfuatilia kwa undani utagundua kwamba kilichomwezesha kutajirika siyo mtaji aliopewa na benki au ndugu zake au wazazi wake. Wengi wametajirika kutokana na kusoma vitabu nya waliotajirika.

Milionea au bilionea kuishi bila kusoma vitabu nya mabilionea wengine ni hatari kwa miradi yako. Kitabu chochote kinachohusu utajiri, fedha na uchumi hata kama kimeandikwa na mtu usiyemjua wewe inapendeza kama utakisoma ili kupata ujuzi na uzoefu wa wengine. Epuka kukaa bila kusoma vitabu nya matajiri wakubwa waliofanikiwa. Soma magazeti makini ya Kiswahili, kingereza na lugha nyinginezo unazoweza. Unaweza kusoma kupitia kwenye mitandao ya intaneti kadri unavyoweza.

Ni mwiko kwa tajiri kukaa bila kufuatilia maswala muhimu yanayotendekea duniani au nchini mwake kupitia vitabu au vyombo nya habari. Hakikisha kwamba kila taarifa inayotokea duniani au kwenye nchi yako unaijua na haupitwi na wakati. Soma vitabu zaidi na zaidi vyenye kuhusu kazi, fani yako, au miradi yako. Hudhuria semina na makongamano kila mara inavyowezekana na kila unavyoalikwa. Nunua vitabu vyenye mafunzo yenye akili nyingi zaidi ili usome akili zaidi za watu wengine waliofanikiwa. Kumbuka kwamba unaposoma vitabu unakuwa unasoma akili za watu walioandika vitabu hivyo.

Syo lazima kukaa na mtu fulani mahali pa faragha ili akusimulie jinsi alivyofanikiwa. Kusoma vitabu nya matajiri wakubwa zaidi yako ni njia mojawapo rahisi ya kupata mawazo yao na siri zao zote. Hata mimi ninayezungumza na wewe kupitia kitabu hiki, nimefanikiwa kwa sababu ya kusoma vitabu nya watu wengine waliofanikiwa. Si kwamba nimeshafika kiwango ninachokitaka cha mafanikio, lakini nimefika hapa nilipo kwa sababu ninasoma na kujifunza kutoka kwa wengine waliofanikiwa zaidi yangu. Bilionea ni muhimu sana usome vitabu sana. Jiendeleze kwenye fani yako na uongeze ujuzi, uzoefu, maarifa, ubunifu, nk, kwa kusoma mara nyingi vitabu na machapisho mengi kadri inavyowezekana.

## **8 . EPUKA KUWA NA WAPENZI WENGI**

Kama wewe una mke au mume mmoja hakikisha ukishakuwa milionea usiingie kwenye mtego wa kuwaza kuongeza mke wa pili, wa tatu au zaidi. Endelea kuwa na mke mmoja tu hadi kifo kiwatenganishe. Kama wewe huna dini au wewe ni Muislam usioe wanawake zaidi ya maelekezo ya dini yako au jadi ya mila zenu. Kumbuka kuwa mabilionea wote duniani huepuka kuwa na mahusiano na wanawake wengi. Aidha, kama wewe ni milionea au bilionea wa kike jiepushe kuwa na mahusiano na wanaume wengi kwani utafilisika mapema sana. Kama wewe ni mwanamke uliyetajirika na kwa sababu zilizoko nje ya uwezo wako huna mume wa kuishi naye, unashauriwa utafute mume mmoja tu wa kuishi naye ili kufarijiana au ufunge naye ndoa kisheria. Bilionea mwanamke, epuka kuwa na wanaume wengi, wasije wakakufilisi mali zako zote. Ukiwa na wapenzi wengi huku ukiwa bilionea, wasipokuua watateka mali zako.

Ukifanya uchunguzi utagundua kwamba matajiri wengi waliofilisika walijiingiza katika mahusiano ya kimpenzi na wapenzi wengi na hatimaye wakafilisika haraka sana. Wapo mamilionea waliokuwa wamiliiki wa makampuni makubwa, lakini kwa kukiuka mwiko huu, utajiri wao wote ulipukutika na mpaka sasa hata kumbukumbu yao haipo tena. Nakuomba ujifunze kwao.

## **9 . EPUKA KUWA NA MAJUKUMU MENGI**

Epuka kabisa kuwa na majukumu mengi au kazi nyingi kuliko uwezo wa akili na mwili wako. Jitahidi kuajiri watu wakusaidie kazi katika miradi yako. Tafuta washauri wenyе utalaam wa miradi au biashara zako wakushauri jinsi ya kufanya miradi/biashara zako. Watu wengi hawafanikiwi kwa sababu wanataka kazi zote wafanye wao. Eti wanaogopa kuibiwa. Hakikisha kwamba unaajiri wasaidizi wenyе uwezo ili waweze kukusaidia kutenda kazi zako. Ajiri watoto wako kama wamemaliza shule au vyuo na wanaweza kazi. Ajiri mkeo au mumeo kama anao ujuzi na anaweza kazi hiyo. Mwajiri ndugu yako ye yote kwa kuzingatia uwezo wake na siyo kuzingatia udugu. Ukiajiri kwa kujali udugu au urafiki utaangamiza miradi yako. Ni mwiko kwa bilionea kubeba au kufanya kila kazi kwenye miradi au

kampuni yake. Utazeeka haraka. Bilionea wengi wenye busara hukasimu madaraka kwa watu wengine wamsaidie. Hiyo ndiyo siri ya kufanikiwa kwa mabilionea wengi.

## **10 . EPUKA KUPOTEZA MUDA WAKO**

Jitahidi kuepuka tabia na utamaduni wa kupoteza muda kwa mambo yasiyo na tija kwa miradi yako. Kama wewe unataka uwe bilionea, epuka tabia ya kupoteza muda kwenye mambo yasiyo na maana. Epuka kukaa kwenye vijiwe vyta watu ambao hawakupanui mawazo yako kiuchumi na kifedha.

Epuka kukaa unajadili maswala ya siasa ambazo hazina tija kwako wala kwa biashara zako. Usipoteze pesa yoyote kwenye mambo yasiyofaa wala kuongeza faida kwa mradi wako. Jitahidi uwe na bidii sana kwenye kazi zako. Uvivu uwe adui wa kudumu kwenye kazi zako.

## **11 . EPUKA KUJITENGA NA MARAFIKI ZAKO**

Watu wengi wapatapo utajiri mkubwa huanza kujitenga na marafiki zao au ndugu zao. Kama nilivyoeleza hapo awali, unapaswa kujiepusha na watu au marafiki wasiofaa kwenye biashara yako. Hata hivyo, hii haina maana kwamba uwatupe marafiki zako wote au ujitenge nao.

Kinachopendekezwa hapa ni busara tu za jinsi ya kuwa nao karibu na kuwasaidia kwa mawazo na mtaji kila inapowezekana bila kuwafanya wakutegemee kwa kila jambo. Epuka kuwaruhusu kuwa tegemezi kwako kifedha badala yake wasaidie mawazo na mbini za kujitegemea kama hawajainuka kiuchumi. Wape mtaji marafiki au ndugu kama inawezekana. Badala ya kuwasaidia pesa ndogo ndogo, ni heri ukawapa mtaji siyo wa pesa peke yake bali pia mawazo ya nini wafanye.

## **12 . EPUKA KUKAA BILA MAZOEZI YA VIUNGO**

Matajiri wengi wapatapo mafanikio hujikuta wakinenepeana sana hata kama awali hawakuwa wanene. Hali hii husababishwa na utamaduni wa watu wengi kudhani kwamba eti kunenepa hasa kuwa na vitambi ndiyo ishara ya mafanikio. Epuka kunenepa ovyo. Epuka kula ovyo. Epuka kula Vyakula vitamu sana au vyenye mafuta sana. Epuka kuishi bila nidhamu

ya ulaji. Kula kwa kiasi na adabu na kwa utaratibu ambao utakuwezesha kuwa na afya njema isiyo na magonjwa ya matajiri kama BP, Kisukari, Mfadhaiko, nk. Fanya mazoezi ya kutosha ili kuwezesha miguu na ubongo wako viwe imara wakati wote. Mazoezi ya kutosha yanayopendekezwa na watalaaam wengi ni pamoja na kutembea kwa mguu angalau kila siku kwa muda usiopungua nusu saa na utembee mwendo wa haraka hadi jasho litoke mwilini.

### **13 . EPUKA KUWA NA WIVU MBAYA**

Epuka kuwawazia watu wengine mabaya. Epuka kutaka au kuwaombea wengine waharibikiwe mambo yao. Epuka kutaka kila jambo zuri liwe la kwako kwa gharama ya kuwanyang'anya wengine ili upate wewe. Huu ndio wivu mbaya. Wivu mzuri ni ule wa kutamani kupiga hatua kubwa au nzuri kwa bidii yako binafsi hasa unapokuwa umejilinganisha na wengine ukajikuta wewe bado uko chini.

Kwa mfano unapaswa kujua kwamba ukipata utajiri mkubwa bado kutakuwa na watu wanaokuzidi utajiri. Huwezi kutajirika halafu wewe ukakosa wanaokuzidi utajiri. Kumbuka kila unavyopanda juu kwa utajiri ndivyo utagundua kwamba wapo wanaokuzidi utajiri ulio nao. Kama unamiliki mabasi ya abiria yapatayo 10 kisha ukadhani wewe ndiye mkubwa sana kuwazidi wafanya biashara wa aina hiyo, ujue kuwa kama siyo Tanzania wapo wenye kumiliki mabasi hadi 20 ya biashara tena yenye hadhi ya juu kuzidi hayo uliyonayo.

Kama unamiliki majumba 10 hapa Tanzania na unapata mabilioni ya mapesa ujue kuwa wapo wanaokuzidi na wanamiliki zaidi ya majumba 20 tena siyo Tanzania tu bali hadi nje ya nchi. Kwa hiyo epuka kuonea vivu watu ambao wanakuzidi utajiri badala yake unapaswa kuona kuwa wao kukuzidi mali walizonazo ni chachu na changamoto kwako ya kukufanya ufanye mipango na mikakati zaidi ili kama siyo kuwafikia basi uwakaribie. Usitafute kuwadidimiza waliokuzidi mali bali tafuta kuwaiga na kuwafuata. Huu ndio wivu unaofaa. Wakati huo huo epuka kuwadharau watu ambao hawajafanikiwa kifedha kama wewe.

## **14 . EPUKA KUFANYA KAZI BILA KUPUMZIKA**

Matajiri wengi huwa hawapumziki. Wanapofanikiwa kumiliki miradi zaidi ya mmoja hujisahau sana na kujikuta wakiwa na kazi nydingi (busy) kila siku. Hakikisha kuwa unapata siku moja kila wiki upumzike kabisa. Pumzika siku nzima kuanzia asubuhi hadi jioni. Hata kama kazi zako ni lazima zitoe huduma kwa masaa yote 24 ya siku na siku zote 7 za wiki, hakikisha unapata angalau siku moja kwa wiki. Kama huwezi kufunga siku hiyo, ni vyema ukawaachia wasaidizi wako wakafanya kazi siku hiyo na wewe uweze kupumzika kabisa.

Wataalam wa afya wanashauri pia kwamba ni vema kila mwaka mtu awe na mwezi mmoja mzima wa kupumzika. Pumzika mwezi mzima kabisa kwa maana ya wiki nne bila kwenda kazini. Waweza kwenda kutalii mbuga za wanyama, waweza kwenda nchi za nje wewe na mkeo au mumeo ukapumzike huko kwa mwezi mzima. Kama ni mwisho wa mwaka au katikati ya mwaka au mwezi wowote ni vyema ukachagua mwezi mmoja ambaao utakuwa unapumzika kabisa. Ukifanya hivyo, utaishi miaka mingi sana. Utafurahia utajiri wako. Utaepuka misongo ya mawazo. Utaepusha uchovu wa mwili (body fatigue). Utajiepusha na hatari ya akili kugota kufanya kazi kwa sababu ya kazi nydingi za bila kupumzika.

## **15 . EPUKA SIASA ZISIZO NA TIJA**

Kuna watu wanadhani kwamba kwenye siasa kuna pesa nydingi. Wanadhania hivyo baada ya kuwaona baadhi ya watu walioingia kwenye siasa wakiwa wamebadilika kabisa kifedha. Hata hivyo, mimi nawashauri wafanyabiashara wote wanaomiliki miradi yao inayowapa pesa kwa mamilioni, wasijaribu kujilingiza kwenye siasa uchwara kama alivyozita Bwana Rostam Azizi alipotakiwa kuijuzulu mwaka 2012 kwa hoja za ufisadi alioshutumiwa kujihusisha nao. Wakati anatangaza kuijuzulu alisema aliamua kuijuzulu kwa sababu ya siasa uchwara zilizokuwepo kwenye chama chake. Hata mimi naziita siasa uchwara.

Hii ni kwa sababu watu wanaoingia kwenye siasa Tanzania wengi wao waliingia wakidhani kwamba watamaliza umaskini wao na wa familia zao.

Lakini ukweli ni kwamba ukijiingiza kwenye siasa uchwara za Tanzania, utajikuta unahatarisha miradi yako yote uliyonayo. Sina maana kwamba wale wenye nia thabiti ya kulitumikia taifa hili wasiingie kwenye siasa, la hasha; nina maana kwamba usiingie kwenye siasa ambazo zitahatarisha biashara zako. Siasa zenye kuhtarisha miradi yako ni pamoja na siasa ambazo wewe mwenyewe unalazimika kutumia fedha zako kutetea kitu unachogombea ama kwa kuwapa wapiga kura, Mawakala, wapambe, na wengineo unaodhani watakuwezesha kushinda uchaguzi. Hizi ni siasa uchwara kama alivyozibatiza jina ndugu Rostam Azizi aliywahi kuwa Mbunge wa Igunga mkoani Tabora. Hakika zitakufilisi kabisa. Epuaka nazo kabisa.

Siasa nzuri ni zile ambazo hazihitaji wewe utumie pesa yako kuwahonga wapiga kura na wapambe ili upate ushindi unaoutaka. Siasa safi ni zile ambazo hulazimishwi kutoa matambiko na kafara za watu au wanyama ili upate kinga na ushindi. Siasa safi ni zile ambazo watu wanakuchagua wewe bila kujali umewapa nini kwanza ili uwawakilishe panapohusika.

## 16 . **EPUKA KUWEKEZA KWA WATU WASIOKUFAA**

Ukitaka uendelee kuwa bilionea maisha yako yote, epuka kuwekeza nguvu na mali zako kwa watu wasiofaa au watu wenye gharama nafuu (cheap people). Watalaam wa maswala ya fedha wanasema usitarajie uaminifu kwa watu rahisi (Do not expect honest from cheap people). Watu wasiofaa au rahisi ni pamoja na wapenzi, marafiki, ndugu jamaa na wanasiasa uchwara wanaotaka kuchuma fedha zako bila hata aibu. Wao wanataka wavune wasichopanda. Usiwaamini sana wala kuwatumanini hadi kuwakabidhi majukumu au mali zako. Mara nyingi watakuangusha kwenye kazi zako. Wengi wao wanataka wachume mali zako ikiwezekana mpaka utakaposema kwamba umefilisika ndipo watakoma kuja kwako. Wanataka uwalipie gharama za kila kitu. Epuka kuwekeza fedha zako kwa wapenzi wako. Punguza wapenzi kabisa kama huwezi kujitoa kwenye mtandao. Lakini kama unaweza kujinasua kwenye mtandao wa wapenzi ukabaki na mpenzi mmoja tu, hapo utakuwa umejiepusha na uwezekano wa kafilisika mapema.

## **17 . EPUKA KUWA NA WOGA CHINI YA JUA**

Kuna watu wenyewe woga kwa kila jambo jipya. Ukihakuwa tajiri bilonea usiogope kuthubutu kufanya jambo jipya au mradi mpya. Epuka kuogopa watu wasioweza kuua roho yako. Muogope Mungu tu awezaye kuua mwili na roho yako. Hapa duniani chini ya Jua hili usiwe mwoga. Unaogopa uchawi na wachawi, unaogopa matukio, acha tabia hiyo. Uwe na moyo wa ushujaa na Mungu atakuwa na wewe.

Woga huleta hofu. Ukianza kuwa na woga kuhusu majirani zako au wafanyabiashara wenzako, utakuwa ni mwanzo wako wa kuelekea kushindwa maishani mwako. Ukihsafanikiwa kifedha, hakikisha kwamba huwi mwoga kwa maswala ambayo hayana maana. Kuogopa wachawi au washirikina haina maana kwako. Hauna sababu ya kuanza kujihusisha na ushirikina kwa hofu ya kwamba utafilisika au kukosa wateja wa huduma au biashara yako. Hofu na woga vitakufanya ushindwe kuwaza na kusonga mbele. Badala ya kusonga mbele utajikuta unarudi nyuma kuwatafuta wachawi wakuzindikie miradi yako na ndio utakuwa mwanzo wa mali zako kuanza kuelekea kwa wachawi na wapiga ramli. Woga ni adui wa maendeleo yako. Epuka sana roho ya woga hakika utaona matokeo makubwa.

## **18 . EPUKA KUTAFUTA UTAJIRI WA HARAKA**

Kama umenunua kitabu hiki kwa matumaini ya kupata utajiri wa haraka, umekosea sana. Ukweli ni kwamba kitabu hiki siyo cha watu wanaotaka utajiri wa haraka haraka kama vile kucheza bahati nasibu. Kitabu hiki kinawalenga watu wenyewe ari ya kazi wasiokuwa na kasumba au fikra za kutaka kupata utajiri wa haraka haraka tena kwa njia za mkato. Kitabu hiki hakiwahuusu watu wanaodhani kwamba bila kumwaga damu za watu wasio na hatia hawawezi kupata utajiri mkubwa.

Kutokana na ukweli kwamba watu wengi wanapenda utajiri wa haraka haraka, makampuni mengi yamekuwa yakianzisha mashindano mengi ya bahati nasibu. Pamoja na makampuni mengi kuendesha bahati nasibu nyingi, bado wanaocheza bahati nasibu hizo hawajaweza kutajirika. Ukweli ni kwamba kampuni zinazoendesha bahati nasibu hizo ndizo huzidi kuwa

tajiri zaidi. Kwa mfano, kuna michezo ya bahati nasibu yenyeye kuonekana kuwa inalipa pesa nyingi sana. Kwamba ukishiriki tu utashinda na utapata milioni 100 au zaidi. Hebu kwa mfano tazama kampuni moja ya simu inaendesha michezo wa bahati nasibu na kila mtu anayeshiriki kama ni kwa kutuma ujumbe (sms) analipa Tshs 350 tu kwa kila ujumbe wa kushiriki. Tufanye kwamba kama kampuni ya simu ina wateja wapatao 1,000,000 labda wateja wapatao 200,000 watashiriki kwa wiki. Ukifanya hesabu za haraka utagundua kwamba kampuni hiyo itakusanya kwa wiki Tshs  $350 \times 200,000 = 70,000,000$ . Kwa hiyo kampuni inaweza kuingiza Tshs 280,000,000 kwa mwezi kwa kuendesha michezo wa bahati nasibu tu. Kama bahati nasibu itakuwa ya miezi 3; kampuni hiyo ya simu itakuwa na uwezo wa kuingiza zaidi ya Tshs 840,000,000 kwa kipindi hicho. Lakini katika pesa zote hizo, watatoa Tshs 100,000,000 tu kwa mshindi mmoja. Ndiyo maana unashauriwa kuepuka kuwatajirisha wachezesha bahati nasibu. Ukishakuwa tajiri epuka kabisa kujihusisha na miradi inayosemekana kwamba inalipa haraka. Epuka kufanya biashara ya upatu au bahati nasibu zenyeye kuonekana kwa macho kuwa zinalipa pesa harakaharaka.

Mtu akikwambia kuna biashara au kazi fulani anataka mkaifanye na kwamba mkiweza kuifanya tu kwa siku hiyo moja au mbili mtaingiza mamilioni au mabilioni ya pesa, tulia kwanza kisha rudi nyuma uachane naye. Hiyo siyo biashara itakuwa ni wizi na utapeli kama siyo ujangili wa maliasili za taifa basi itakuwa ni utapeli wa kawaida tu au kuuza dawa za kulevyta. Epuka sana miradi na biashara za kutabiri mapato makubwa na ya haraka.

## 19 . EPUKA KUSEMA MABAYA YA WENGINE

Ukiisha kupata utajiri mkubwa epuka mtego wa kuwasema vibaya watu wengine. Kama wewe unawaona hawafanyi vizuri kama wewe siyo busara kuanza kuwasema kwenye vyombo vya habari, kwenye mikisanyiko au kwenye mabaa. Epuka kuwasema watu vibaya. Badala ya kusema mabaya yao ni vema ukakumbuka mema yao na kuyasema badala ya kukaa muda mwiningi ukiwasema mabaya yao. Epuka kushupalia jambo Fulani ambalo limefanywa au kusemwa na watu wengine juu yako au biashara yako. Usiwaseme vibaya wanasiasa, wahubiri wa dini, viongozi wa nchi, wanawake, wanaume, vijana, watoto na watu wengine katika

jamii. Wewe tazama kwa makini hoja zao na kisha uzungumze hoja zako zaidi. Usiwaseme watu vibaya kwani nao watakusema vibaya na mwisho wa yote utafilisika mali zako zote.

## **20 . EPUKA KUJIONA UNAJUA SANA**

Matajiri wengi waliokwishafanikiwa hudhani kwamba wanajua sana kiasi kwamba wanakuwa hawashauriki tena. Watu wengi wakishakuwa Matajiri hufanya maamuzi mazito tena mengi bila hata kuwashirikisha wanafamilia wenzao. Epuka kuwa katika kundi lisilopenda kuwasikiliza wengine. Jifunze kusikiliza wengine. Jifunze kuwa mtu anayetamani kupata maarifa kwa watu wengine. Jifunze kuwa mkimya kila mara inapowezekana. Hii ndiyo siri ya matajiri. Usitake kuteka kusanyiko lolote unalokuwamo kwa sababu tu wewe unaona kwamba unawazidi mali na utajiri. Hata kama wewe ni tajiri sana kuwapita wengi katika mtaa wako au jamii yako, siyo vema ukawa ndiyo mwongeaji sana asiyekuwa na mpinzani wala mbadala. Jifunze kuwa mnyenyekevu hata kama umeshakuwa bilionea.

## **21 . EPUKA KUJIHUKUMU**

Acha kujihukumu kwamba huwezi kuwa tajiri mkubwa katika kijiji, mji au mtaa unaoishi. Hata kama wewe una ulemavu wowote usijihukumu. Kama una upungufu wowote unaodhani unakukosesha uwezo wa kufanya jambo fulani, acha kujihukumu kwamba huwezi. Sahau makosa yaliyofanywa na babu au bibi yako. Hata kama wazazi wako walikuwa maskini sana, wewe hupaswi kuanza kujihukumu kwamba huwezi kutajirika na kuwa bilionea. Kama umeshaanza kuwa tajiri kwa kiwango fulani hupaswi kujiona kwamba hawawezi kuwfikia watu fulani waliokwishatajirika sana. Usijihukumu kwa sababu ya jinsia yako au kwa sababu ya kiwango chako cha elimu. Epuka kujihukumu kwa sababu yoyote ile iwe ya kihistoria, kielimu, kabila lako, familia au ukoo wako, taifa lako, au rangi yako. Wewe usijihukumu hata kidogo kwa sababu yoyote. Endelea kusaka utajiri mpaka uwe bilionea bila kujali historia yako au ulikotokea kihistoria.

## **22 . EPUKA KUONGEA SANA**

Watu wengi hushindwa kusonga mbele kifedha kwa sababu wanaongea sana. Wanasema mambo mengi na mipango mingi bila utekelezaji. Watu wengi hukaa vikao vingi kupanga mipango mingi, mikakati mingi, na mambo mengi, lakini wanayoyatekeleza yanakuwa machache na hatimaye kuzidi kudidimia kifedha. Ukitaka kufanikiwa kifedha epuka kuongea sana na watu kuhusu mipango yako au mawazo yako. Ukitaka kufanikia usimwambie kila mtu kila kitu unachotaka kufanya. Usipende kumweleza kila mtu kuhusu nini unawaza kufanya au nini unapanga kufanya mwaka huu au mwaka ujao. Jitahidi sana kuwa na mipango mingi au mawazo mengi ya mambo ya kufanya lakini ujitahidi sana kutokumwambia kila mtu. Jitahidi kuwa na Maneno machache lakini vitendo vingi ndivyo viongee na watu. Acha matendo yako ndiyo yaongee. Jitahidi kuonekana ukifanya mambo yanayoeneekana kuliko kuongea maswala mengi unayoyapanga kufanya huku kukiwa hakuna hata moja linaloonekana umefanya.

## **23 . EPUKA KUDHARAU WAZO LA MTU**

Jifunze kuheshimu wazo la mtu bila kujali huyo mtu ana kiwango gani cha pesa au elimu. Kwa mfano, mke wako au mume wako hata kama hakusoma shule, hata kama hawezi kuandika jina lake wewe usimdhara kamwe. Wapo watu wenye busara kubwa hata kama hawajapata utajiri kama ulio nao. Jifunze kuishi maisha ya unyenyekevu na kuishi maisha ya kawaida unapokuwa na watu wa kawaida. Hata kama ni mtu usiyemjua, hata akiwa mgeni kwako, akikupa wazo zuri usilidharau. Epuka kujikweza mbele za watu kwasababu watakushusha. Acha watu wenyewe wakukweze badala ya wewe kujikweza.

## **24 . EPUKA UVIVU WA KUFIKIRI**

Watu wengi wakishapata utajiri hugeuka kuwa wavivu. Wanakuwa wavivu wa kufikiri nje ya sanduku yaani nje ya mazoea yao. Wanakuwa wavivu siyo wa kutembea kwa miguu tu au kufanya mazoezi ya viungo bali hata kuwaza na kufikiri wanakuwa wavivu sana au tuseme wanakuwa wazito. Uvivu wa kufikiri ninaousema hapa ni ule wa kutowaza tena jambo jipya.

Kutokuwaza jinsi ya kupanua miradi yako kutoka hatua moja kwenda nyingine. Uvivu wa kutofikiri jinsi ya kuwaendeleza wafanyakazi wako, nchi yako, mkoa wako au kijiji chako, nk.

Tajiri makini lazima ajitahidi kuwa na muda wa kuwaza kwa kina kuhusu mada na maswala mbalimbali siyo yahusuyo biashara na miradi yake tu bali hata kuhusu watu wake na nchi yake. Tajiri makini siyo yule anayependa kwenda kwenye baa kila siku kunywa pombe na kuwanunulia rafiki zake pombe, bali ni yule anayetafakari kila siku njia bora za kukuza mtaji wake kutoka milioni kumi kwenda bilioni kumi au kutoka bilioni kumi kwenda bilioni mia moja. Tajiri mtembeleaji wa baa kila siku, ukweli ni kuwa hatakuwa na muda wala siku ya kuwaza kwa kina kuhusu miradi au biashara zake. Tajiri kama huyo atajikuta hasongi mbele bali atazidi kurudi nyuma. Mpenzi msomaji, kila siku unapaswa kuwaza jambo jipya hasa kuhusu maendeleo ya miradi na biashara zako. Kaa na watu wanaofikiri mambo kwa mtazamo chanya. Epuka kukaa sana na watu wasiowaza kwa upembuzi yakinifu wa mambo. Epuka kukaa sana na watu wanaopiga soga tu bila kuwaza maendeleo.

## 25 . EPUKA MAJUNGU

Tajiri makini hafanyi kazi zake kwa kufuata majungu au taarifa za uongo kutoka kwa washindani wake au wafanyakazi wake. Kumbuka kuwa ukishakuwa tajiri utaletewa majungu mengi sana. Majungu kibao yataletwa na wafanyakazi uliowaajiri, majungu yataletwa na watu wa nje ya kampuni zako au miradi yako, majungu yataletwa na wanasiasa, majungu yataletwa na washindani wako kibiashara, majungu yataletwa na wapenzi wako, nk. Njia pekee ya kuepuka kupokea majungu na kujikuta ukifanya maamuzi ya hovsky, ni kufanya utafiti wa jambo lolote kabla ya kufanya uamuzi. Watalaam wanasema kwamba kama hujafanya utafiti huna haki ya kusema jambo au usifanye uamuzi wowote (No research mo right to speak). Kumbuka utaletewa majungu kuhusu mke au mume wako kwamba anajihuisha kimpenzi na mtu Fulani, utaletewa majungu kuhusu miradi yako kwamba wafanyakazi wako wanaiba sana, nk. Wewe fanya utafiti wa kina kwanza ndipo ufanye uamuzi wa haki. Unapoletewa majungu yoyote,

kabla ya kutafiti kwa kina na ukajiridhisha huna haki ya kusema chochote. Nyamaza tu. Usifanye maamuzi yenyenye kusimamia majungu kama unataka miradi yako ikue na uweze kuendelea kuwa bilionea.

## 26 . USIOGOPE KUSHINDWA

Kama una wazo la kujenga jengo la ghorofa 3, 5 au 10 usiogope gharama wala kuwaza kushindwa. Wewe songa mbele na wazo lako kwani hata hao walioweza kujenga majengo ya maghorofa zaidi ya 10 nao ni watu kama wewe. Usiogope kuwaza au kuweka mipango mikubwa mbele yako. Waza zaidi maswala makubwa ya maendeleo yako ili hata kama hutaweza, basi waseme kwamba ulithubutu.

Je, Unawaza kumiliki kituo cha Televisheni au Radio? Usiogope hata kidogo, wewe anza mchakato!! Kama unawaza kuwa na kampuni ya mabasi makubwa ya abiria usiogope kushindwa. Songa mbele kwani changamoto utakazokutana nazo zinapaswa kuwa somo lako la kukuwezesha wewe kupata ushindi zaidi kwenye miradi yako.

## 26. EPUKA KUAHIRISHA JAMBO.

Kuna watu ni mabingwa sana wa kuwaza au kusema kufanya jambo fulani kesho, lakini kamwe hawatendi wanaishia kupanga na kuahirisha mada waliyokuwa wanayo. Epuka kupanga na kuahirisha jambo ulilokuwa umepanga kila mara. Ukitaka uzidi kuwa milionea hadi kuwa bilionea acha utamaduni wa kuahirisha kutekeleza jambo ulilokuwa umepanga. Usiwe na tabia ya kusema sana bali fanya jambo ambalo ikifika kesho wengine hawataweza kulifanya. Fanya jambo ambalo ikifika kesho wewe utakuwa umeshalifanya jana wakati wengine wanahangaika kulifanya.

## 27. USIOGOPE KUROGWA

Kuna watu wanaodhania kwamba huwezi kuwa tajiri mpaka utambikie makaburini, uchanje sana, utoe kafara ya wanyama kwa waganga wa kienyeji. Ukweli ni kwamba hiyo ni imani tu. Kama inasaidia kufanya mtu aweze kuwa bilionea mimi sina ushahidi. Lakini hoja yangu hapa ni kwamba kama unapenda uendelee kuwa bilionea maishani mwako usiwaogope

wachawi wala wanajimu. Uchawi huwa haumshiki mtu asiyekuwa na hatia hata kidogo. Huwezi kurogwa na mtu kama hujamkosea jambo lolote. Kama hujaanza kujihusisha na uchawi maishani mwako huwezi kurogwa kamwe. Wachawi hawana lolote watakalolifanya kukudhuru wewe usipojihuhsisha kwenye maswala hayo ya ushirikina. Kama unataka kujiingiza kwenye sekta hiyo ya uganga na ushirikina ingia ukijua kwamba utauawa mapema na washirikina wenzako. Chini ya Jua ukiwa mwoga sana, kile unachoogopa ndicho kitakachokuondoa duniani.

## **27 . USIFANYE JAMBO JIPYA BILA UTAFITI**

Mjasiriamali makini hufanya utafiti wa jambo jipya au ili apate mawazo mapya kwenye biashara zake na miradi yake lazima afanye uchunguzi na utafiti. Usifanye mradi mpya bila kuufanya utafiti. Epuka kutumbukiza pesa zako kwenye miradi ambayo hujafanya utafiti. Matajiri wengi hujikuta wakiingia hasara kubwa kwa kufanya miradi au biashara ambazo hawakufanya utafiti hata mdogo. Ni vyema ukajitafutia taarifa sahihi kabla ya kutekeleza azimio lolote la kuwekeza pesa.

## **28 . EPUKA KUTOSHEKA HARAKA**

Kujisikia moyoni mwako kwamba umeridhika na mradi fulani kwa sababu tu mradi huo unatoa pesa nyingi ni mwanzo wa kuanza safari ya kurudi nyuma kiuchumi. Tajiri makini ni yule anayezidi kubuni jambo jipya na kuibua miradi mipyi inayomwingizia pesa. Safari moja huanzisha safari nyingine, hivyo mradi mmoja unapaswa kuanzisha mradi mwiningine. Kutosheka kunakosemwa hapa ni kule kubweteka na hali fulani ya kipato na kushindwa kuwaza na kutafakari jambo jipya. Hata kama ungekuwa umeshafikisha uwezo wa kupata pato la shilling bilioni moja (1,000,000,000) kwa mwezi usibweteke hata kidogo. Siku utakapobweteka tu ndipo bilioni yako moja itakapoanza kupungua. Kila siku unapohisi kutosheka kimapato ndivyo kurudi nyuma kifedha kunavyokujia kila siku.

## **29 . EPUKA KUSUKUMWA NA WAPAMBE**

Wapo matajiri wengi ambao hufanya maamuzi kwa kuzingatia kusukumwa na ndugu zake au serikali au wapambe wake. Jiepushe na misukumo

---

isiyokuwa na tija kwenye miradi yako. Kama swala siyo la kisheria usikubali kuburuzwa na matajiri wenzio kujihusisha na maswala yasiyoleta tija kwenye biashara na miradi yako. Kama uko kwenye umoja wa wafanyabiashara au wa sekta fulani inayohusu miradi yako na wakapanga kufanya mambo ambayo wewe huoni kama yataleta tija kwako na nchi yako, jitahidi kuwakwepa na usikubali kufanya maamuzi kwa kusukumwa na watu au matajiri wenzako. Usifanye maamuzi ukiwa hujachunguza madhara ya maamuzi yako. Usifanye uamuzi ukiwa katika hali ya jazba wala hasira.

### **30 . USIWAZE MABAYA TU**

Kuna watu wanawaza upande wa mambo mabaya tu. Huwezi ukawakuta wana mtazamo chanya kuhusu maswala kadhaa ya jamii au serikali. Wao ni kupinga tu kila kitu na kila jambo. Jitahidi kuwa na utamaduni wa kuwaza upande wa mema (chanya) dhidi maswala hasi ndani ya jamii yako, kanisa lako, msikiti wako, hekalu lako, serikali yako, viongozi wako na wengine hata kama umewapita sana viwango vyta pesa. Hata kama ukiwa bilionea na unacho kila kitu, siyo vema kuwawazia mabaya wale ambao hawajafanikiwa kifedha kama wewe.

### **31 . EPUKA KUKWEPA KULIPA KODI**

Ni aibu kwa tajiri kukwepa kulipa kodi. Ni laana kwako na taifa lote. Kama unataka uwe raia mwema na mwenye heshima katika taifa lako, hakikisha unalipa kodi kutoka kwenye mapato yako. Unapaswa kukumbuka kwamba kutolipa kodi ya mapato serikalini ni laana kwako na taifa lako lote. Kutolipa kodi ya ongezeko la thamani (yaani VAT) ni kuwaibia wananchi wanaolipia bidhaa hizo na huku wewe ukishindwa Kuwasilisha kodi hiyo ya VAT kwenye mamlaka ya mapato nchini kama inavyotakiwa. Ni laana sana kwako kujaribu kukwepa kulipa kodi ya VAT. Inapaswa kuwa mwiko sana kwako kama bilionea tajiri kukwepa kodi. Ukiona mtu anakwepa kulipa kodi ujue huyo siyo mwenzako. Naam, yawezekana akawa siyo raia wa nchi hii. Raia wazalendo wa nchi hakika hulipa kodi. Wasio wazalendo hawalipi kodi yoyote kwa mamlaka ya nchi.

## **32 . EPUKA KWANYANYAPAA WATU MASKINI**

Ukishakuwa bilionea, hakikisha kwamba unajipatia marafiki kutoka kwenye kundi la watu maskini kama vile walemvavu, wajane, yatima, na makundi yaliyoko mbali na huduma za jamii zinazohudumiwa na serikali. Toa misaada kwa wenyewe umasikini na mahitaji maalum. Wasaidie bila masharti yoyote. Ukufanya hivyo, hakika utaendelea kuwa bilionea wa Tanzania ambaye hata ukifariki dunia sadaka hizo hazitafutika kwenye kumbukumbu za mioyo ya watanzania.

## **SURA YA NNE**

### **MBINU ZA KUPATA MTAJI**

Ukiongea na watanzania wengi bara na visiwani watakwambia kwamba tatizo lao kubwa ni mtaji. Utakutana na watu wengi wakisema kwamba siku watakapopata mtaji ndipo watafanya hiki au kile kitakachowainua kiuchumi. Kila kona watu wanalia kwamba hawana mitaji. Serikali kuu na serikali za mitaa nazo zinalia kwamba bajeti haitoshi. Wazazi nao kama wakuu wa familia wanalia hivyo hivyo kwamba hawana mtaji wala fedha za kutosha mahitaji yao. Ukichunguza sana utagundua nchi nzima watu wanalia kwamba watu wake hawana mtaji. Je, ni kweli tuna tatizo la mitaji kwa kiasi hicho? Katika sura hii nitakufafanulia mbinu kadhaa unazoweza kutumia ili kupata mtaji wa mradi unaoutaka kufanya. Kama utafuata maelekezo ndani ya sura hii ya kitabu hiki, hakika utapata mbinu nyngi zitakazokupa mtaji wa kiasi chochote unachohitaji na utafanya mradi unaoutaka na hakika hautakuwa masikini tena:

#### **Mbinu Na. 01: Kujiwekea akiba ya Malengo**

Kama kuna mradi wowote ulioelezwa katika kitabu hiki uliokuvutia na ungependa uanze kufanya ili uweze kupata utajiri mkubwa, ni lazima kuanzia sasa uanze kuweka akiba ya fedha kila siku au kila mwezi kutoka kwenye kazi unayoifanya kwa sasa. Kwa mfano kama wewe ni mwalimu au Muuguzi au mfanyakazi wa kuajiriwa kwenye sekta yoyote na unalipwa mshahara, kama wewe unafanya biashara ndogo au ukubwa; ni vyema sasa ukaanza kuweka akiba ya malengo. Weka akiba kila mara kwa lengo moja tu. Lengo lako kuu liwe kupata mtaji. Ustumie akiba hiyo kwa jambo lingine lolote hata kama lingekwa la dharura namna gani.

Kwa mfano kama unalenga kupata mtaji wa Tshs 2,000,000 ili uanze mradi wa kupanda miti, au kufuga kuku, au kilimo cha Matikitimaji, au chochote unaweza kuanza kuweka akiba ya Tshs 100,000 kila mwezi. Kama utaweka akiba kama hiyo kila mwezi ni dhahiri kwamba baada ya miezi 20 tu utakuwa umeshapata mtaji huo unaotaka. Mfano mwengine ni kama wewe una mshahara kamili (net pay) wa Tshs 1,200,000 kila mwezi, unaweza

kuamua kuweka Tshs 450,000 kila mwezi. Baada ya Mwaka mmoja utakuwa umekusanya Tshs 450,000 x 12 = Tshs 5,400,000.00. Ukfanya hivyo kwa miaka mitatu utakuwa umekusanya 16,200,000.00. Kwa miaka sita (6) utakuwa umekusanya karibu Tshs 32,400,000.00. Je, una habari kwamba ukiwa na mtaji wa Tshs 32,400,000 waweza kufanya jambo au mradi mkubwa ulilokusudia? Unaweza kuweka akiba hiyo kwenye akaunti maalumu za mabenki au ukaweka akiba hiyo kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii kama vile LAPF, NSSF, PSPF, PPF na GEPF ili kila mwezi pesa yako iongezeke kwa riba inayoongezwa kila mwaka na mifuko hiyo.

Ukitaka kuweka akiba yako kwenye benki yoyote nchini ni vyema ukazitembelea benki hizo angalau tatu kabla ya kuamua ni benki gani uweke pesa yako. Kumbuka kuwa benki zinatofautiana kwa riba wanazotoa. Endapo utaamua kuweka akiba yako ya malengo kwenye mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama ilivyotajwa awali pesa zako zitakuwa na faida zaidi kwani kila mwaka mifuko hiyo huongeza faida ya asilimia zaidi ya tano kila mwaka. Faida nyingine pia ni kwamba huruhusiwi kuzitoa peza zako wakati wowote kama ilivyo kwenye mabenki. Hii itakusaidia sana kuweza kufikia lengo lako zaidi.

Kwa mfano kama umeweka lengo la kujenga nyumba baada ya miaka mitano, itakuwa rahisi kufikia lengo lako kama utajiunga na mifuko ya pensheni hiyo na Kuweka akiba yako kila mwezi. Kama utalenga kufikisha Tshs 10,000,000 au zaidi, itakuwa rahisi zaidi kama utaweka akiba yako kwenye mifuko hiyo ya hifadhi ya jamii kuliko kwenye mabenki.

## **Mbinu Na. 02: Kuugawanya Mshahara Vipande Vipande**

Chanzo kingine cha mtaji ni kuhakikisha kwamba kama una mradi mmoja unaozalisha faida hakikisha kwamba faida hiyo au kipato hicho unakigawa katika matumizi mawili; moja matumizi ya kawaida ya familia yako au wewe mwenyewe na pili elekeza kwenye mradi mwингine. Kwa mfano kama unapata kipato cha Tshs 1,000,000 kwa mwezi, waweza kuanzisha mradi mwингine kwa kugawa pesa hiyo kwa asilimia 40% ya pesa hiyo kuelekea kwenye mradi wako mpya na 60% ya kipato hicho ikawa ndiyo matumizi ya familia yako. Hii ina maana kwamba shilingi 600,000 zitumike kwa mahitaji

nyumbani na shiling 400,000 zielelekezwe kwenye mradi wako wa pili. Yawezekana unataka kufanya mradi wa ujenzi wa nyumba ya kupangisha, hapo ni vema mgawanyo wako huo kila mwezi shilingi 400,000 ukazitumia kwenye kufyatua tofari, Kununua mbao, mabati, milango, misumari nk, mpaka umalize kujenga nyumba yako ya vyumba sita (6 room house). Kama unataka kujenga nyumba ya vyumba 6 itahitaji takribani matofari 2000. Ukiwa na Tshs 400,000 utaweza kufyatua angalau tofari 500 za block kwa kutumia saruji (cement) kila mwezi. Kama kila mfuko wa saruji utatoo tofari 40 tu ambazo ni kiwango cha ubora unaokubalika, utahitaji mifuko ya saruji kama 13 tu. Kwa bei ya Tshs 20,000 kila mfuko wa saruji utahitaji Tshs 260,000 kununua mifuko ya saruji ambapo Tshs 140,000 iliyobakia utanunua mchanga na kumlipa fundi wa kufyatua tofari hizo na mengineyo. Kama kila mwezi utafyatua tofari 500 ni dhahiri kwamba baada ya miezi 4 tu utakuwa umetimiza tofari 2000 ambazo zinatosha kuanza ujenzi. Ili ufanye vyema kwenye mradi kama huu ni vyema mwezi unaofuata ukaanza ujenzi wa boma la nyumba hiyo. Kila mwezi tumia pesa hiyo Tshs 400,000 kujenga nyumba yako mpaka boma la nyumba limalizike kwanza. Baada ya boma kumalizika ndipo sasa unaweza kuanza Kununua vifaa muhimu vya kupaua nyumba yako kama vile mabati, mbao za kENCHI, milango, na vifaa vyote muhimu kwa ujenzi. Vikishakamilika vyote hapo wewe ni kumtafuta fundi wako aje kupandisha mabati juu ya nyumba, aweke milango na madirisha na nyumba inakuwa inaelekea kukamilika.

Ukijenga nyumba kwa kutumia mbinu hii, baada ya miezi 30 tu unaweza kukamilisha ujenzi wa nyumba yako ambapo ukijumlisha gharama zote utakuta kwamba umetumia zaidi ya Tshs 12,000,000. Lakini kama utasubiri kwamba ukakope kwanza kiasi hicho cha Tshs 12,000,000 ndipo ujenge nyumba yako, au uanze biashara, hautazipata pesa hizo kamwe na huenda ukazipata kwa riba kubwa kutoka kwenye taasisi za kutoa mikopo. Tenga shilingi 200,000; Tshs300,000; Tshs 400,000 au Tshs 500,000 kila mwezi hadi pale utakapofikia lengo lako. Usikate tama kwa namna yoyote. Mtegemee Mungu wako kwa Imani yako. Fanya upande wako naye Mungu atakusaidia upande wake.

## **Mbinu Na. 03: Kuomba Mkopo kutoka Benki**

Kama unahitaji mtaji wa kufanya mradi wowote unaweza kuchukua mkopo kutoka benki hata kama huna hati ya kiwanja. Benki ya Posta Tanzania (TPB) inatoa mikopo kwa wajasiriamali kuanzia Tshs 300,000 hadi Tshs 5,000,000.00. Masharti yao ni kwamba lazima uwe unafanya mradi wako au biashara yako angalau kwa mwaka mmoja au zaidi. Sharti pia uwe unataka kupanua mtaji au kuendeleza mradi wako zaidi. Benki nyingine zilizopo hapa Tanzania ambazo pia zinatoa mikopo kwa wajasiriamali ni: CRDB, NMB, NBC, AZANIA, TWIGA, EXIM BANK, n.k zote hizo zinatoa mikopo kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wakubwa kwa wadogo. Kama mjasiriamali anayo nyumba na hati ya kiwanja au nyumba anaweza kukopeshwa na benki hizo kiasi kikubwa kabisa kulingana na thamani ya dhamana ya mali zake. Kwa mfano kama mjasiliamali ana mali isiyohamishika yenye thamani ya Tshs 200,000,000 (milioni mia mbili) benki hizo zinaweza kabisa kutoa mkopo kama huo. Benki inaweza kukupa mkopo wa shilingi milioni mia mbili bila wasiwasi ili mradi uwe unafanya miradi yenye tija kwako na kwa benki husika. Kama wewe unacho kiwanja nyumba na hati halali kabisa, nenda benki yoyote hapa Tanzania. Nenda ukakopeshwe pesa yoyote unayotaka. Nenda usiogope. Nenda ukamwone meneja wa tawi lolote la benki. Nenda ukamweleze unataka kufanya nini na unatarajia kupata faida kiasi gani? Nenda wakupe mwongozo wa jinsi ya kuandika mikakati ya biashara yako (business plan) ili wakupe pesa. Unataka mtaji wa kiasi gani? Je, unataka mkopo wa milioni hamsini, milioni mia moja, milioni mia moja na hamsini au milioni mia mbili? Nenda benki yoyote sasa hivi, wanakusubiri wakupe pesa unazotaka.

## **Mbinu Na. 04: Kumwomba Mzazi Akupe Mtaji**

Kama wewe ni kijana mwenye wazazi au walezi ni wajibu wao kuhakikisha wanakupa mtaji. Ni wajibu wa wazazi kuwapa mitaji ya miradi au biashara watoto wao. Kama wewe ni kijana uliyemaliza elimu ya chuo, au sekondari usiogope kumwomba mzazi wako akupe mtaji. Unatakiwa umweleze mzazi wako kwamba unataka kufanya mradi gani na ungependa akupe mtaji kiasi gani. Panga mikakati yako ikiwezekana uiandike kwenye kalatasi na umshirikishe mzazi au mlezi wako. Mweleze jinsi utakavyoendesha

---

mradi au biashara yako na jinsi utakavyopata faida na mwelekeo wako kiuchumi na kifedha endapo atakupa mtaji. Wapo vijana wenye wazazi wao ambao wanatarajia kulipwa kiinua mgongo kutoka mifuko ya pensheni ambapo mara nyingi wazee hao wanapostaafu hulipwa pesa nyingi sana kiasi kwamba kama wana vijana waliojipanga vyema wazazi hao hawatawanyima pesa ya mtaji. Kwa mfano, wewe ni kijana na unaye mzazi ambaye anatarajia kustaafu, ni vyema ukawa umeshaandika mpango mkakati (strategic plan) au mpango mzima wa biashara/mradi wako na umwoneshe mzazi wako ausome na auelewe ili mara tu anapopata kiinua mgongo aweze kukupatia mtaji wako. Kuna watu wanapostaafu hulipwa hadi Tshs 120,000,000, wengine hulipwa hadi Tshs 180,000,000 kutoka kwenye mifuko ya pensheni kama PPF, NSSF, LAPF au PSPF. Kama unaye mzazi anayekaribia kustaafu, ni vyema ukajiweka tayari ili upewe mtaji na mazazi wako au mlezi wako huyo. Kwa mfano kama unataka kufanya mradi wa thamani ya Tshs 15,000,000 nina uhakika kwamba mzazi wako huyo akistaafu hataacha kukupa mtaji kama huo mara anapostaafu kazi. Hakikisha kwamba wazo la mradi wako umelifanyia upembuzi na utafiti wa kutosha ili mara tu upatapo pesa hiyo uielekeze kwenye mradi huo ulioukusudia na siyo vinginevyo.

Hata kama wewe wazazi au walezi wako hawana kipato kikubwa, ni vyema tu ukaandika mchanganuo wa biashara yako au mradi wako na uandike kwenye kitabu au kalatasi ili kila mtu aweze kusoma mawazo yako na kama unataka akupe mtaji akupe akijua wazo lako ni lipi na litaleta faida gani kwako na kwake ye ye unayetaka akupe mtaji.

Unaweza ukapata mtaji pia kwa kusaidiwa na rafiki yako, ndugu yako, jirani yako ambaye tayari amekwishajikwamua kwa hatua kubwa kiuchumi na kifedha. Rafiki au nduguyo anaweza akakupa fedha kama mkopo au kama msaada tu au kwa maelewano yoyote kama ndugu na wewe ukapata mtaji wako. Unachotakiwa kumwonesha ndugu au rafiki yako ni uaminifu wako na uhakika wa kupiga hatua kubwa mara tu upatapo mtaji kutoka kwake. Mhakikishie tu kwamba akikupa pesa ya mradi unaoutaka hakika wewe utasonga mbele na kujiondona kwenye lindi la umaskini. Mzazi, nduguyo au rafiki yako anaweza kukupa mtaji endapo tu utaonekana kuwa umejipanga na unayo mawazo mazuri na yenye mwelekeo wa mafanikio mbele ya safari.

## **Mbinu Na. 05: Kufanya kazi yoyote ukilenga Kupata Mtaji**

Watanzania wengi kisaikolojia wanataka wafanye kazi zenyenye kuwapa ujiko. Kijana anataka aonekanae anafanya kazi kwenye mashirika makubwa zenyenye mishahara inayosemekana kuwa ni mikubwa. Ukiwaambia wafanye kazi fulani amabayo haionekani kuwa ni ya kifahari utaona kwamba wanarudi nyuma. Hawataki. Wasomi na wasiosoma wanataka kazi nzuri. Wanazunguka huku na kule wakitafuta kazi zenyenye mishahara mikubwa sana. Lakini kwa mtu mwenye kuishi kwa fikra pepu na kwa malengo ya kujikomboa kiuchumi atakuwa tayari kufanya kazi yoyote zenyenye malipo mazuri hata kama kazi hiyo haionekani kuwa ya kifahari sana. Sisemi kazi zenyenye kutweza utu wa mwanadamu, bali hoja yangu ni kuhusu kazi yoyote halali zenyenye kuweza kukupa pesa unazozitafuta na ukaweza kutoka hatua moja kwenda nyingine kiuchumi na kifedha. Kwa mfano, unaweza kufanya kazi kama vile; vibarua vya ujenzi wa nyumba au barabara, kazi za kilimo, kazi za kuajiriwa hata na mtu ambaye humpendi labda kwa sababu za imani yako au kabilalako, kazi za uvuvi ziwani au baharini, kazi za udreva, kazi za kufanya usafi, nk. Endapo kazi hiyo itakupa pesa ambazo zitawezza kukupatia mtaji unaoutafuta ni vyema ukaifanya bila hata chembe ya aibu. Usiwe na kasumba ya kuona aibu kufanya kazi fulani hata kama zinakupa kipato. Acha tabia za kuona aibu kwenye kazi. Kwa mfano kuna kazi unaweza kufanya kwa muda mfupi na ukapata pesa nyingi kwa mkupuo hadi Tshs 1,500,000.00 kwa mwezi au hata kwa wiki mbili kutegemeana na aina ya kazi yenye hasa za ufundi au ujenzi. Unaweza kufanya kibarua fulani na ukapata malipo makubwa hata Tshs 10,000,000 ndani ya mwezi mmoja kutegemeana na kazi yenye hasa za ufundi. Ukipata pesa kama hiyo jitahidi ufanye mradi mwingine sasa ambao unakuwa wa kudumu na kukuinua zaidi.

Hata kama ni kazi ya kuzibua vyoo vya watu mijini, kama inakupa pesa ya kutosha kujikwamua na kuanzisha biashara nyingine au mradi mwingine kama nilivyofafanua katika sura ya pili, ukiifanya hakika unaweza ukafika mbali sana. Kazi ya kuzibua vyoo, ni moja ya kazi ngumu sana lakini inalipa sana. Unaweza kuifanya kwa malengo tu ya kujipatia mtaji siyo kwa ajili ya kuzeeka nayo. Mtaji unaoupigania kutoka kwenye kazi ya kuzibua au

kusafisha vyoo vilivyojaa inapaswa iwe ya mpito ili kujitoa katika dimbwi la ufukara. Usiwe na kinyaa wala unyanyapaa kwa kazi yoyote yenye kipato halali. Kumbuka kwamba huwezi kusafisha choo au kuchota uchafu uliojaa kwenye choo kwa bei chini ya Tshs 100,000 kwa kila shimo moja la choo. Katika miji mikubwa kama Mwanza na Dar es salaam ambako vyoo hujaa sana mara kwa mara na watu hawana maeneo ya kujenga vyoo vipyaa kama ilivyo vijijini; uwezekano wa kupata wateja kila siku ni mkubwa sana. Kwa wiki unaweza kupata hata wateja 4 au zaidi. Kama utapata wateja 10 kwa mwezi na ukafanya kazi hiyo kwa miezi 10 tu utakuwa umeshapata zaidi ya Tshs 10,000,000 kwa miezi hiyo kumi. Je, utakosa mtaji wa kuanzisha mradi wako uupendao kutoka sura ya pili ya kitabu hiki? Unaweza ukafanya kazi ya kuajiriwa serikalini au sekta binafsi kwenye makampuni au mashirika ya kimataifa au ya watu binafsi. Kwa mfano waweza kukubali kuajiriwa kama mwalimu, muuguzi, daktari, mwandishi wa habari, afisa kilimo, afisa mifugo, afisa maendeleo ya jamii, nk. Unapaswa kukubali ajira hiyo kama swala la mpito tu. Usichukue ajira hiyo na kutaka iwe swala la ajira ya mpaka kufanya kazi hiyo kwa muda wa miaka 5 au 10 tu kwa lengo la kupata pesa za mtaji.

Kwa mfano kama kila mwezi utaweka kiasi cha Tshs 150,000 baada ya miezi 60 ambayo ni miaka mitano utakuwa umeshakusanya Tshs 9,000,000. Na kama mshahara wako ni mkubwa zaidi ya shilingi 1,000,000 kwa mwezi; unaweza Kuweka akiba ya shilingi hadi 300,000 kwa mwezi. Utaona kwamba kwa miaka 5 utakuwa umeweka akiba isiyopungua shilingi 9,000,000 ukiweka akiba ya Tshs 150,000 kila mwezi au shilingi 18,000,000 ukiweka akiba ya Tshs 300,000. Mtaji huu unaweza kukuwezesha kufanya mradi kama wa ufugaji ng'ombe wa maziwa, kilimo cha matunda, kuwa wakala wa kampuni za vinywaji baridi au vikali kama vile Coca Cola, Pepsi Cola, Azam Cola, TBL, nk. Unaweza kuanzisha mradi wowote kati ya miradi zaidi ya 60 iliyoorodheshwa katika kitabu hiki. Ni wewe tu kuamua kwamba sasa muda wa kuacha ajira umefika. Hii ni njia njema ya kupata mtaji bila kulazimika kukopa kutoka kwa mwajiri wako au kutoka benki, kutoka SACCOS au kutoka popote pale. Ukikusanya mtaji wa Tshs

9,000,000 ndani ya miaka mitano bila kukopa kutoka kwa mtu au taasisi unakuwa huru zaidi hata kuacha kazi ya ajira na kuanza kujiajiri. Kumbuka kama ungeomba mkopo kutoka taasisi fulani kwa mkatuba wa kurejesha Tshs 150,000 kwa mwezi ingekukuchukua zaidi ya miaka mitano kurejesha mkopo huo. Lakini wewe mwenyewe unajiwekea akiba kila mwezi ingawa ni kweli kwamba inahitaji uwe na nidhamu ya hali ya juu kujiwekea akiba bila kulazimishwa. Hata hivyo, unapaswa kusukumwa na hali halisi ya maendeleo unayoyataka. Je, unataka kuwa bilionea miaka kumi ijayo? Kama jibu ni ndiyo fanya uamuzi leo.

### **Mbinu Na. 06: Kuuza Mali ya thamani**

Kuna watu wanazo mali za thamani lakini wameendelea kuwa na maisha duni na ya kimaskini. Mali za thamani zaweza kuwa mifugo kama vile ng'ombe, kuku, mbuzi, nguruwe, shamba, nk. Kwa mfano, kama mtu ana ng'ombe wapatao 100 na bado anaishi maisha duni huyo atakuwa ni miuongoni mwa watu maskini siyo tu kifikra bali pia kiakili. Kama ng'ombe mmoja anauzwa Tshs 400,000 kwa nini usiuze ng'ombe 50 kwa ajili ya kupata Tshs 20,000,000 za kufanya mradi mwengine wenye kukupa faida zaidi kama ilivyofafanuliwa sura ya pili? Kama una shamba na liko eneo zuri kibashara na linauzika vizuri, kama shamba hilo siyo tegemeo lako kuu na la peke yake ulilonalo na ungependa kufanya mradi mwengine mkubwa wa kukupatia kipato kikubwa zaidi, ninakushauri uuze shamba lako. Shamba lako la ukubwa wa hekari tano unaweza kuliiza kwa zaidi ya Tshs 150,000,000 kama umepata mteja mzuri asiyekuwa na ubabaishaji. Kwa mfano kama shamba lako lipo kando ya njia kuu (highway) usiliuze kwa bei ndogo chini ya bei hiyo niliyoitaja. Matajiri wengi hupenda viwanja vilivyoko kando ya njia kuu (barabara kuu) ili wafanye biashara kubwa kama vile kuweka vituo vyta mafuta ya magari au kujenga majengo makubwa kama vile mahoteli na migahawa mikubwa. Kwa hiyo usije ukauza shamba lako kwa bei ndogo.

Unaweza kuuza mali ya thamani kama vile nyumba yako au gari lako la kutembelea. Jambo la muhimu ni kupiga hesabu ili kujiridhisha kwamba ukiiza gari au nyumba yako utapata mtaji wa kutosha na utatoka moja kwa moja. Kwa mfano unaweza kuuza gari lako kwa Tshs 8,000,000 au

10,000,000 au 15,000,000 kutegemeana na aina ya gari na ubora wake na ukafanya mradi mwингine wenyе uwezo mkubwa kukiungizia kipato cha zaidi ya Tshs 3,000,000 kwa mwezi. KUMBUKA: Unapaswa kutafakari kwa kina kwanza kabla ya kuuza mali yako ya thamani kama nyumba. Hata hivyo, nashauri mtu auze gari lake ili ajiokoe kiuchumi kwa sababu watu wengi hununua magari kwa sababu za kufuata mkumbo tu na fasheni ya siku hizi kwamba kuwa na gari ni ufahari. Ndiyo maana baada ya muda wengi hugundua kwamba hapakuwa na sababu ya kununua gari hasa baada ya kugundua kuwa kumiliki gari ni gharama. Ukweli ni kwamba kumiliki gari ni gharama sana tofauti na wengi wanavyodhani. Gharama kama mafuta ya kila siku, kodi ya mapato kila mwaka, bima ya gari kila mwaka, matengenezo ya mara kwa mara, nk ni baadhi ya gharama za kumiliki gari. Kutokana na hali kama hiyo, ushauri wa pekee kwa mtu mwenye gari lisiloingiza faida yoyote ni kuuza gari hilo na ili kupata mtaji wa kufanya jambo jipya lenye tija kifedha.

Kwa mfano, unaweza kuuza gari lako na ukafanya mradi wa ufgaji kuku wa mayai au kuku wa nyama na ukajipatia faida kubwa sana kuliko kuwa na gari ambalo halikuingizii hata senti kwa mwezi zaidi ya ufahari wa kulitembelea tu tena mitaani. Kusema ukweli haiingii akilini kuwa na gari la kutembelea wakati hauna kipato kikubwa cha kutosha mahitaji yako mengine yaliyo ya muhimu. Ni bora ukaliuza gari ukapata mtaji wa mradi uupendao. Gari la kutembelea linapaswa liwe nyenzo ya kazi zako ili kurahisisha shughuli zako zinazokuingizia kipato. Haifai Kununua gari kwa ajili ya kukatisha mitaani tu huku ukishindwa kumudu mahitaji yako muhimu kila siku.

## **Mbinu Na. 07: Changamkia Mikopo ya Serikali**

Watu wengi hawajui kwamba serikali hutoa mikopo kwa wajasiliamali na vikundi vya maendeleo. Kila Halmashauri hapa Tanzania hutenga fungu la bajeti ya kutoa mikopo kwa makundi ya wajasiriamali, vijana, wanawake na walemovu. Kama wewe ni kijana au mwanamke na unataka kuinuka kiuchumi na unao mradi wako ambao umeshauanzisha au unataka kuuanzisha, nenda kwenye ofisi za Halmashauri ya wilaya au manispaa yako kwenye idara ya maendeleo ya jamii ukapewe taarifa sahihi na

ujipatие mkopo wa riba nafuu. Nenda ukaonane na mkuu wa Idara hiyo au maafisa wa Idara hiyo upewe utaratibu wa kufanya mpaka upate mkopo wa mtaji wako. Unapaswa kwenda ukijua na kukumbuka kuwa dawa ya deni ni kulipa. Usiende kuomba mkopo kutoka serikalini au kwa mtu yejote kisha ukageuza mkopo huo kuwa ni msaada au ruzuku. Jipange vyema kabla ya kuchukua mkopo usije ukashindwa kurejesha mkopo uliopewa. Usichanganye mkopo na matatizo yako binafsi. Usitumie mkopo kutatua majanga ya magonjwa au misiba yako wala usitumie mkopo kupata raha au starehe zako. Ukipatwa na majanga ukiwa na mkopo, jitahidi usiwaze kwamba unazo fedha. Jiweke kwenye upande wa kutokuwa na pesa ili majanga hayo uyatatue kwa njia nyingine badala ya kutumia pesa ya mkopo wako.

Habari hii ya mikopo serikalini inawahu su watu wote wenye ulemavu, wanawake au vijana wajasiriamali wanaotamani kuinuka kiuchumi. Kama wewe ni mlemavu na unataka kufanya mradi wa ushonaji nguo, mradi wa ushonaji viatu, mradi wa duka nk; nenda haraka kwenye Halmashauri yako ufuatilie mkopo huo. Usiogope na kusema kwamba wanapeana wao wenyewe au kwamba ni mpaka uwe unamjua mtu yejote aliye huko kwenye ofisi za Halmashauri, bali wewe nenda tu umwone muhusika. Hakika utapata mkopo wako.

## **Mbinu Na. 08: Shiriki Shindano linalotoa Zawadi ya Kitita cha Pesa**

Kuna mashindano mengi yenyе tija. Mashindano yanayota zawadi ya kitita cha pesa kama yale ya MAISHA PLUS, RUKA JUU, BONGO STAR SEARCH, MISS TANZANIA, MISS UTALII, na mengine yanayofanana na mashindano hayo yanafaa sana kwani washiriki wake hupewa kitita cha pesa nyingi zinazoweza kumfanya mtu akainuka kiuchumi. Pamoja na kwamba mshindi huwa mmoja tu lakini pia mashindano mengi huwa yanatoa mshindi wa pili wa tatu hadi wa tano wanapewa zawadi ya kitita cha pesa.

Kwa mfano mashindano ambayo mshindi wa kwanza anapewa hadi Tshs 50,000,000 siyo mabaya ukishiriki kwani huwezi kujua huenda mshindi

akawa wewe unayesoma kitabu hiki. Utakuta mashindano kama hayo mshindi wa pili hadi wa tano wanapewa zawadi za thamani pamoja na pesa kulingana na shindano liliyopangwa ambapo wakati mwingine wanapewa hadi Tshs 5,000,000 kwa kupata ushindi huo. Kama mtu atashiriki shindano hilo akiwa amejiandaa kufanya mradi mmojawapo katika miradi ilioelezwa katika kitabu hiki, na kama atashinda na akafanya mradi mmojawapo, ni hakika mtu huyo atakuwa bilionea baada ya muda mfupi. Hata waandaaji wa shindano watajivunia kuwa na mshiriki kama huyo. Kama wewe hauna mtaji na unadhani unaweza kushiriki mashindano kama hayo unashauriwa uchangamkie fursa hiyo kila mara unapoisikia. Huenda wewe ukawa ndiye mshindi wa shindano hilo na ukajipatia mtaji wa kuingia katika vitabu nya historia ya watu walijirika na kuwa mabilionea.

### **Mbinu Na. 09: Anzisha Mradi Kidogo Kidogo**

Kuna watu wameweza kutajirika hadi kuwa mabilionea kwa kuanza na mtaji mdogo tu wa kuuza karanga mitaani au nyumba kwa nyumba. Kuna watu wametajirika sana mpaka wameweza kujenga siyo nyumba tu za kuishi bali majumba kwa kuuza kahawa tu. Nawafahamu vijiji na jijini Dar es salaam wapo wengi tu. Tembelea wauza kahawa wa Dar es salaam uwaulize walianza na mtaji kiasi gani. Wengi walianza kwa kutembeza kahawa mitaani na sasa walishatajirika wakaamua kuacha biashara hiyo baada ya kupata mitaji ya kuwawezesha kufanya miradi mingine ikiwemo nyumba za kupangisha.

Hoja yangu hapa ni kwamba siyo lazima usubiri upate pesa nyingi ndipo uanze mradi fulani. Kwa mfano kama mradi wote utagharimu kiasi cha Tshs 10,000,000 wewe waweza kuanza na hatua za mwanzo mpaka utakapofikia viwango nya juu. Kwa mfano lengo lako kama ni kufuga kuku wa kienyeji wapatao 3000 siyo lazima usubiri upate pesa ya kununua vifaranga wapatao 3000. Unaweza ukaanza na vifaranga 500 mwaka huu, mwaka ujao tena vifaranga 500 na baada ya miaka 6 ukawa tayari unafuga kuku wa kienyeji wapatao 3000. Kumbuka kuwa ufugaji wa kuku wa mayai wapatao 3000 ni mradi mkubwa sana wenye uwezo wa kukuingizia zaidi ya Tshs 600,000 kwa siku. Hii ni zaidi ya posho anayolipwa Mbunge kwa siku. Maelezo ya kina kuhusu mradi wa ufugaji kuku yanapatikana sura ya pili ya kitabu hiki.

Hali kadhalika kama unataka Kufuga ng'ombe, mbuzi, nguruwe, sungura, nk na ungetaka uwe mbuzi wapatao 500 kwenye shamba lako la mifugo, siyo lazima uanze na mbuzi wote 500 bali waweza kuanza na mbuzi 10, 50, 100, 200, 300 hadi 500 ndani ya miaka mitatu au kulingana na unavyofanikiwa au ulivyojipangia. Kwa kufanya hivyo waweza kutajirika sana hatua kwa hatua.

### **Mbinu Na. 10: Kopa Kutoka Mifuko ya Pensheni**

Kama wewe umeajiriwa au umejajiri na unachangia moja ya mifuko ya hifadhi ya jamii hapa nchini kama vile LAPF, PSPF, PPF, GEPF au NSSF na ungependa kuwa na biashara au miradi mingine zaidi ya kazi ulio nayo kwa sasa, unaweza kukopa kutoka mifuko hiyo. Hata hivyo kumbuka kuwa sharti kuu la mifuko hiyo lazima uwe mwanachama hai kwa kipindi kirefu ili uweze kukopeshwa. Mifuko kama LAPF na PSPF wanatoa mikopo ya riba nafuu sana kwa watumishi wanaokaribia kustaafu. Sharti lao lingine kuu ni lazima uwe umefikia umri wa miaka 55 ndipo unaweza kuchukua mkopo usiozidi nusu ya kiinua mgongo chako unachotrajia kulipwa utakapostaafu kazi rasmi. Kwa hiyo, kwa wale ambao tayari wana umri wa miaka 55 na wanachangia mifuko hiyo wanapaswa kuchangamkia fursa ya mikopo iliyopo kwenye mifuko ya LAPF na PSPF ili kujianaa na maisha ya izeeni baada ya kustaafu kwenye kazi za kuajiriwa. Mikopo hiyo kutoka kwenye mifuko hiyo inaweza kutumika kujenga nyumba za biashara kama vile; nyumba za kulala wageni (guest houses), nyumba za kupangisha (apartments), mabasi ya kubeba abiria, nk.

Kama unataka mtaji wa milioni 40 au zaidi lakini huwezi kupata pesa kama hiyo mahali popote kutokana na kukosa dhamana inayotosha kushawishi benki wakupe mkopo huo unaweza kuomba mkopo kutoka mfuko wa LAPF au PSPF kama umeshatimiza miaka 55 na kama unalenga kustaafu ukiwa na umri wa miaka 60 kwa lazima kwa mujibu wa sheria ya serikali. Kwa mfano kama wewe ni mchangiaji wa mfuko wa LAPF au PSPF na una mshahara unaozidi Tshs 1,500,000 kwa mwezi, na umechangia mfuko huo kwa zaidi ya miaka 25 unayo fursa nzuri ya kuweza kukopeshwa nusu ya kiinua mgongo chako ambapo kwa watu wenye kipato kama hicho kiiunua mgongo chao ni mara nyingi ni zaidi ya Tshs 80,000,000. Kwa

mujibu wa sera yao ya mikopo kwa watu wanaokaribia kustaafu unaweza kukopeshwa nusu ya kiiunua mgongo chako na ukapewa mkopo wa Tshs 40,000,000 ili utakapostaafu sasa ulipwe nusu iliyosalia. Hali kadhalika kwa wanaochangia PSPF nao wanalipwa kwa kanuni kama hiyo hiyo ya LAPF. Hata hivyo, karibu mifuko yote ya hifadhi ya jamii nchini (GEPF, PPF, NSSF, PSPF na LAPF) imeanzisha utaratibu wa kukopesha wanachama wake kuititia vyama nya akiba na mikopo yaani SACCOS.

Kwa hiyo kama wewe ni mwanachama wa moja ya mifuko hiyo, na ungependa kupata mkopo wa kutimiza ndoto yako ya utajiri tembelea ofisi za mifuko hiyo ili upate maelezo ya kutosha na uweze kupata mkopo unaoutaka. Mikopo hiyo kwa wanachama wa Mifuko ya hifadhi ya jamii ya (GEPF, LAPF, PSPF, NSSF na PPF) kuititia SACCOS hutolewa bila kujali umri wao kazini wala umri wao wa kuzaliwa. Hata hivyo, Kama wewe unachangia moja ya mifuko hiyo na ungetaka mkopo kutoka kwenye mfuko wako, ni lazima kwanza uwe mwanachama wa SACCOS iliyopo mahali pako pa kazi ili uweze kudhaminiwa na SACCOS inayotambuliwa na mwajiri wako wa sasa. Jambo zuri kwenye mifuko hiyo ni kwamba unaweza kukopeshwa kiasi chochote unachotaka kwa ajili ya kufanya miradi yako yoyote unayotaka kama ilivyoelezwa ndani ya kitabu hiki. Kwa maelezo zaidi tembelea ofisi za mfuko wako unaohusika.

## **SURA YA TANO**

### **MAWAZO POTOFU KUHUSU PESA NA UTAJIRI MKUBWA**

Katika kuhitimisha kitabu hiki ni vyema nikakueleza kwamba kamwe hautaweza kuwa bilionea kama bado unayo mawazo mabaya au potofu kuhusu kuwa bilionea. Katika sura hii mawazo mabovu kuhusu utajiri yanadodoswa ili uweze kuondokana nayo. Ukiweza kuondokana nayo ndipo utaweza kuchukua hatua thabiti za kuanza kutekeleza miradi kadhaa iliyotajwa katika kitabu hiki. Yafuatayo ni baadhi ya mawazo potofu yanayowazuia watanzania wengi kuwa mabilionea:

#### **1. Kuamini kwamba Pesa zina “Mashetani”**

Tanzania watu wanaoamini akilini mwao kwamba fedha zina mashetani ni wengi sana. Imani hii hutokana na jinsi watu wanavyobadilika tabia njema walizokwanazo walipokuwa bado masikini. Watu wengi wakiwa matajiri hugeuka kuwa watu wasiokuwa marafiki wa maskini tena, wasiojali tena watu masikini wala kutaka kutazamana na watu mafukara tena. Hali kama hii, huwafanya watu waone kuwa pesa ni ibilisi na shetani mkubwa. Kuna watu wanadiriki kusema “pesa ni ibilisi”. Wanaosema usemi huu ni wale hasa wanaoona watu wenyewe pesa wakifanya maasi na maovu mengi katika jamii hasa yale ya uonevu kwa watu wanyonge kama yatima, wajane na mafukara katika jamii. Aidha, wengi wanaoamini kwamba hakuna mtu awezaye kuwa na pesa nyingi sana na akawa na tabia njema. Imani hii imetokana na mazoea au uzoefu ambaow watu wanaushuhudia katika jamii wa watu matajiri kutokujali tena watu maskini. Hata hivyo, imani hii ni Potofu sana. Imani hii ni potofu kama zilivyo imani na mila nyingi potofu hapa Tanzania. Imani hii inapaswa kupigwa vita sana kama zinavyopigwa vita imani na mila potofu zingine zilizopo nchini. Mashirika yasiyo ya kiraia (NGOs), makanisani na misikitini, kwa kushirikiana na serikali ni vyema wakapiga vita imani hii potofu ili watanzania waweze kujkwamua kifedha.

Ukweli ni kwamba “fedha siyo ibilisi” kamwe. Nakuhakikishia kuwa Pesa ni malaika tu. Pesa ni malaika maalum awezaye kukuletea kila unachohitaji kila wakati kila mahali duniani. Pesa kwa tafsiri rahisi ni

kalatasi au madini yaliyochongwa vizuri yaliyokubaliwa na jamii husika au taifa fulani ili iwe kama chombo tu cha kutumia kubadilishana bidhaa au huduma bila usumbufu. Tafsiri nydingine tena tunaweza kusema kuwa pesa ni chombo tu kitumiwacho na watu kupima thamani ya huduma au bidhaa sokoni. Tunapaswa kuelewa kuwa fedha zimetengenezwa na mwanadamu mwenyewe na wala siyo ibilisi aliyezitengeneza. Mwanadamu ametengeneza fedha kwa ajili ya kurahisisha ubadilishanaji wa huduma na bidhaa kila mahali na kila wakati. Waswahili husema, “Ibilisi wa mtu ni mtu mwenyewe” na wala siyo fedha. Pesa kamwe haina Ibilisi hata kidogo ndani yake. Ni vyema ikaeleweka vyema kwamba ibilisi ni fikra zako mwenyewe na jinsi ulivyoolewa tangu utotoni na kundi la watu wanaokuzunguka hapo ulipo kila siku. Kundi la watu lilokuzunguka laweza kukufanya ukawa na vitendo vya kiibilisi hata kama hauna pesa. Na unaweza kuwa na pesa nydingi sana na bado usiwe na vitendo vya kishetani.

Sababu kuu inayowafanya watu wafanye maovu na maasi mengi mara tu wanapopata pesa nydingi ni uovu na uasi wanaokuwa nao miyoni mwao kabla ya kuwa na pesa nydingi na uovu huo hujidhihirisha au kujitokeza wazi katika jamii mtu apatapo pesa nydingi. Hii ni kwa sababu kila analolitamani moyoni mwake hujikuta anaweza kuliendea, kulifanya au kulinunua kwa sababu pesa anayo ya kufanya hivyo.

Ukitaka uwe bilionea achana na imani potofu kama hii kuhusu pesa. Unatakiwa uzione pesa kama rafiki yako wa karibu kuliko mtu ye yote hapa duniani. Zifanye pesa kuwa mama na baba yako. Je, mama na baba yako unaweza kuwaita ibilisi? La hasha. Unatakiwa pia uzione pesa kama nguo yako unayoipenda sana kati ya nguo zote ulizonazo. Je, kitu unachokipenda unaweza kukiita ibilisi? Pesa ukizifanya ziwe kama baba na mama yako huwezi kamwe kuwa mwepesi kuzitoa (pesa) kuzielekeza kwenye manunu au matumizi ambayo ni ya kiibilisi. Pesa ukiziona kuwa zina thamani utazitumia kwa maswala ya maana zaidi. Unatakiwa uzione pesa kuwa ni mpenzi wako mwaminifu anayeweza kukupatia kila kitu unachokihitaji moyoni mwako kila mahali tena wakati wowote.

Kama ungependa uwe bilionea, lazima pesa zako uzithamini. Ujue kuwa pesa ndiyo pekee inayotumika kubadilishana huduma au bidhaa zozote

---

utakazozitaka maishani mwako. Je, unataka kununua gari zuri sana kuliko zote zilizopo Tanzania? Je, unataka kujenga jumba kubwa na nzuri kuliko majumba yote yaliyopo Tanzania? Je, unataka uishi maisha ya ufahari zaidi ya mtu ye yote Tanzania? Kama jibu lako ni ndiyo, anayeweza kukupatia mambo yote hayo ni rafiki yako pekee, kipenzi wako wa kila hali. Rafiki yako huyo ni "FEDHA". Na wala siyo mwingine awaye ye yote. Je, hadi hapa utaendelea kumwita rafiki yako huyo kuwa ni "IBILISI?". Sidhani. Maana kama rafiki yako anaweza kukupa vitu vizuri sana kama hivyo halafu ukamwita "Ibilisi" hatakuwa rafiki yako tena. Ondokana na fikra potofu juu ya pesa ili uweze kuwa na pesa nyingi sana mikononi mwako, mifukoni mwako, kwenye akaunti zako za benki, kwenye miradi yako, kwa ndugu zako, na kwa kizazi chako chote hadi kwa wajukuu wa wajukuu zako.

## **2. Kuamini kwamba Pesa ni Chanzo cha Uovu**

Watanzania wengi bado ni waumini wa 'fedha ni chanzo cha maovu'. Mtu ye yote anayeamini kwamba fedha ndiyo chanzo cha maovu hawezi kujibidiisha kutafuta pesa nyingi sana. Ukiendelea kuamini hivyo, hautaweza kupata utajiri kamwe. Ili utajiri la zima uondokane na imani potofu kuwa chanzo cha maovu ni fedha. Unapaswa kuamini kuwa "fedha ndiyo chanzo cha mema yote". Ukiamini hivyo, fedha itakuwa jambo jema kwako. Utakuwa tayari kuona unapata pesa nyingi sana. Ninaposema pesa nyingi nadhani unanielewa kwamba sizungumzii milioni moja, milioni tano au kumi. Nazungumzia mabilioni ya fedha yawe chini ya miliki yako. Namaana kwamba kwenye akaunti zako zote za benki unamiliki pesa zenye tarakimu kuanzia kumi na kuendelea kwa mfano 1,000,000,000. Ninaposema pesa nyingi namaana ya pesa kuanzia shilingi bilioni moja, bilioni mbili, bilioni tano, bilioni kumi na kadhalika. Ili uweze kupata utajiri wa mabilioni ya pesa lazima kwanza "Uamini kwamba fedha ni takatifu na ni chanzo cha mambo mema duniani". Ukiamini kwamba fedha ni njema utazitafuta. Lakini ukiamini kuwa ni "uovu" hautazitafuta. Ukiendelea na mtazamo huo kwamba pesa ni chanzo cha uovu utashindwa kutafuta pesa hata kwa njia zilizo halali mbele ya jamii, serikali na dini yako.

### **3. Kuamini kwamba tajiri Hawezi kuurithi Ufalme wa Mungu**

Imani ina nguvu sana. Huwezi kuwa bilionea bila kuwa na imani. Ubilionea ni imani. Ukiamini inawezekana kuwa bilionea. Imani humfanya mtu aonekane jinsi alivyo. Watu wote unaowaona mitaani wakiwa maskini au matajiri kwa tafsiri yoyote ile, wako hivyo walivyo kwa sababu ya imani yao ama kwa Mungu au kwa vitu na pesa na mali.

Mpendwa msomaji wa kitabu hiki, napenda nikueleze kwamba hata kama wewe ungekuwa ni mcha Mungu sana yaani wewe ni mtakatifu kwa asilimia mia moja, huenda hautaweza kumzidi Nabii Ibrahimu kwa utakatifu aliokuwanao na utajiri mkubwa aliokuwa nao. Ukiyatilia hadithi ya Nabii Ibrahimu katika maandiko matakatifu utakuta kwamba alikuwa tajiri tena bilionea mkubwa sana aliyekuwa anamiliki mifugo ya kila aina, mashamba, fedha, dhahabu, vito vya thamani, na wafanyakazi wengi sana. Huyu alikuwa Nabii wa Mungu na hadi leo hii vizazi na vizazi wanaendelea kumheshimu kama Nabii na ucha Mungu wake aliokuwa nao pamoja na utajiri mkubwa aliokuwa nao. Kama Ibrahimu na manabii wengine waliokuwa matajiri waliingga peponi au Mbinguni, ni wazi kwamba hata wewe unayetafuta kuwa bilionea wa kitanzania, hakika utaurithi ufalme wa Mungu kama unayo imani hiyo hata ukiwa bilionea.

Ni vyema ukaelewa kwamba kama unaamini kuwa matajiri ni vigumu kuurithi ufalme wa Mungu; basi uelewe kuwa ni vigumu pia kwa masikini nao kuurithi ufalme huo. Kama wewe uko mahali wanapofundisha kwamba matajiri hawataurithi ufalme wa Mungu, unatakiwa kutafakari upya kwa jicho la upande wa pili ujiulize kama ni busara kuendelea kukaa mahali hapo.

Anza kuamini kwamba Matajiri mabilionea kama wewe, ni rahisi kuingia mbinguni. Tafuta sababu za kimaandiko kuthibitisha msimamo wako huo vilevile kama wale wanaotetea kwamba matajiri ni vigumu kuurithi ufalme wa Mungu. Kama wao wanatumia maandiko fulani kutetea msimamo wao, na wewe pia tumia maandiko hayo hayo kukataa mafundisho yao. Kama wewe ni msomaji wa maandiko ya Biblia Takatifu au Quran tukufu

nina hakika kuwa utapata maandiko lukuki yanayokutetea kusonga mbele mpaka uwe bilionea wa ukweli.

#### **4. Kuamini kwamba Huwezi kutajirika bila kutumia Uchawi, kafara au ndumba**

Uchawi na ushirikina umeendelea kupata waumini wengi siyo Tanzania tu bali karibu duniani kote. Wasomi kwa wasiokuwa wasomi, wengi wao wameendelea kusikika au wakionekana wakienda kwenye vibanda vya ndumba kupatia dawa za biashara au kufanya ushirikiana kila kona kunaposikika kwamba kuna mtalaam wa kuwezesha watu kutajirika. Kuna watu warajaribu hata kutoa kafara za watoto wao, wake zao, waume zao, au ndugu zao ili kupata utajiri na pesa. Ni bahati mbaya sana kwamba bado kuna watanzania wanaamini kwamba bila uchawi, ndumba au kafara hawawezi kufanikiwa kwenye miradi yao. Huu ni ufinyu wa fikra.

Mpendwa msomaji wangu, Ukweli utabaki kuwa, ndumba au uchawi haviwezi kuleta utajiri. Na kama una imani hiyo na umeshajiingiza huko, endelea kwa hasara yako (continue with that business at your own risks). Uchawi hauwezi kuleta maendeleo wala ubilionea unaoutaka. Ubilionea wa kweli huletwa na bidii ya kazi. Ubilionea huletwa kwa kufanya kazi kwa umakini, juhudhi, maarifa na kwa uchungu wa hali ya juu na wa dhati unaokusudia kujitoa katika umaskini na kuingia katika ulimwengu wa matajiri. Achana na fikra potofu, elekea kwenye ulimwengu mpya wa mabilionea. Achana na ushirikina. Acha kuroga bishara za wenzako. Acha kutoa kafara za watoto wako au mke wako. Achana na utamaduni wa kutafuta utajiri kwa kuititia damu za watu, utalaaniwa na kufa kifo cha aibu sana. Tafuta ubilionea kwa kufanya kazi hatua kwa hatua hadi uwe bilionea. Acha uchu wa mali za haraka.

#### **5. Kuamini kwamba Pesa hutoka kwa shetani**

Watanzania wengi bado wanaamini kwamba kuna kundi la watu walioumbwa wakiwa matajiri zaidi. Kuna watu wanaamini kwamba ukijiunga na makundi kama ya “freemason” ndipo unakuwa bilionea. Wanaamini kwamba fedha ni mali ya shetani na kwa hiyo ukitaka upate pesa nyingi lazima ujiunge na makundi kama hayo ndipo upate ubilionea. Huu ni uongo mkubwa.

Mpendwa msomaji, napenda kukuhakikishia kwamba fedha haitoki kwa mashetani. Fedha hutoka Benki Kuu ya nchi husika na kuingizwa kwenye mzunguko wa fedha kupitia benki za biashara nchini. Hakuna fedha yoyote ni mali ya mashetani. Fedha zote ni mali ya Benki Kuu ya Taifa. Mashetani au mafreemason hawana fedha yoyote wanayomiliki. Kamwe fedha hazitoki kwa shetani bali Benki Kuu. Fanya bidii sana uzipate fedha nyngi kwa njia ya ukweli na sahihi na makini na halali kwa mujibu wa sheria za nchi. Acha ndoto za alinacha. Acha ndoto za Pwagu na Pwaguzi. Fanya kazi kwa weledi na umakini mkubwa na fedha zote zitakufuata popote ulipo.

## **6. Kufikiri kwamba kuna watu waliumbwaa wawe Matajiri**

Ukitaka uwe bilionea achana na tabia ya kufikiri kwamba kuna watu waliumbwaa toka matumboni mwa mama zao wawe mabilionea. Bilionea wengi sana wanaweza kutokea Tanzania kama watu wengi wataacha kufikiri upotofu na kuzama kwenye fikra potofu kama hizi. Pesa nyngi zinakungoja kila kona hapo ulipo. Unaweza ukawa bilionea wa ukweli kama tu utafuata kanuni za kuwa bilionea ambazo nyngi zimefafanuliwa sana hapo awali katika kitabu hiki. Hakuna aliyeumbwa akiwa bilionea. Watu wote waliumbwaa tumboni mwa mama zao na walizaliwa wakiwa uchi kama wewe. Kama wao wameweza kuwa mamilionea na mabilionea kwa nini wewe ushindwe? Mabilionea wote wana mikono miwili, miguu miwili, macho mawili, kichwa kimoja, nk. Kwa nini wafanikiwe kuwa mamilionea na mabilionea lakini wewe ushindwe? Wao wana kitu gani ambacho wewe hunaa?

## **7. Kufikiri kwamba Dunia inakaribia kufika Mwisho**

Kuna watanzania wengi ambao kutokana na mahubiri ya imani zao za dini wanaamini kwamba dunia inakaribia kufika ukomo yaani kiyama. Wanaamini kwamba hapa duniani hakuna haja ya kutafuta mali kwani wakati wowote dunia itakwisha. Fikra hizi hazina ukweli. Ni vyema ukaammini kwamba dunia haijulikani ni lini itakwisha kamwe. Maandiko mengine husema, hakuna ajuaye siku wala saa. Mimi nakushauri utafute utajiri mkubwa sana kama vile dunia haitakwisha kabisa. Fanya kazi kwa

bidii sana na utajirike sana kama vile hakuna kiyama kabisa itakayotokea, lakini kama wewe unaamini basi mwamini Mungu kama vile kiyama inakuja kesho. Ni afadhali kiyama ikukute kwenye maisha bora na ya amani ukiwa tajiri bilionea kuliko kiyama ikukute ukiwa fukara na masikini asiyekuwa na chochote.

## **8. Kufikiri kwamba Utajiri ni Bahati tu.**

Achana na fikra potofu kwamba utajiri ni bahati. Achana na kucheza michezo ya kubahatisha badala yake, fanya kazi kwa bidii na hakika utapata utajiri mkubwa. Ukweli ni kwamba kila mtu anaweza kuwa tajiri milionea au bilionea. Kwa nchi kama Tanzania ambayo ina amani kisiasa na kijamii kama ilivyo sasa, ni dhahiri kabisa kwamba kila mmoja anaweza kuwa milionea hadi bilionea. Ni aibu sana kwa watanzania kuendelea kuwa masikini wanaopata Tshs 1600 tu kwa siku yaani dola moja kwa siku. Kwa nini uendelee kuamini kuwa utajiri ni bahati nasibu wakati ukweli ni kwamba maarifa, kazi na bidii ndiyo siri kuu ya ubilionea. Hakika nakwambia unaweza kupata zaidi ya Tshs 200,000 kwa siku kama ukiamua leo. Soma tena maelezo ya miradi yote niliyioieleza kwenye sura ya pili. Kama umezoea kuishi maisha ya kubahatisha, unakula kwa kubahatisha, sasa sema baaasi imetosha.

## **9. Kuogopa kurogwa kama utakuwa na Pesa Nyingi**

Fikra nyiningine potofu inayowasumbua watanzania, ni hofu ya kurogwa. Kama hapo ulipo wewe huna hofu ya kurogwa kwa mafanikio uliyokwishapata, uelewe kwamba kuna watu huko wanakoishi, wanaishi kwa hofu ya kurogwa. Wanaogopa kurogwa kila siku. Wanalazimika kufanya mambo kwa kujificha au kwa kutotaka wajulikane kwani wakijulikana tu watarogwa.

Ukweli ni kwamba kama uchawi upo au haupo hiyo siyo hoja hapa. Lakini mimi nakushauri tu uhakikishe wewe hujihusishi na ushirikina kamwe. Nashauri hivyo kwa sababu usoefu unaoelezwa na watu wengi ni kwamba ukiishajihuisha na maswala ya ushirikina tu huwa ndio mwanzo wa wewe kupata majoribu ya kishirikina na hatimaye kama wewe siyo mtalaam au mwenye ufundi wa hali ya juu hapo sasa ndipo utarogwa. Ni nadra sana kwa mtu ambaye hajihusishi na ushirikina kurogwa na akarogeka.

Wanaorogwa ni wale wanaoroga pia. Kwa mujibu wa shuhuda mbalimbali na uzoefu wangu, naamini kwamba kama wewe hujawahi kujihusisha na uchawi au ushirikina hautarogwa kamwe.

Wewe tafuta mali na utajiri wote kwa kadri unavyoweza. Tafuta kuwa bilionea na huo utajiri wote ambao hakuna mtu atakayeupata asipofanya kazi kwa bidii kama wewe. Acha woga wa kurogwa. Wewe ni mtoto wa Mungu na kamwe huwezi kurogeka kama wewe mwenyewe hujawahi kujaribu kuroga watu wengine.

10. Kuwaza kupata pesa kidogo badala ya Mabilioni Ukitaka kuwa bilionea unapaswa kuwa na mawazo ya kupata pesa katika kiwango cha mabilioni. Usiwaze kuwa na maelfu au malaki ya pesa. Kwa mfano kama wewe unafanya mradi wako unaingiza faida ya Tshs 200,000 kwa siku yaani Tshs 6,000,000 kwa mwezi hebu anza kuwaza kutoka kiwango hicho cha milioni sita kwa mwezi na uvuke hadi milioni kumi kwa mwezi. Ukishafika kwenye kipato cha Milioni 10 kwa mwezi, sasa anza kutamani kuwa na kipato cha Tshs 30,000,000 kwa mwezi au endelea kuwaza kuwa na kipato cha Tshs 100,000,000 kwa mwezi hadi Tshs 1,000,000,000 kwa mwezi. Hili linawezekana ukiamua kwamba sasa umaskini baaasi. Hebu fikiria tajiri mmoja anaitwa Said Bakhresa ambaye sasa ameanzisha mradi wa Azam Tv kwa kutumia ving'amuzi vya setelite ambapo kila mteja analipa Tshs 12,500 kwa mwezi. Hebu tufanye kwamba kwa nchi nzima atapata wateja wapatao laki mbili Tanzania bara na visiwani. Sasa kwa mwezi wote wakilipa gharama ya ving'amuzi kwa bei hiyo ya Tshs 12,500 atapata kiasi gani? Hebu tazama hesabu hii ya fedha atakayoipata; Tshs 12,500 x 200,000 = Tshs 2,500,000,000.00 Utaona kwamba kwa mwezi anatarajia kukusanya shilingi bilioni mbili na nusu. Lakini ukumbuke kwamba anayo miradi mingi sana huyu bwana na kwa siku huenda anakusanya zaidi ya bilioni kumi kutoka kwenye vyanzo vya miradi yake yote. Yeye kutamka neno "shilingi bilioni" kila siku ni jambo la kawaida sana kwake. Kwa nini wewe ushindwe? Kwa nini Bakhresa ameweza? Yeye ameweza kwa sababu kila siku anawaza kumiliki mabilioni ya pesa.

## **11. Kuamini kuwa“Aliyekupa wewe ndiye kaninyima mimi”**

Kuna watu humsingizia Mungu kwamba hawajaweza kupata utajiri na fedha nyingi kwa sababu Mungu amependa wawe hivyo walivyo kifedha. Watu wengi huendekeza misemo mibovu kama vile: “Aliyekupa wewe ndiye kaninyima mimi”. Misemo kama hii inamfanya mtu aridhike na hali yake kifedha huku wenzake wasioridhika na hali walizonazo wakizidi kupanda juu kifedha. Msemo huu unadumaza akili hadi inashindwa kuwaza kwa kina juu ya kipi afanye ili kujikwamua kifedha. Msemo huu, unawafanya watu waamini kwamba Mungu atawapatia fedha kwa miujiza badala ya kufanya kazi kwa bidii na maarifa wanaishia kusema na kuamini kwamba, “aliyempatia fedha nyingi mtu fulani ndiye aliyemnyima ye ye asiye kuwa na fedha”.

Kuna misemo mingi mingine ambayo imeendelea kudumaza watu wengi sana kifedha na kiuchumi. Misemo kama vile: “aliyeko juu mngojee chini”. Msemo huu nao ni hatari sana kwa uchumi wako. Vijana wa kisasa husema, “aliyeko juu mfuate huko huko aliko” wakimaanisha kwamba ukisubiri mtu aliye tajiri arudi chini ndipo wewe uweze kupanda juu kifedha utachoka sana. Msemo mwininge mbaya ni kama huu: “haraka haraka haina Baraka”. Msemo huu na mingine inayofanana na hii ni hatarishi sana kwa ustawi wako kifedha na kiuchumi. Ni vyema ukajiondoa kwenye misemo mibovu kama hii ili uweze kuinuka kiuchumi na kifedha.

## HITIMISHO

Katika kitabu hiki, tumeona mambo mengi sana yanayoweza kukubadilisha maisha yako ukiamua sasa hivi. Kubadilika kimapato hakuwezekani usipoamua leo. Maendeleo yako ya hali ya juu kifedha na kiuchumi utakayokuwa nayo miaka 10 ijayo unayaamua leo. Amua leo kuwa na kipato cha Tshs 1,000,000 kwa siku ili miaka 5 ijayo uwe tayari unapata kipato hicho kwa siku.

Katika kitabu hiki tumetoa mifano mingi sana ya waliofanikiwa kifedha. Hakikisha ya kwamba sasa unaanza kutajwa mionganini mwa watanzania mabilionea waliofanikiwa.

Aidha, Kitabu hiki kimeorodhesha zaidi ya miradi 60 ambayo ukifanya hautaendelea kuwa maskini wa kipato. Utakuwa bilionea. Ukiamua kuanza mradi mmojawapo leo hakika baada ya miaka mitano utakuwa mtu wa tofauti kabisa. Kumiliki 1,000,000,000 (bilioni moja) kwa mwezi au kwa mwaka inawezekana kabisa.

Ndani ya kitabu hiki utapata kujua tabia na miiko ya mabilionea wengi duniani. Utajua miiko ya matajiri ili uweze kudumu na utajiri wako miaka na miaka hadi kwa wajukuu wa wajukuu wako kizazi hadi cha nne. Fuata nyota za matajiri ili uendelee kuwa tajiri. Achana na nyota za wanajimu na washirikina badala yake fuata roho ya uchaji wa Mungu na kuwaheshimu watu wote wanyonge kwa wasio wanyonge. Saidia wanyonge kila Mwaka kama siyo kila mwezi. Ukiufata kanuni hizo hakika wewe utajiri wako hautakuwa na mwisho kamwe.

Kama utaondokana na fikra mgando na zisizo na uhai wala uendelevu, hakika utapata utajiri mkubwa sana hapo hapo ulipo iwe kijijini au mijini, manispaa au jijini. Epuka kuwaza pesa kidogo. Waza pesa nydingi sana. Fanya kazi kwa bidii, epuka kutafuta njia za mkato kuuendea ubilionea. Epuka utapeli na ujambazi au uhuni na wizi wa fedha za mali ya umma. Fanya kazi zako halali na za ukweli ili uwe bilionea wa ukweli. Fikra potofu na danganyifu za wizi na udokoaji hakika hazitakufaa kamwe na zitakupeleka pasipostahili.

Kwa kusoma kitabu hiki nina hakika utapata mbinu za kujipatia mtaji ikiwemo kuchangamkia mikopo itolewayo na mabenki, halmashauri zetu na serikali. Usisubiri kuanza kesho. Anza leo leo. Usingoje kesho ili kuanza miradi yako ya kuelekea kwenye ubilionea. Anza safari yako leo na usingoje kesho. Usisubiri siku utakapopata pesa nyngi ndipo uanze. Futa historia ya umaskini kwako na kwa wajukuu wako.

## KUHUSU MWANDISHI

Venerando J. Milinga, Mwandishi wa kitabu hiki alizaliwa katika kijiji cha Kasumo wilayani Kasulu mkoani Kigoma nchini Tanzania miaka 42 iliyopita. Kwa sasa ni mfanyakazi katika shirika la hifadhi ya jamii la LAPF linaloshughulika na kulipa mafao kwa wafanyakazi wa sekta binafsi na walioajiriwa serikalini. Akiwa mfanyakazi wa LAPF, amekuwa akifanya kazi za kufundisha wafanyakazi wa serikali na sekta binafsi kuhusu maswala yote yahusuyo Hifadhi ya jamii, biashara na ujasiriamali tangu Mwaka 2005. Ameweza kuzunguka katika maeneo mengi ya nchi ya Tanzania kwa ajili ya kutoa semina mbalimbali. Mikoa mingi aliyotembelea ni ile iliyoko katika kanda ya ziwa Victoria. Katika semina zake amekuwa akiwafundisha wafanyakazi mbinu mbalimbali za kuijandaa na maisha ya uzeeni. Ameshafundisha semina mbalimbali za hifadhi ya jamii, ujasiriamali na miradi ya maendeleo katika halmashauri za wilaya kama vile; Tarime, Musoma, Serengeti, Bukoba, Karagwe, Misenyi, Shinyanga, Kahama, Kishapu, Ngara, Biharamulo, Meatu, Bariadi, Kibondo, Kasulu na Kigoma. Aidha, ameshafundisha katika Hospitali teule za Nyakahanga DDH, Bunda DDH, Serengeti DDH, Kigoma Ujiji CDH, na St. Augustine University of Tanzania(SAUT).

Mwandishi ni mahiri sana katika maswala ya Hifadhi ya Jamii, maendeleo ya jamii, uchumi na ujasirimali. Mwaka 2012 Oktoba, alihitimu Shahada ya Uzamili katika maendeleo ya jamii na Uchumi katika Chuo Kikuu huria cha Tanzania (Masters in Community Economics Development) ambapo kabla ya hapo mwaka 2002 alihitimu Stashahada ya Juu katika fani ya Hifadhi ya Jamii kutoka chuo cha Usimamizi wa Fedha (Advanced Diploma in Social Security Administration) kilichoko jijini Dar es Salaam.

Mwandishi ana mke na watoto wawili. Anamiliki kampuni binafsi ya “Remili Enterprises Company” (REC) inayojishughulisha na utungaji na usambazaji wa vitabu pamoja na kuendesha semina mbalimbali za ujasiliamali. Aidha, anamiliki kampuni tanzu na REC inayojishughulisha na ufugaji wa kuku wa kisasa wa mayai inayoitwa “Remili Interchick Investment”.

## **Juma Venerando Milinga**

(Masters in Community Economics Development- OUT 2012)

(Advanced Diploma in Social Security Administration- IFM 2002)

**All rights reserved, 2014**



## REJEA

- Beckwith, A. 2013: Goal Setting For Success. Imechukuliwa kutoka mtandao wa: [www.Bookboon.com](http://www.Bookboon.com)
- Carson, Ben. 1990: Gifted Hands, Zondervan, USA.
- Carson, Ben. 1990: Think Big; Zondervan, USA.
- Fridson, M. 2013: How to be a Billionaire – Proven Strategies From The Titans of Wealth: Imechukuliwa Kutoka mtandao wa: [www.summaries.com](http://www.summaries.com)
- .
- Hale, M. 2008: Become Rich By Making The Most of Your Money, Published in Kenya.
- Kiyosaki R. T, 2000: Guide to Investing: What Rich people invest in and Poor people do not, Business Plus, New York.
- Kiyosaki, R.T. 2002: Rich Dad Poor Dad, New York, USA.
- Kiyosaki, R.T. et all, 2010: The Business of The 21<sup>st</sup> Century: Dreambuilders, USA.
- Meade, W. 2012: The Little Black Book of Billionaire's Secrets, Logic Fund Management, Inc.
- Mwang'amba, J. 2011: Mambo 10 ya Kuzingatia Kabla ya Kuacha Kazi. Street University DVD Video Vol.1, Global Publishers Ltd, Dar es salaam.
- Nangoli, C.M, 2004: How to Make Money, Holy Star Books, USA.
- Nyabongo J, 2013: Customer Care, Do's and Don'ts: Service Excellence Publishers Ltd. Dar es Salaam.
- Pensioners Union of Tanzania, 2009: Retirement Benefits in Tanzania, Dar es salaam.
- Shigongo,E.J, 2011: Jinsi ya Kuongoza Biashara Kutoka Sifuri Hadi Mabilioni; Street University DVD Video, Global Publishers Ltd, Dar es salaam.
- Tracy, Brian. 2014: 21 Success Secrets of Self-made Millionaires. Imechukuliwa kutoka mtandao wa [www.empoweronline.com](http://www.empoweronline.com).
- Zephania, K.I, 2009: Jinsi ya Kupata Pesa: Victoria Promotional Centre, Mwanza.